Ksh 3000/5 1

# TATHMINI YA MTALAA WA ISIMUJAMII WA SHULE ZA UPILI NCHINI KENYA

**TASNIFU YA**

**NGUGI MWANGI BONIFACE**

**ILIYOTOLEWA KWA MADHUMUNI YA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI**

**CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

Ngugi,Mwangi Boniface
*Tathmini ya mtalaa wa isimujamii wa shule*
2009/333653

**2008**

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika Chuo Kikuu kingine chochote.

______________________ Tarehe: 21-11-08

**NGUGI MWANGI BONIFACE**
**(MTAHINIWA)**

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii wa Chuo Kikuu.

______________________ Tarehe: 24/11/08

**DKT. CHARLOTTE ALI RYANGA**
**IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA ZA KIAFRIKA**
**CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

______________________ Tarehe: 25/11/2008

**DKT. CLARA MOMANYI**
**IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA ZA KIAFRIKA**
**CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

# TABARUKU

Kwa mamangu mpendwa, Esther Wangari Ngugi. Ulijinyima mengi ili kunisomesha nawe utayapata matunda ya kazi yako.

Kwa marehemu babangu, Zakariah Ngugi Chacha. Bidii zake hazikupotea.

Kwa mke wangu mpendwa, Rose Waithera Mwangi. Ulihakikisha nimeamka alfajiri niendelee na kazi hii licha ya uhisani wako. Tutasafiri pamoja katika mkondo wa maisha.

Kwa binti yangu, Yvonne Wangari Mwangi. Ulivumilia mengi baba na mama walipokuwa wanasoma nawe hutajuta.

## SHUKRANI

Mosi namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo wa kusoma na kuikamilisha kazi hii. Nawashukuru sana wasimamizi wangu Dkt. C.W. Ryanga na Dkt. C. Momanyi kwa uongozi wao hadi nikaukamilisha utafiti huu. Mlinishauri bila kukawia nami nikaikamilisha kazi hii kwa muda uliofaa. Mungu awabariki.

Shukrani zangu pia ni kwa wahadhiri wote wa Idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika kwa kunifundisha na kunielekeza vizuri katika kozi hii. Safari ilionekana ndefu, yenye mabonde na milima lakini kwa juhudi zenu ikawa rahisi. Nikayakamilisha masomo yangu bila doa wala ngoa. Nawaombea maisha yenye mafanikio.

Siwezi kuwasahau wanafunzi wenzangu, **Njurai**, **Hellen**, **Nakhisa**, **Muange**, **Muinde** na **Mumbua**. Darasani na maktabani tulisumbuka pamoja. Ushirikiano wenu ulikuwa nguzo imara. Nawashukuru nyote.

Chuo Kikuu cha Kenyatta chastahili shukrani nyingi kwa kugharimia sehemu ya masomo yangu kupitia idara ya Kiswahili. Bw. J. Mugambi, Mkuu wa Idara anastahili pongezi kwa kunishauri na kunielekeza kuhusu jambo hili. Tume ya Kuajiri Walimu (T.S.C.) inastahili pia pongezi kwa kunipa likizo ili niendelee na masomo yangu.

Asanteni walimu wa shule za upili za Wilaya ya Thika; Mang'u, Gachororo, Thika, Chania, St. Teresa, MaryHill, Gatanga, Kanunga na Nyaga. Bila nyinyi, nisingeweza

kukusanya data ya utafiti huu. Kadhalika, naishukuru Taasisi ya Elimu Kenya kupitia Bw. Waititu kwa kunipa habari nilizohitaji kuhusu utafiti huu.

Wahazili katika Idara ya Kiswahili walichangia sana utafiti huu hasa Anne Kimotho ambaye kwa kujitolea kwingi, aliipiga chapa kazi hii. Bw. John Waweru wa Kiswahili Resource Centre (K.R.C.) alinisaidia sana kwa makala na marejeleo ya kazi hii. Shukrani sana na Mungu awabariki.

Shukrani za kipekee zimwendee mke wangu, Rose, kwa mchango wake katika kufanikisha kazi hii. Pamoja na binti yetu Yvonne, walivumilia mengi mpaka nikakamilisha masomo yangu.

Namshukuru mamangu, Wangari, ambaye alijikakamua kunisomesha baada ya kuachwa na Marehemu babangu. Shukrani nyingi pia ni kwa ndugu zangu Muturi, Irungu na Josphine ambao walinipa shime ya kuendelea na masomo yangu. Sitawasahau marafiki zangu Mbethe na Maina kwa mawaidha yao mambo yaliponilemea.

# IKISIRI

Utafiti huu umeshughulikia kutathmini mtalaa wa Isimujamii wa shule za upili nchini Kenya. Utafiti huu ulidhamiria kutathmini na kuimarisha mtalaa wa Isimujamii katika lugha ya Kiswahili kama chombo cha mawasiliano kwa kuongozwa na misingi ya nadharia za ufundishaji wa Lugha ya Pili na Isimujamii. Utafiti huu pia ulibainisha changamoto zinazowakumba walimu wanapofundisha Isimujamii iliyojumuishwa katika silabasi ya mtalaa wa sasa. Wilaya ya Thika ilichaguliwa kama eneo la utafiti kwa vile ina shule za Taifa, Mkoa, Wilaya na za Kibinafsi zilizohitajika kufanyia utafiti. Ukusanyaji wa data ulifanywa kupitia mahojiano ya walimu, watalaamu wa elimu na kuchunguza ratiba ya vipindi vya masomo kutoka kidato cha kwanza hadi cha nne. Dhana ya mitalaa pamoja na uandalizi wa mitalaa imepitiwa kwa vile ni muhimu katika utekelezaji wa mtalaa wowote mpya. Maoni ya walimu na wakuza mitalaa kuhusu dhana ya mtalaa na maandalizi yake yamewasilishwa kwa njia ya mjadala. Vile vile, uchanganuzi wa maoni ya walimu na wakuza mitalaa kuhusu mawanda ya Isimujamii umeshughulikiwa. Hatimaye matokeo ya utafiti huu pamoja na mapendekezo yameshughulikiwa ambapo imebainika kuwa, mtalaa wa Isimujamii una udhaifu katika kumwongoza mwalimu ili aimarishe kiwango cha mawasiliano cha wanafunzi. Walimu wengi wanasisitiza miundo ya lugha badala ya uamilifu wa lugha. Jambo jingine linalotinga utekelezaji wa mtalaa wa Isimujamii ni ukosefu wa vifaa vya kufundishia. Utafiti huu utafaidi sera na upangaji wa lugha. Ili kuimarisha uhusiano mwema katika jamii yenye lugha nyingi, lugha moja inahitajika. Lugha kama hiyo itapatikana kwa kuifunza shuleni.



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

# YALIYOMO


| | | Ukurasa |
|---|---|---|
| | **Ungamo** | ii |
| | **Tabaruku** | iii |
| | **Shukrani** | iv |
| | **Ikisiri** | vi |
| | **Yaliyomo** | viii |
| | **Ufafanuzi wa dhana muhimu na vifupisho** | xi |
| | **SURA YA KWANZA** | 1 |
| **1.0** | **Utangulizi** | 1 |
| **1.1** | **Swala la Utafiti** | 4 |
| **1.2** | **Maswali ya Utafiti** | 5 |
| **1.3** | **Malengo ya Utafiti** | 6 |
| **1.4** | **Tahadhania** | 6 |
| **1.5** | **Sababu za Kuchagua Mada** | 6 |
| **1.6** | **Upeo na Mipaka ya Utafiti** | 9 |
| **1.7** | **Yaliyoandikwa kuhusu Mada** | 10 |
| | 1.7.1 Maandishi ya Kijumla kuhusu Isimujamii | 10 |
| | 1.7.2 Tafiti Bayana kuhusu Ufundishaji wa Kiswahili Shuleni | 12 |
| | 1.7.3 Matumizi ya Mitalaa katika Elimu | 14 |
| **1.8** | **Misingi ya Nadharia** | 15 |
| | 1.8.1. Nadharia ya Ufundishaji wa Lugha ya Pili | 15 |
| | 1.8.1.1 Nadharia ya Lugha ya Mawasiliano | 16 |
| | 1.8.2 Nadharia ya Isimujamii | 20 |
| **1.9** | **Mbinu za Utafiti** | 23 |
| | 1.9.1 Ukusanyaji wa Data | 23 |
| | 1.9.1.1 Utafiti Maktabani | 23 |

1.9.1.2 Utafiti Nyanjani ........................................ 24
1.9.2 Watafitiwa ........................................ 24
1.9.3 Uchanganuzi wa Data ........................................ 26

**SURAYA PILI** ........................................ 27
**DHANA YA MITAALA NA UKUZAJI WAKE: SOMO LA LUGHA**
**2.0 Utangulizi** ........................................ 27
**2.1 Maana ya Mtalaa** ........................................ 28
**2.2 Malengo ya Elimu Nchini Kenya** ........................................ 30
**2.3 Hatua za Kuandaa Mitalaa** ........................................ 34
2.3.1 Kutathmini Mahitaji ........................................ 35
2.3.2 Uundaji wa Mradi wa Mtalaa ........................................ 37
2.3.3 Upangaji wa Mtalaa ........................................ 38
2.3.4 Maandalizi ya Zana za Kufundishia ........................................ 38
2.3.5 Majaribio ........................................ 40
2.3.6 Utekelezaji ........................................ 42
2.3.7 Tathmini ........................................ 43
**2.4 Muhtasari** ........................................ 49

**SURA YA TATU** ........................................ 51
**MAONI YA WALIMU NA WAKUZA MITALAA KUHUSU DHANA YA MTALAA NA MAANDALIZI YAKE**
**3.0 Utangulizi** ........................................ 51
**3.1 Dhana ya Mtalaa na Hatua za Kuuandaa** ........................................ 52
**3.2 Maandalizi ya Walimu** ........................................ 65
**3.3 Vifaa na Vitabu vya Kufundishia** ........................................ 69
**3.4 Njia za Kufundishia** ........................................ 71
**3.5 Muda na Majukumu ya Walimu** ........................................ 71

**3.6 Muhtasari** ........................................................................ 73

**SURA YA NNE** ........................................................................ 76

**UCHANGANUZI WA MAONI YA WALIMU NA WAKUZA MITALAA KUHUSU MAWANDA YA ISIMUJAMII KATIKA SHULE ZA UPILI**

**4.0 Utangulizi** ........................................................................ 76

**4.1 Yaliyomo kwenye Silabasi** ........................................................ 79

4.1.1 Sifa za Matumizi ya Lugha katika Miktadha Mbalimbali ...... 80

4.1.2 Sajili za Lugha ........................................................ 81

**4.2 Maoni ya Walimu kuhusu yaliyomo kwenye Silabasi** .............. 85

**4.3 Maoni ya Wakuza Mitalaa kuhusu yaliyomo kwenye Silabasi** ... 95

**4.4 Ubora na Udhaifu wa Mtalaa wa Isimujamii** .................... 98

**4.5 Mapendekezo ya Walimu kuhusu Uboreshaji wa Mtalaa wa Isimujamii wa Shule za Upili Nchini Kenya** ........................ 104

4.5.1 Baraza la Mitihani Kenya (KNEC) ............................ 104

4.5.2 Ualimu na Vyuo vya Walimu Nchini ......................... 106

4.5.3 Wazazi ........................................................ 110

4.5.4 Kamati ya Chama cha Wazazi ................................. 111

4.5.5 Udhibiti wa Ubora wa Elimu ................................. 111

**4.6 Muhtasari** ........................................................................ 111

**SURA YA TANO** ........................................................................ 116

**MUHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO**

**5.0 Utangulizi** ........................................................................ 116

**5.1 Muhtasari** ........................................................................ 116

**5.2 Matokeo na Hitimisho la Utafiti** ........................................ 119

**5.3 Mapendekezo** ........................................................................ 128

**Marejeleo** ........................................................................ 133
**Kiambatisho I** ................................................................. 138
**Kiambatisho II** ................................................................ 141

## UFAFANUZI WA ISTILAHI MUHIMU NA VIFUPISHO

**Jamiilugha** : Ni kundi la watu ambao wanajulikana kuzungumza na kujimudu katika shughuli zao kwa kutumia lugha moja.

**L1** : Lugha ya kwanza.

**L2** : Lugha ya pili.

**Sarufi Zalishi** : Nadharia ya Chomsky inayotazama lugha kama mfumo wa ujuzi uliojisawiri akilini mwa msemaji. Ujuzi huu huitwa umilisi lugha.

**Pragmatiki** : Huu ni uchunguzi wa maana isiyo wazi. Aidha, ni jinsi tunavyoweza kutambua maana iliyokusudiwa hata kama haikusemwa waziwazi.

**NPA** : New Primary Approach.

**Umilisi Mawasiliano**: Ujuzi wa vikwazo vya kijamii unaomfanikisha msemaji katika kutumia lugha kwa njia ya kuridhisha na kufurahisha.

ɣ : Ishara ya kifonetiki ya sauti **gh**.

Mtalaa : Mafunzo ya masomo ya kujiendeleza.

# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

Wataalamu wa mitaala kama vile Oluoch (2002), Okech na Asiachi (1992) wanaafikiana kuwa mtalaa ni juhudi katika taasisi za elimu zitumikazo kuwaandaa wanafunzi katika masomo. Wakuza mitalaa wanakubaliana kuwa mitalaa ni yale yote yanayopangwa ili kuwawezesha wanafunzi kuwa na maarifa, ujuzi na mielekeo inayofaa kuhusu maisha (Taz. Shiundu na Omulando (1992), Benaars, Otiende na Boisvert (1994) na Hawes (1979). Taasisi ya Elimu Kenya (K.I.E.) ndiyo yenye jukumu la kuandaa na kusambaza mitalaa katika taasisi mbalimbali za elimu nchini Kenya.

Mitalaa inapotayarishwa, huhifadhiwa na kusambazwa kwa walimu kwa njia ya silabasi, miongozo ya walimu na ratiba ya kazi za walimu. Mapitio ya silabasi si tukio jipya. Katika nchi zote, mabadiliko katika mitalaa hutokea mara kwa mara kutegemea mpito wa wakati na mahitaji. Nchini Kenya, mfumo mzima wa elimu ulibadilishwa kutoka 7-4-2-3 hadi 8-4-4 mwaka 1984 kufuatia mapendekezo ya Tume ya Mackay (Government of Kenya, 1981). Mageuzi haya yalipelekea kutayarishwa kwa silabasi mpya katika masomo yote. Kwa mara ya kwanza, somo la Kiswahili lilipata silabasi kamili iliyoandikwa kwa lugha ya Kiswahili.

Tangu hapo, mtalaa huu umefanyiwa mapitio mara kadhaa. Lakini mapitio ya mwaka 2002 yalikuwa muhimu zaidi. Shughuli hii ambayo Taasisi ya Elimu ya Kenya imeita mapitio na usawazishaji wa silabasi (KIE, 2002), imeupa mtalaa huu sifa mpya. Baadhi

ya sifa hizi ni kujumuishwa kwa masomo mapya kama vile Isimujamii katika lugha ya Kiswahili na kutahiniwa katika mtihani wa K.C.S.E karatasi ya 102/2.

Marekebisho ya mtalaa kwa somo la Kiswahili yalipelekea kufundishwa kwa Isimujamii kutoka kidato cha kwanza hadi cha nne. Kulingana na *Teachers Handbook* (KIE, 2006) walimu wanapaswa kufundisha somo hili kutoka kidato cha kwanza hadi cha nne chini ya stadi za kusikiliza na kuzungumza. Kufikia sasa, somo la lugha ya Kiswahili katika shule za upili nchini Kenya lina sehemu nne ambazo zinafundishwa na kutahiniwa katika mtihani wa kitaifa wa K.C.S.E. Sehemu hizi ni ***Ufahamu***, ***Ufupisho***, ***Matumizi ya Lugha (sarufi)*** na ***Isimujamii***. Sehemu ya Isimujamii ndiyo ya mwisho zaidi kuwekwa katika mtalaa wa elimu kwa mara ya kwanza (KIE, 2002). Ni sehemu ambayo imeanza kushughulikiwa na wasomi wengi kwa lugha ya Kiswahili.

Kulingana na watalaamu mbalimbali, Isimujamii ni sehemu ya isimu ambayo huchunguza uhusiano uliopo baina ya lugha na jamii. Huangalia jinsi jamii au watu wanavyotumia lugha katika mawasiliano, (Taz. Masinde 2007, Mathooko 2007 na Aswani na wenzake 2006). Vile vile, wataalamu hawa wanafafanua isimu kama maarifa ya kujua lugha na jamii ni mkusanyiko au kundi la watu. Kwa hivyo, Isimujamii ni taaluma inayochunguza matumizi ya lugha kulingana na vikwazo vya kijamii.

Utambuzi wa umuhimu wa Isimujamii umeifanya Taasisi ya Elimu Kenya (KIE, 2002) kutaja madhumuni mojawapo ya kufundisha Kiswahili katika shule za upili kuwa,

"Kumpa mwanafunzi uwezo wa kudumu wa kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika ipasavyo kwa lugha ya Kiswahili". Lengo kuu la somo la Isimujamii katika mtalaa wa elimu ni kuwawezesha wanafunzi kuwasiliana vilivyo pamoja na kurutubisha uwezo wao wa kuhusiana na watu wa matabaka mbalimbali. Baada ya kozi hii watakuwa na weledi mzuri wa uhusiano wa lugha na jamii. Vipengele muhimu kuhusu Isimujamii kama vile sajili za lugha, lugha na uana, muktadha na pragmatiki hulenga kuangazia mambo yote yanayohusu utumiaji lugha katika jamii kwa mapana na marefu. Ili kufanikisha jambo hili, vipengele mbalimbali vya Isimujamii vitafunzwa chini ya stadi za kusikiliza na kuzungumza, (KIE, 2006) japo havijaonyeshwa moja kwa moja.

Msukumo wa utafiti huu umetokana na sababu kuwa utekelezaji wa mtalaa mpya wa somo la Isimujamii katika somo la Kiswahili umekuwa na shida kadha. Utafiti awali umeonyesha kuwa baadhi ya walimu wanadai kuwa hawajui wafunze nini kwa vile mada kuhusu Isimujamii hazijawekwa wazi. Wengi wao hawakuandaliwa kufunza somo hili katika vyuo vya ualimu.

Kulingana na Bishop (1985) ubora wa silabasi si uzuri wa yaliyomo tu bali ni utekelezaji wake. Shiundu na Omulando (1992) wanadahili kuwa ingawa utekelezaji wa silabasi shuleni hutegemea mambo kama vile fedha, vifaa na wanafunzi miongoni mwa mengine, jambo lililo muhimu zaidi ni walimu. Benaars, Otiende na Boisvert (1994) wanashadidia hoja hii ifuatavyo: "Ili mabadiliko ya mtalaa yafanikiwe au kukita mzizi inategemea kwa kiasi kikubwa mwalimu katika shule. Ni yeye katika ngazi ya darasa anayetekeleza."

Obanya anayenukuliwa katika Bishop (1985) anasisitiza ukati wa mwalimu. Anatoa mfano wa namna utekelezaji wa mtalaa mzuri wa somo la Kifaransa ulivyokwama nchini Nigeria kutokana na mwelekeo hasi wa walimu.

Odeo (2007) akimrejelea Hawes (1979) na Bishop (1985), anasema kuna baadhi ya mambo yanayohusu walimu ambayo yanaweza kufanikisha au kufifisha juhudi za utekelezaji wa mtalaa. Haya ni pamoja na kuhusika au kutohusika kwa walimu katika michakato ya mageuzi, uelewa wa dhana ya mtalaa, maandalizi, mazingira na majukumu ya walimu pamoja na usaidizi wanaopata kutoka kwa wataalamu na watawala. Kutoteua kitabu mahsusi kama ilivyo sasa kwaweza kuchangia kutotekelezwa kuzuri kwa mtalaa wa Isimujamii au mtalaa mwingine wowote mpya.

Tathmini ya mtalaa wa Isimujamii wa shule za upili ni jambo lisiloepukika kufanywa ikiwa tutafaulu kuwa na utekelezaji wa silabasi mpya ya Isimujamii katika somo la Kiswahili.

## 1.1 SWALA LA UTAFITI

Utafiti huu ulilenga kutathmini mtalaa wa Isimujamii wa shule za upili nchini Kenya. Kulingana na Odeo (2007), tangu mtalaa wa somo la Kiswahili wa shule za upili uliopitiwa uzinduliwe mwaka 2003, maoni mengi yamesikika kutoka kwa walimu, hususan walimu wa somo la Kiswahili katika shule za upili. Imedaiwa kuwa, kuna ukosefu wa vitabu, vifaa vya kufundishia na mwongozo wa mtihani wa mwisho wa

4) Ni vigezo vipi vinavyopima utendakazi wa mitalaa?

## 1.3 MALENGO YA UTAFITI

Malengo haya ndiyo yalilengwa kutimizwa:-

1) Kufafanua sifa zinazotawala matumizi ya lugha katika miktadha mbalimbali kulingana na mtalaa wa Isimujamii.
2) Kubainisha maoni ya walimu na wakuza mitalaa wa somo la Kiswahili katika shule za upili kuhusu maudhui ya mtalaa mpya wa Isimujamii.
3) Kudhihirisha uhusiano uliopo baina ya uandalizi wa mtalaa na ufunzaji.
4) Kufafanua vigezo vinavyopima utendakazi wa mitalaa.

## 1.4 TAHADHANIA

1) Mtalaa wa Isimujamii katika shule za sekondari una udhaifu katika kumwongoza mwalimu.
2) Somo la Isimujamii lilipendekezwa kufundishwa katika lugha ya Kiswahili bila kuwaandaa walimu vilivyo.

## 1.5 SABABU ZA KUCHAGUA MADA

Utafiti huu ulihusu uchunguzi wa mtalaa wa Isimujamii wa shule za upili nchini Kenya. Msukumo wa utafiti huu ulitokana na kuanzishwa kwa silabasi mpya katika mfumo wa elimu ya 8-4-4 katika shule za upili na kujumuishwa kwa Isimujamii katika mtihani wa Kiswahili karatasi 102/2. Sababu kuu kwa hivyo ni kuwawezesha walimu kupata

mawanda ya kuzingatia kwa uwazi zaidi katika kufunza somo hili. Wanafunzi watafaidika kwa kuwa, licha ya kufunzwa, wataweza kutumia lugha kimuktadha, kihali, kiumri, na kijinsia. Kilele cha utafiti huu kitakuwa kuwawezesha walimu na wanafunzi kufanya maandalizi mema ya K.C.S.E. kupitia utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na wadau katika elimu.

Mchango mwingine wa utafiti huu ni kuwa ufafanuzi wa dhana za Isimujamii utachangia ghala la Isimujamii. Dhana hizi nyingi zimefafanuliwa na wanaisimujamii, lakini ziliangaliwa upya katika kiwango cha wanafunzi hawa na mchango wake katika lugha ya Kiswahili kulingana na mapendekezo ya mtalaa. Upanuzi wa dhana hizi waweza kuchangia katika uundaji wa Kamusi ya Isimujamii inayoweza kupendekezwa na Taasisi za elimu kutumiwa na wanafunzi.

Mchango mwingine ulikuwa kwa lugha ya Kiswahili. Vitabu na tafiti nyingi kuhusu Isimujamii zimeandikwa kwa lugha ya Kiingereza. Utafiti huu utawasaidia wasomi wanaoshughulikia Isimujamii kwa lugha ya Kiswahili na hasa wanaolenga Isimujamii kwa shule za upili wajue vipengele watakavyotilia maanani. Utawasaidia kuandika vitabu vya Isimujamii vinavyolenga kiwango cha wanafunzi wa sekondari.

Aidha utafiti huu utaweza kuwa na mchango wa kinadharia. Mojawapo ya malengo ya Isimujamii ni kufasili matumizi na mitindo ya lugha kulingana na kategoria za kijamii. Kategoria hizi huegemea vigezo vya uana, ajira, elimu, umri hususan ujana na tabaka

(Taz. Gumperz na Hymes 1989). Uamilifu wa lugha unadhihirika katika uhusiano wa lugha na jamii katika kufanikisha mawasiliano na kujenga uhusiano kati ya wanajamii. Nadharia ya ufundishaji wa Lugha ya Pili (L2), ambayo ilijikita katika mkondo wa nadharia ya lugha ya mawasiliano iliyotumiwa huzingatia uyakinifu wa matumizi ya lugha na kwa jumla kupitia vigezo vya kijamii. Matumizi haya yatachangia kuendelezwa na kukuza taaluma ya Isimujamii katika mtalaa wa Isimujamii.

Utafiti huu utasaidia asasi zinazohusika na ukuzaji na utekelezaji wa mitalaa, hasa Taasisi za Elimu Kenya na Idara ya Kudhibiti Ubora wa Elimu kuhakikisha zinazingatia mapendekezo ya nadharia na taratibu za kitaaluma katika utendakazi. Walimu nao wataweza kupitia matokeo ya utafiti huu, kuelewa nafasi yao katika utekelezaji wa mtalaa mpya wa Isimujamii katika silabasi ya Kiswahili. Aidha, matokeo ya utafiti huu yatachochea mijadala miongoni mwa wataalamu kuhusu ukuzaji wa mitalaa ya Kiswahili na utekelezaji wake.

Michango hii iliyotajwa inabainisha umuhimu wa utafiti huu. Somo hili linapaswa kutazamwa na walimu, wanafunzi na wasomi wa lugha ya Kiswahili kama baraka humu nchini. Lugha ya Kiswahili itapata maana zaidi kupitia uelewa wa wanafunzi wa umilisi mawasiliano na baada ya kozi hii mwanafunzi ataweza kuingiliana na jamii kwa vile ataweza kutumia lugha kimuktadha. Sarufi pekee haimtoshi mwanafunzi bali Isimujamii itaziba pengo linalopatikana baada ya kufunzwa uamilifu katika kutumia lugha na hivyo hatakuwa na upungufu wa lugha yoyote.

## 1.6 UPEO NA MIPAKA YA UTAFITI

Utafiti huu ulihusu tathmini ya mtalaa wa Isimujamii wa shule za upili nchini Kenya. Isimujamii inafundishwa katika shule za upili na vyuo vikuu nchini Kenya. Hata hivyo utafiti huu ulijikita katika kuchunguza mtalaa wa Isimujamii wa shule za upili pekee chini ya stadi za kusikiliza na kuzungumza.

Utafiti huu ulijikita katika kutathmini sehemu ya Isimujamii katika mtalaa wa elimu kwani ndiyo mpya zaidi na imetahiniwa kwa mara ya kwanza mwaka 2006. Ni taaluma ambayo imeanza kuandikiwa na wasomi wengi kwa lugha ya Kiswahili na kwa hivyo utafiti haukujikita katika uchambuzi wa mada wanazoandika bali zile ambazo zinalenga miktadha fulani ya lugha iliyopendekezwa na Taasisi ya Elimu Kenya katika kila kidato (K.I.E. 2006).

Utafiti huu ulichunguza mtalaa wa Isimujamii na maoni ya walimu kuhusu mtaala huu katika Wilaya ya Thika. Walimu wa shule hizi walikuwa ni wa shule za serikali na za kibinafsi. Msingi wa uteuzi huu ni kuwa walimu katika shule hizi huzingatia mapendekezo yaliyo katika silabasi kwa njia tofauti. Aidha, kulikuwa na uwezekano wa kupata shule za Kitaifa na za Mikoa pamoja na za Wilaya katika Wilaya ya Thika. Walimu wana tajriba tofauti kutegemea shule wanazofunza.

## 1.7.0 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA

Sehemu hii itazingatia maandishi ya kijumla kuhusu Isimujamii, tafiti kuhusu ufundishaji wa lugha ya Kiswahili na matumizi ya mitalaa katika elimu.

### 1.7.1 Maandishi ya kijumla kuhusu Isimujamii

Isimujamii ni sehemu ya isimu ambayo huangalia mahusiano yaliyopo baina ya lugha na jamii. Tunaangalia jinsi jamii au watu fulani wanavyotumia lugha katika mawasiliano (Taz. Mathooko 2007 na Aswani na wengine 2006). Masinde (2007) anasema neno Isimujamii linalotakana na maneno mawili: isimu na jamii. Akimnukuu Besha (1994), anafafanua isimu kama maarifa ya kujua lugha. Kamotho (2006) na Masinde (2007) wanatoa maana ya jamii kama mkusanyiko au kundi la watu. Watu huweza kuletwa pamoja kwa sababu maalum. Tunaweza kuwa na jamii ndogo au kubwa. Jamii inaweza kuwa familia, wazee, vijana, waumini, wanataaluma, timu ya wachezaji, wafugaji, genge la wezi, kabila, taifa au jumuiya fulani. Utekelezaji wa mtalaa mpya wa Isimujamii utahakikisha wanafunzi wameelewa maana hizi na kuchangia katika umilisi wao wa mawasiliano.

Aidha, Spolsky (1968) anasema jamii-lugha ni jumla ya watu wote wanaozungumza lugha moja. Naye Bloomfield anasema ni kikundi chochote cha watu kinachoingiliana kwa njia ya mazungumzo. Naye Gumperz (1968) anaonelea kuwa jamii lugha ni kikundi cha watu kinachotagusana kila mara au kila wakati kupitia ishara za kimaongezi na kinachotofautiana na kingine kwa kiasi fulani katika matumizi yao ya lugha.

katika kuifunza ni kuwa itawapa wanafunzi masharti, nidhamu au kaida kuhusu matumizi ya lugha kwa mujibu wa mazingira.

### 1.7.2. Tafiti Bayana kuhusu Ufundishaji wa Kiswahili Shuleni

Kuna maandishi na tafiti chache ambazo zimeshughulikia suala la ujifunzaji wa lugha ya pili. Odeo (2007) katika "Kiswahili na Elimu Nchini Kenya" ametafiti juu ya utekelezaji wa silabasi mpya ya somo la Kiswahili katika shule za upili. Katika utafiti wake, aliweza kuwahoji walimu na wakataja udhaifu wa silabasi mpya unaotatiza utekelezaji. Wengi walidai baadhi ya mafunzo ya sarufi yalilenga kiwango cha Chuo Kikuu. Baadhi yao walieleza kuwa ugumu wa mada unawatisha wanafunzi na kuwafanya wachukie somo la Kiswahili. Odeo hajataja mifano ya mafunzo ya sarufi na mada zinazolenga chuo kikuu. Utafiti wa Odeo ni tofauti na utafiti huu kwa vile wake ulihusu tu somo la Kiswahili kwa jumla katika silabasi mpya kwa upande wa fasihi na lugha ya Kiswahili lakini utafiti huu ulitathmini Isimujamii katika mtaala mpya wa lugha ya Kiswahili.

Nthiga (2003) ameonyesha matumizi ya ubadilishaji msimbo katika shule za chekechea. Umatini wa lugha katika kiwango hiki cha wanafunzi ni muhimu katika kupitisha ujumbe kwa watoto wa kiwango hiki cha wanafunzi. Uchunguzi huu ni muhimu katika upangaji wa vipindi vya masomo na jinsi ya kushughulikia wanafunzi wa kiwango hicho. Utafiti huu uliendeleza uchunguzi huu kwa kuonyesha jinsi ufundishaji kama huu unavyoweza kuboreshwa katika kiwango cha shule za upili.

Musau (1992) alifanya utafiti juu ya ujifunzaji na ufunzaji wa lugha ya pili, kipengele cha fonolojia. Alishirikisha wanafunzi waliokuwa wanajifunza lugha ya pili, kipengele cha fonolojia. Ilibainika kuwa mwanafunzi anapojifunza lugha ya pili, yeye huhamisha baadhi ya istilahi kutoka lugha yake ya kwanza. Kazi hiyo inatofautiana na hii kwa vile ilichunguza kipengele cha fonolojia katika mtalaa lakini kazi hii ilichunguza Isimujamii katika mtalaa wa shule za upili.

Onyango (1990) alifanya utafiti juu ya lugha ya Kiswahili hususan mielekeo ya wasomi kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili nchini Kenya. Kazi hiyo ilionyesha kuwa mielekeo ni zao la jamii na husababishwa na utamaduni wa jamii ambamo lugha mbali mbali huzungumzwa. Utafiti huo ni tofauti na utafiti huu kwani ulijikita katika kipengele kimoja cha lugha ya Kiswahili katika mtalaa wa elimu. Utafiti huu ulijihusisha na maoni ya walimu na wakuza mitaala kuhusu mtalaa wa Isimujamii wa shule za upili.

Wanyoike (1978) na Mbaabu (1985) wanaafikiana kuwa watu wanaojifunza lugha ya pili hupata shida kutokana na athari ya lugha ya kwanza. Wanyoike (1978) anapendekeza utafiti wa kina ufanywe na watu walio na umilisi wa lugha ya Kiswahili. Akisisitiza anasema, matokeo ya utafiti yanaweza kutumiwa na wanaoandaa mitalaa katika maandalizi itakayolenga na kuafiki mahitaji ya wanafunzi. Hali hii inaweza kurahisisha na kuboresha ufunzaji na ujifunzaji. Kazi ya Wanyoike ina ukuruba na utafiti huu kwa kujaribu kuboresha mtalaa fulani lakini tofauti kwa vile hii ilichunguza mtalaa unaoendelea kutekelezwa.

Udurusu wa tafiti kuhusu ufundishaji wa Kiswahili umeonyesha kuwa uchunguzi wa kutosha kuhusu mtalaa mpya wa lugha ya Kiswhaili haujafanywa. Nyingi ya tafiti hizi zinashughulikia ujifunzaji na ufundishaji wa Kiswahili.

### 1.7.3 Matumizi ya Mitalaa katika Elimu

Kulingana na Oluoch (2002) elimu ni ile hali ya kupata na kuendeleza maarifa, ujuzi na mielekeo. Wataalamu wa taaluma ya ukuzaji mitalaa kama vile Hooper (1971), Shiundu na Omulando (1992), Oluoch (2002) na Okech na Asiachi (1992) wanakubaliana kuwa mtalaa ni yale yote yanayopangwa na taasisi za elimu ili kufuatwa na walimu katika ufunzaji wao. Wataalamu hawa wa mitalaa wanataja hatua saba za ukuzaji mitalaa kama vile:

(i) Uamuzi wa kisera

(ii) Kutathmini mahitaji

(iii) Kuunda mtalaa

(iv) Kuandaa zana za kufundishia

(v) Majaribio

(vi) Utekelezaji

(vii) Tathmini

Vigezo hivi vilitumiwa katika uchanganuzi wa data juu ya maoni ya walimu na wakuza mitalaa kuhusu dhana ya mitalaa na uandalizi wake. Kila hatua ilitathminiwa na umuhimu wake kuangaziwa zaidi na uchunguzi ulifanywa iwapo walimu walihusishwa.

Hatua hizi ni muhimu katika utafiti huu kwa vile ikiwa hatua fulani haitashughulikiwa kitalaaluma, huenda athari mbaya ikatokea katika utekelezaji wa mtalaa.

### 1.8.0 MISINGI YA NADHARIA

Utafiti huu umeongozwa na nadharia changamano ambayo imejumuisha vipengele kutoka nadharia za ufundishaji wa lugha ya pili na vingine kutoka nadharia ya Isimujamii.

Lengo la Isimujamii katika mtalaa wa elimu ni kufafanua dhima ya lugha katika jamii; Mawasiliano na kujenga uhusiano kati ya wanajamii. Jambo hili limetekelezwa na nadharia ya ufundishaji wa L2 ambayo imejikita katika sarufi ya lugha na uamilifu au utendekazi wake katika jamii. Aidha, kwa kutumia nadharia ya Isimujamii, imedhihirika jinsi lugha inavyohusiana na jamii na baadhi ya vipengele vinavyoathiri matumizi ya lugha.

### 1.8.1 Nadharia ya Ufundishaji wa Lugha ya Pili

Nadharia ya Ufundishaji wa L2 duniani imejumuisha nadharia (mikondo) mbalimbali ambayo imewahi kuathiri, na ambayo mpaka sasa inaathiri ufundishaji wa L2 (Taz. Musau na Chacha, 2001). Baadhi ya mikondo hiyo ni kama:

i. **Nadharia ya Utabia**

ii. **Nadharia ya Lugha ya Mawasiliango**

iii. **Nadharia ya Ufundishaji kwa Vitendo**

iv. **Nadharia ya Kijumla na Kibinadamu**

v. **Nadharia ya Mwalimu Aliye Kimya**

vi. **Nadharia ya Moja kwa Moja**

Lengo la ufundishaji wa Isimujamii ni kuweza kukuza uwezo wa mwanafunzi wa kuwasiliana na kuhusiana na jamii na kwa hivyo mtazamo uliofaa utafiti huu ni wa Nadharia ya Lugha ya Mawasiliano.

Nadharia ya Lugha ya Mawasiliano ilishika kasi na kupanuka nchini Uingereza katika miaka ya 1970. Lengo kuu la nadharia hii kama itakavyobainika baadaye ni kukuza uwezo wa kuwasiliana lakini siyo kukuza ujuzi wa miundo au vipengele vya lugha tu.

#### 1.8.1.1 Nadharia ya Lugha ya Mawasiliano

Katika miaka ya 1960 na kuendelea, kulikuwa na imani kuwa ujuzi wa miundo au vipengele vya lugha ulimtambulisha mwanalugha. Kama McDonough (1993) anavyosema, mwanafunzi wa lugha alistahili kujua miundo ya lugha pekee. Mazoezi kwa mwanafunzi yalihusu minyambuliko ya vitenzi au kutambua maneno yanayounda sentensi. Katika muktadha wa shule za nchi ya Kenya, jambo hili lilidhihirika kuwa la kweli ndipo Isimujamii ikaanzishwa ili mwanafunzi awe na uamilifu wa mawasiliano badala ya kuwa na ujuzi wa miundo ya lugha.

Kufikia mwisho wa miaka ya 1960, wanaisimu walianza kukosoa mfumo wa ufundishaji wa lugha kwa wanafunzi. Ilidaiwa kuwa, mafunzo hayo yaliwafanya wanafunzi wajuzi

wa miundo pekee lakini wasiokuwa na ujuzi wa mawasiliano (Johnson, 1982). Umilisi wa miundo ya lugha ni muhimu lakini hautoshi (McDonough, 1993). Wanafunzi wenye ujuzi wa miundo wanaweza kuunda sentensi sanifu lakini hawawezi kuzitumia katika maisha ya kila siku kuwasiliana. Hii ilikuwa ni sarufi zalishi. Kulingana na Chomsky (1957, 1965) sarufi Zalishi ilitambua lugha kwa misingi ya umilisi wa mtu binafsi. Sarufi Zalishi ni mtazamo unaoiona lugha kama mfumo wa ujuzi uliojisawiri akilini mwa msemaji. Ujuzi huo huitwa umilisi lugha. Mtazamo wa sarufi zalishi husisitiza umsingi wa muundo wa maumbo ya lugha dhidi ya muundo wa maana.

Miaka ya 1970 muundo wa maumbo ya lugha ulianza kukashifiwa na wanaisimu. Msisitizo ukawa kuwa licha ya kuwa na umilisi lugha, wanafunzi wanapaswa kuwa na umilisi wa mawasiliano. Waasisi wa mtazamo huu kama Hymes (1972) wanaonelea kuwa anayejifunza lugha lazima awe na uwezo wa kuitumia vilivyo. Haya hujulikana kama uamilifu wa mawasiliano kwa vile humpa uwezo anayejifunza L2 kuitumia katika miktadha mbalimbali. Jambo hili huwezeshwa na sarufi amilifu mfumo. Kulingana na Halliday (195, 1994) sarufi amilifu mfumo hutazama lugha kama mtandao wa maana. Kwa hivyo, ufundishaji wa lugha ukachukua mtazamo mwingine na msisitizo ukawa wanafunzi lazima wawe na uamilifu wa mawasiliano licha ya kuwa na umilisi lugha. Sarufi amilifu mfumo ni mtazamo wa lugha unaosisitiza matumizi kulingana na miktadha halisi ya mawasiliano. Mtazamo huu unaweka msisitizo wa mifumo ya maana. Mfumo wa maana hushughulikiwa katika taaluma ya semantiki na pragmatiki ambapo mfumo wa maumbo hushughulikiwa katika taaluma ya sintakisia. Pragmatiki huchunguza maana ya

lugha kulingana na muktadha wa matumizi. Uchunguzi wa kipragmatiki huchunguza athari za miktadha mbalimbali katika semantiki na pragmatiki.

Nadharia ya ujifunzaji lugha inapendekeza hatua kadha kuchukuliwa ili ujifunzaji na ufundishaji huo utimilike. Johnson (1982) anapendekeza shughuli za ufundishaji wa lugha zitakazohusisha na maisha halisi ya kila siku kwa vile hufanikisha ufundishaji. Johnson anasema kuwa baada ya kipindi mwanafunzi wa lugha aweze kupata maarifa ya kufanya jambo asingelifanya kabla ya kufunzwa.

Ili mwanafunzi awe na ujuzi wa kuwasiliana, ni heri kuwe na kuwasiliana kwingi kati ya mwalimu na wanafunzi wenzake. Kwa hivyo, ukaririshaji wa mawasiliano hautaepukika katika darasa kama hilo. Kazi ya mwalimu itakuwa kuzua miktadha mbalimbali darasani itakayoibusha mawasiliano kati yao. Kwa mfano, kuwe na michezo ya lugha, michezo ya kuigiza yenye majadiliano mengi na mazungumzo mengi katika darasa.

Drili ni shughuli nyingine inayoweza kutumiwa na mwalimu katika ufundishaji wa lugha ya mawasiliano. Katika matumizi ya drili, mwalimu humdhibiti mwanafunzi katika matumizi mwafaka ya lugha lengwa hadi atakapoitumia inavyotakikana. Ili kutimiza jambo kama hili, ufundishaji ushirikishe mwalimu na mwanafunzi.

Kulingana na Johnson (1982) ufundishaji wa lugha ya mawasiliano utaimarika ikiwa kutakuwa na mazoezi mengi ya lugha inayofunzwa. Ni kupitia matumizi ya lugha hiyo



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

ambapo wanafunzi wanaweza kuwasiliana (Rivers, 1983). Lugha itakuwa na maana na kuonekana yenye manufaa kwa wanafunzi na kwa hivyo kuwapa motisha wa kuendelea kujifunza. Shughuli hizi zote hufanya ufundishaji wa L2 rahisi na kuwa na athari kubwa kwa wanafunzi. Jambo hili linaungwa mkono na Willis na Willis (1996) ambao wanasema kuwa kupitia shughuli hizi, wanafunzi watakuwa na uwezo wa kuwasiliana kwa lugha hiyo na matumizi yake yatadumu. Wazo hili pia linashadidiwa na Musau na Chacha (2001) ambao wanasema kuwa Nadharia ya Lugha ya Mawasiliano inakusudiwa kuimarisha mbinu za ufundishaji ambazo zinasisitiza uhusiano uliopo kati ya miundo ya lugha na mawasiliano. Wanaendelea kusema kuwa nadharia hii inapendekeza ufundishaji ambao unatumia shughuli zinazoendeleza mawasiliano. Hii ni kwa sababu wafuasi wa nadharia hii wanaamini kuwa ujifunzaji wa L2 huendelezwa na vitendo au shughuli zinazoendeleza mawasiliano badala ya kukariri miundo. Utafiti huu umeongozwa na mihimili ya nadharia kama ilivyofafanuliwa na Musau na Chacha kuwa:

(i) Maana ya miundo husisitizwa kwani lengo kubwa la nadharia hii ni mawasiliano. Kwa mujibu wa nadhaira hii, madhumuni makuu ya lugha ni kuwasiliana, kwa vile lugha ni mfumo wa kueleza maana.

(ii) Vipashio muhimu vya lugha siyo vile vya kisarufi na kimuundo tu, lakini pia vile vya kimawasiliano.

(iii) Matumizi ya lugha kwa wingi darasani hupendekezwa kwani nadharia hii husisitiza kuwa mtu hujifunza lugha vizuri kwa kuitumia.

(iv) Muktadha hupewa nafasi muhimu katika ufundishaji. Kwa mfano, maneno mapya au miundo fulani ya kisarufi huwekwa katika muktadha wa mawasiliano, kama vile katika sentensi, mazungumzo na makala.

(v) Drili zinafanywa lakini siyo za lazima kwa mujibu wa nadharia hii.

Mihimili ya nadharia hii imefanikisha utafiti huu kwa njia kadha. Lengo kubwa la Isimujamii ni kuchunguza uhusiano uliopo baina ya lugha na jamii na jukumu la ufundishaji wa L2 ni kuwapa wanafunzi ujuzi wa mawasiliano. Mtafiti aliweza kuchunguza vipengele vya Isimujamii vinavyofundishwa katika mtalaa mpya katika shule za upili nchini Kenya na kwa kuwahoji walimu na kupata maoni yao alichanganua data yake na kutathmini iwapo wanayoshughulikia yanalenga azma ya somo hili. Maoni zaidi yalipatikana kutoka kwa walimu na wakuza mitalaa ili kudhihirisha ubora na udhaifu wa mtaala huu kwa wanafunzi wanaojifunza L2. Aidha, mada zinazopendekezwa na mtalaa mpya wa Isimujamii zilichunguzwa na kuchanganuliwa na kutathminiwa iwapo zina manufaa kwa wanafunzi wanaojifunza L2. Vile vile, mada hizo zilichanganuliwa na kutathminiwa iwapo zimelenga kiwango cha wanafunzi wa shule za upili na uchanganuzi zaidi ulifanywa kuhusu umuhimu wa yaliyomo ya Isimujamii katika uboreshaji wa mawasiliano.

### 1.8.2 Nadharia ya Isimujamii

Nadharia ya Isimujamii pia inasisitiza umuhimu wa motisha katika mawasiliano. Wanaisimu wanaoshughulikia vipengele vya kimotisha ni pamoja na Giles, Talor, Bourhis, Bradac (tafiti zao zimetajwa katika Giles (1990), na Scotton (1993). Kwa

mujibu wa tafiti hizi, mahusiko ya Isimujamii yananuia kueleza sababu zinazowafanya watu watumie lugha kwa njia fulani na wachague lugha fulani ili wajinasibishe au wajitofautishe na wazungumzaji wengine.

Kipengele kingine kinachoshughulikiwa na nadharia ya Isimujamii ni cha kijamii-muundo. Vipengele vya kijamii-muundo hueleza jinsi uchaguzi na matumizi ya lugha hutawaliwa na maumbo na miundo mipana ya kijamii na wala sio tu motisha na sababu za mzungumzaji. Waasisi wa mtazamo huu ni pamoja na Giles, Young, Sachder, Tajfel, Gudykunst (Taz. Giles, 1990) na pia Ting-Toomey (1989). Vipengele vifuatavyo vya kijamii-muundo huathiri uteuzi wa lugha na jinsi inavyotumiwa:

**(a) Idadi ya watu au wazungumzaji wa lugha fulani**

Idadi ya wazungumzaji huamua jinsi mtu anavyotumia lugha ama kujinasibisha au kujitofautisha. Lugha iliyo na wazungumzaji wengi ndiyo hutumiwa kama kioo au kiini cha kujinasibisha. Wazungumzaji wa lugha zenye watu wachache mara nyingi hulazimika kutumia lugha za watu wengi. Kwa mfano, watu wengi Nairobi hutumia Kikuyu kwa sababu ni lugha yenye wazungumzaji wengi (Parkins: 1974).

**(b) Utabaka**

Lugha inavyochukuliwa kuwa ya tabaka la juu kiuchumi na kijamii huwa ndiyo inayochaguliwa kutumiwa na wazungumzaji. Kwa mfano, Wasuba hujinasibisha

na Dholuo kwa sababu hii ndiyo lugha inayochukuliwa kuwa ya juu kitabaka (Ang'iella: 2002).

**(c) Dhima na jukumu la lugha**

Hapa tunarejelea matumizi ya lugha katika elimu, vyombo vya habari na dini. Lugha zinazotumika katika mawanda haya hupendelewa zaidi na huchukuliwa kuwa na hadhi ya juu.

Kulingana na Mathooko (2007) mtazamo mwafaka zaidi wa kuchunguza maswala ya Isimujamii ni ule jumuifu unaotilia maanani vipengele vya kimapokeo, kimotisha na kijamii-muundo, (Taz. Giles, 1990; Mathooko, 2004). Kutokana na maoni haya, utafiti huu umeongozwa na mihimili ifuatayo:-

(i) Ujifunzaji lugha unahusu jamii na mtu anayejifunza (Hymes, 1971).

(ii) Isimujamii ni kitengo cha isimu kinachoangalia matumizi ya lugha katika jamii, na jinsi miktadha ya kijamii inavyoathiri lugha (Fasold, 1984).

(iii) Tofauti za lugha kijamii hutokana na tofauti za miundo ya kijamii zinazoletwa na elimu, tabaka, uana, umri na mielekeo (Labov, 1972).

(iv) Matumizi ya lugha huathiriwa na mazingira, kichwa cha mazungumzo, lugha azijuazo mtu, elimu, usuli au mbari, hali ya mtu, tabaka, wadhifa, kazi, mielekeo, tajriba, malezi, uana, umri na hadhira.

(v) Kujinasibisha na kujitofautisha – mzungumzaji hujinasibisha ili apate kutuzwa.

Vile vile, hujitofautisha ili kuonyesha tofauti zilizopo kati ya mzungumzaji na wasikilizaji (Taz. Giles 1990 na Ting Tomey 1989).

(vi) Kujitambulisha – Mzungumzaji hutumia lugha au mtindo fulani ili ajitambulishe na kikundi cha watu au wasikilizaji fulani (Taz.Giles 1990 na Scotton 1993).

Mihimili hii ilitumiwa kuchunguza kama mtalaa umeizingatia. Kwa kuongozwa na mihimili hii, mtafiti alichunguza baadhi ya yaliyomo ya mtalaa kwenye silabasi na miongozo na kuthibitisha kama uandalizi wa mtalaa huu uliihusisha.

Misingi na mihimili ya nadharia hizi mbili ilisaidia kutathmini Isimujamii katika mtalaa. Aidha, ilisaidia utafiti huu kuona kama vipengele vilivyopendekezwa kufundishwa vinafaa kufundishwa katika kiwango hiki. Udhaifu wa mtalaa huu kuhusu yale yanayofundishwa uliangaziwa kwa kuhusishwa na maandalizi ya mtalaa.

## 1.9.0 MBINU ZA UTAFITI

### 1.9.1 Ukusanyaji wa Data

Data za utafiti zilikusanywa na mtafiti kwa kutumia njia mbili kuu. Njia hizi ni utafiti wa maktabani na utafiti nyanjani.

#### 1.9.1.1 Utafiti wa Maktabani

Mtafiti alipitia machapisho mbalimbali kama vile makala ya mitalaa: silabasi na miongozo ya silabasi, tasnifu, vitabu na majarida ili kusoma mengi kuhusu mtalaa, Isimujamii kama taaluma na kuona iwapo walimu wanaelekezwa jinsi ya kufundisha

somo hili. Habari katika machapisho haya zilichanganuliwa na kuhakikiwa na hatimaye kujumuishwa katika utafiti huu.

#### 1.9.1.2 Utafiti nyanjani

Utafiti zaidi ulifanywa nyanjani na mtafiti alitumia njia ya mahojiano kupata data alizohitaji. Mahojiano yaliendeshwa ana kwa ana kwa kutumia kiongozi cha maswali mahsusi (Taz. Kiambatisho I na II). Mtafiti aliamua kutumia mahojiano maana kulingana na Seliger na Shohamy (1989) mbinu hii humwezesha mtafiti kufafanua vipengele nyeti vya maswali na kudadisi zaidi ambapo majibu hayakukamilika.

### 1.9.2 Watafitiwa

Utafiti ulifanywa katika Wilaya ya Thika. Sababu ya kuteua wilaya hii ni kuwa kulikuwa na uwezekano wa kupata shule za kitaifa, mkoa, wilaya, kutwa na za kibinafsi katika eneo hili. Mtafiti alifikia uamuzi huu baada ya kung'amua kuwa utekelezaji wa mtalaa hutegemea kwa kiasi kikubwa hali katika ngazi ya shule hasa yanapohusika masuala ya maandalizi ya walimu, mazingira, vifaa, mitazamo na vitabu (Hawes, 1979; Benaars, Otiende na Boisvert, 1994). Mtafiti alichagua shule za kategoria ya mkoa, wilaya, kutwa na za kibinafsi kwa kutumia sampuli kusudi. Mtafiti alitumia mbinu hii kwa vile aliteua shule mahsusi alizohitaji. Hii ni kwa sababu mbinu hii hulenga makundi maalum katika jamii na makundi hayo huchukuliwa kuwa yanawakilisha makundi mengine halisi. Sampuli hii ilikuwa na shule kutoka tarafa tatu za wilaya ya Thika ambazo ni ya Gatanga, tarafa ya Ruiru na tarafa ya Kakuzi.

Kwa kutumia mbinu ya sampuli sahili nasibu, mtafiti aliteua mwalimu wa somo la Kiswahili mmoja kutoka kila shule na hivyo kupata watafitiwa 10. Sampuli iliyochaguliwa ilionyesha hali halisi ya shule zote za taifa. Mbinu hii ni muhimu kwa vile mtafiti hujiepusha na ubaguzi wa kundi fulani. Jumla ya shule zilizotembelewa zilikuwa 10. Msingi wa uteuzi huu ni kuwa shule kumi zimetosha kuona kama Isimujamii inafaa katika mtalaa wa elimu kwa sababu kama Milroy (1987) anavyosema sampuli ndogo ya utafiti wa isimu imetosha. Kulingana na Milroy, sampuli hiyo inatosha uchanganuzi wa data kwa vile sampuli kubwa huweza kukanganya mtafiti anapoichanganua. Walimu hawa walikuwa ni wale waliofuata silabasi na vitabu vilivyoteuliwa na Wizara ya Elimu. Ratiba ya somo la Kiswahili ilikuwa muhimu kwa mtafiti ili mtafiti athibitishe iwapo somo la Isimujamii linashughulikiwa.

Walimu ndio waliohojiwa pekee kwa vile kama wanavyosema Okech na Asiachi (1992) ugunduzi wowote katika elimu hufaulu ikiwa walimu huhusishwa katika ugunduzi huo. Wataalamu wanaweza kuunda malengo na mikakati ya kufundishia lakini ni walimu watakaotekeleza hayo. Mabadiliko yoyote katika elimu yahusishe walimu. Hata hivyo mtafiti alipata maoni zaidi kutoka afisa anayehusika na uandalizi wa mitalaa ya somo la Kiswahili kutoka Taasisi ya Elimu Kenya (K.I.E.).

Aidha, wanafunzi hawakuhojiwa kwa vile walimu ndio wanaochukua dhima kubwa ya utekelezaji wa mtalaa. Wanafunzi huwategemea walimu kwa kufunzwa yanayopendekezwa.

### 1.9.3 Uchanganuzi wa Data

Data kuhusu madhumuni ya utafiti huu zilichanganuliwa na kuhakikiwa kwa vigezo vinavyopima utendakazi wa mtalaa na kuhusishwa na mihimili ya nadharia za lugha ya ufundishaji wa lugha ya mawasiliano na Isimujamii. Aidha, data kuhusu yaliyomo ya mtalaa huu ilichanganuliwa na kuhakikiwa na vile vile kuhusishwa na misingi ya nadharia za lugha ya mawasiliano na Isimujamii. Zaidi ya hayo, maoni ya walimu na ya wakuza mitalaa kuhusu uandalizi wa mitalaa pamoja na yaliyomo kwenye silabasi yenye Isimujamii kwa shule za sekondari yalichanganuliwa na matokeo ya utafiti yakawasilishwa kwa njia ya mjadala.

Maoni ya walimu yamekadiriwa kufuatia asilimia ifuatavyo;

$\frac{X}{y} \times 100 = \%$ ambapo X = Idadi ya walimu waliotoa maoni yao.

Y = Idadi ya walimu walioshiriki katika utafiti.

Takwimu hizi zimetoa mwangaza kuhusu upokezi na mielekeo ya walimu kuhusu mtalaa mpya wa Isimujamii katika shule za upili nchini Kenya. Kwa hivyo, takwimu hizi zitawasaidia washikadau kuboresha ufunzaji wa Isimujamii na vile vile zitakuwa kielelezo chema cha kufuatwa wakati wa kufanya mageuzi mengine katika mtalaa mwingine.

# SURA YA PILI

## DHANA YA MITALAA NA UKUZAJI WAKE: SOMO LA LUGHA

### 2.0 UTANGULIZI

Kumekuwa na mijadala mingi kuhusu uhusishaji wa walimu katika ukuzaji na ubadilishaji wa mitalaa na uhuru wao katika ufundishaji. Vile vile, imethibitishwa kuwa elimu bora hutegemea ubora wa walimu. Ni wazi kuwa jukumu la mwalimu ni kutekeleza mtalaa ili yaliyomo kwenye mtalaa huo yawafikie wanafunzi kwa kuwaongezea maarifa (Jennings – Way 1980). Watu wengi hujiuliza kama walimu ni waamuzi katika ukuzaji na uboreshaji wa mitalaa? Katika mkabala huu pia, walimu hutoa maamuzi ya kielimu kwa njia tofauti. Namna ya kwanza wanayotoa maamuzi haya ni kwa kuchunguza malengo na mada za kufundishia. Namna nyingine ni kuhusu saikolojia ya ufundishaji ambapo mwalimu anafaa azingatie uwezo wa mwanafunzi kivyake na udumishaji wa uhusiano mwema kati yake na mwanafunzi. Jambo jingine linaloathiri uamuzi wa mwalimu ni vile vifaa vya kufundishia vinavyopatikana na muda waliotengewa walimu katika ufundishaji wao (Herrick, 1962).

Uamuzi wa mwalimu kuhusu yaliyomo katika somo huathiriwa na sera za elimu na imani yake kuhusu somo lenyewe (Schwille, Potter na Grant, 1980). Imegunduliwa

baadhi ya walimu nchini hufunza yaliyomo yanayotahiniwa na Baraza la Mitihani Kenya (KNEC) hata ingawa malengo ya elimu hayaruhusu jambo hili (Oketch, 1990). Katika hali zingine, walimu hukwepa mada ambazo ni ngumu kufunza ama ambazo hazijawekwa wazi katika silabasi. Baadhi ya walimu hufunza mada ambazo hazihusiani na mtalaa ili wafaidike kiuchumi (Floden, Porter, Schmidt, Freeman na Schwille, 1981). Walimu wengine hupuuza mada muhimu kwenye silabasi. Kwa hivyo sura hii itachunguza hatua za ukuzaji wa mitalaa kwa kurejelea somo la lugha ya Kiswahili hususan Isimujamii katika shule za upili. Kwa kuchunguza hatua za ukuzaji mitalaa, umuhimu wa walimu katika kila hatua utachunguzwa kwa vile ndio wanaotekeleza mtalaa huo mwishowe. Sura hii ni muhimu kwa vile itathibitisha kuwa jinsi walimu wanavyotekeleza mtaala mpya huonyesha kuwa uandalizi na ukuzaji wa mtalaa ulifanywa kitaaluma.

## 2.1 MAANA YA MTALAA

Hakuna maana mahsusi ya mtalaa inayokubaliwa ulimwenguni. Fasili nyingi zinazopatikana sasa kama za Kerr (1968) na Eaton (1975) kuhusu maana ya mtalaa zinakubaliana na za Tyler (1949), Taba (1962) na Tanner (1971) ambapo mtalaa unafafanuliwa kama maarifa yanayothaminiwa, ujuzi na mielekeo inayopitishwa na mfumo wa elimu ama taasisi mbalimbali nchini. Mtalaa kama huo kulingana na



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

Jetkins na Shipman (1976) huhusishwa na malengo na matokeo yanayotazamiwa.

Nao wataalamu wa elimu kutoka Taasisi ya Elimu Kenya wanasema yafuatayo kuhusu dhana ya mtalaa:

> **Mtalaa ni maarifa mtu anayopata kupitia elimu. Maarifa haya kwa mwanafunzi yanapitishwa kwake kupitia kwa watu wengine na zana za kufundishia. Watu wanaotekeleza mtalaa ni walimu ambao sisi (KIE) tunawaandaa baada ya ugunduzi wa mtalaa na zana za kufundishia ni vitabu, silabasi na miongozo ya walimu na matini zingine ambazo zinaandaliwa na kusambazwa kwa walimu na sisi.** (Mahojiano ya ana kwa ana na Bw. Waititu – Mkuu wa Idara ya Mitalaa ya Lugha ya Kiswahili KIE, tarehe 7, Julai 2008, saa nne, ofisini kwake).

Aidha, **Ukuzaji mitalaa** ni hatua mwafaka zinazochukuliwa katika kuamua yaliyomo yatakayofunzwa, taaluma ya elimu itakayotumika kupitishia hayo yaliyomo, chombo kitakachotumiwa kutekeleza mtalaa huo na tathmini kwa mtalaa huo ili kuona ubora wake. Maendeleo ya mitalaa huwa na lengo la kuinua kiwango cha elimu. Kwa hivyo kama Oluoch (1982) anavyosema, ni vizuri kujua maana ya elimu. **Elimu** ni hali ya kupata na kuendeleza ujuzi, maarifa na mielekeo yetu. Ili mwanafunzi apate elimu hii, lazima asome au afunzwe na mwalimu kwa kutumia vifaa kama vile silabasi, vitabu, miongozo na vifaa visivyohusiana na matini. Yatakayofunzwa katika elimu huandaliwa na wakuza mitalaa na lengo la sura hii ni kuona vile wanavyotenda kazi. Hata hivyo lengo la utafiti huu halitaafikiwa vyema bila kuona malengo ya

elimu ya taifa.

## 2.2 MALENGO YA ELIMU NCHINI KENYA

Baada ya kupata uhuru mnamo mwaka wa 1963, Kenya iliamua kuwa na mfumo wa elimu utakaoleta maendeleo nchini. Wataalamu wa elimu waliunda malengo yaliyolenga mtalaa uliozingatia maendeleo ya teknolojia. Kwa hivyo Kamati ya Ominde (1964) ilisisitiza kuwa elimu lazima izingatie matakwa ya nchi. Elimu hali kadhalika ndicho chombo cha kufanikisha maendeleo ya kiteknolojia, kiuchumi, kijamii na kibinafsi katika nchi nyingi zinazoendelea.

Ngugi (2007) katika **Elimu Nchini Kenya** ameorodhesha malengo haya ya elimu kama:

1. Kukuza utaifa, uzalendo na kuendeleza umoja wa kitaifa.
2. Kuendeleza ujenzi wa taifa kiuchumi, kiteknolojia na kijamii.
3. Kujiendeleza na kujitimiliza kibinafsi.
4. Kuendeleza uadilifu na amali za kidini.
5. Kuhimiza usawa wa kijamii na uwajibikaji.
6. Kukuza, kuhifadhi na kuthamini tamaduni za jamii mbalimbali nchini Kenya.

7. Kuendeleza uhusiano wa kimataifa na kudumisha mwelekeo ufaao kwa mataifa mengine ulimwenguni.

8. Kuendeleza uhifadhi wa afya bora na mazingira.

Malengo haya yana uhusiano mkubwa sana na malengo ya ufundishaji wa Isimujamii katika shule za upili. Katika somo la Kiswahili cha Biashara (Business Kiswahili) ijapokuwa kwa mfano, wanafunzi hujifunza Kiswahili, huwa mafunzo hayo yameegemea upande wa kuweza kuwasiliana vilivyo katika shughuli za kibiashara. Mwanafunzi huhitajika kujifunza stadi za mawasiliano ya biashara kwa jumla na kuweza kuyaweka katika maandishi. Wakuza mitalaa wa lugha huhitajika kuzingatia malengo haya wanapobadilisha au wanapokuza mtalaa.

Malengo haya ya elimu yatapatikana iwapo mwalimu anapofunza Isimujamii atazingatia taxonomia za malengo ya elimu (Taz. Lawton, 1973). Akimnukuu Bloom na wengine (1956) Lawton anasema kuwa taxonomia za malengo hupima maarifa ya mwanafunzi kupitia mabadiliko yake kitabia na mwalimu anapofunza ahakikishe kuwa haya yanajitokeza katika ufunzaji wake. Bloom na wenzake walipendekeza aina tatu za maarifa katika malengo ya elimu:

**(i) Maarifa tambuzi**

(ii) **Maarifa tendi**

(iii) **Maarifa hisi**

Maarifa haya ni muhimu sana katika upangaji na ukuzaji wa mitalaa. Kwa mfano, katika maandalizi ya mada yoyote chini ya stadi za kusikiliza na kuzungumza, inahitajika maarifa yote matatu lazima yajitokeze ikiwa tunatarajia tabia zifaazo kutoka kwa mwanafunzi.

**Maarifa tambuzi** yana stadi sita ambazo hupangwa kutegemea ugumu. Stadi hizi ni **ujuzi,** kwa mfano, wa kuweza kutatua shida mahsusi. **Ufahamu** wa kuweza kutafsiri na kufasili. **Uwelekevu** humwezesha mwanafunzi kutabiri matokeo kutokana na maarifa aliyopata ya somo. **Uchanganuzi** ni maarifa ya kuweza kuonyesha hatua mtu alizopitia alipogundua ukweli fulani. Pia ni uwezo wa kuonyesha uhusiano kati ya tahadhania na ukweli wa mambo. **Usanisi** (synthesis) ni maarifa yatakayomwezesha mwanafunzi kuunda mawazo yenye mantiki. Maarifa haya hudhihirika mwanafunzi anapoandika insha ambayo ina mtiririko wa mawazo bila kutatiza msomaji. Stadi ya mwisho ya maarifa tambuzi ni **tathmini** ambayo huhusu uamuzi wa manufaa ya jambo aidha kwa njia ya maelezo au kwa tarakimu.

**Maarifa tendi** hushughulikia ufundi wa kuunda au kutekeleza mambo. Kwa mfano, shughuli ya kutamka sauti huwa chini ya maarifa tekelezi.

**Maarifa hisi** hutathmini mwelekeo wa mwanafunzi au tabia ya mwanafunzi kwa kuangalia kwa mfano bidii yake, unyenyekevu, uvumilivu wa uwajibikaji.

Ijapokuwa tukiuangalia mtalaa wa Kiswahili tunaona kuwa mwanafunzi anatakiwa awe na uwezo wa kutekeleza yote katika aina hizi tatu za maarifa, walimu wengi wanapofunza hujishughulisha na maarifa tambuzi peke yake. Hii ni kwa sababu, wengi wao hujikakamua katika kukamilisha yaliyomo kwenye silabasi. Katika hali hii, hawafungamanishi wanayofunza na hali halisi ya maisha ili wawafanye wanafunzi watende zaidi. Wanafunzi wanafanywa wakariri wanayofunzwa kikasuku.

Tumeangalia fafanuzi mbalimbali kuhusu mtalaa, elimu na malengo ya elimu nchini Kenya. Hata hivyo kwa kuhitimisha sehemu hii ni muhimu kuangalia maoni ya Tyler (1949) kuhusu maswali yanayostahili kuzingatiwa katika uundaji na ukuzaji wa mitalaa. Tyler anapendekeza maswali manne muhimu ambayo ni:

i) Ni malengo yepi ya elimu yanayotazamiwa kupatikana?

ii) Ni ufunzaji upi wa kielimu unaopitishwa ili malengo hayo yapatikane?

iii) Ufunzaji wa kielimu unaweza kupangwa kwa ufasaha vipi?

iv) Tunaweza kujua vipi ikiwa malengo yameafikiwa?

Malengo haya ya elimu ni muhimu katika utafiti huu kwa vile yalisaidia kutathmini ubora na uboreshaji wa Isimujamii katika shule za sekondari. Ikiwa tunatazamia kupata matokeo mema kutoka kwa wanafunzi katika ufundishaji wa lugha au Isimujamii, ni heri wakuza mitalaa wahusishe aina zote tatu za maarifa kwa yaliyomo wayapendekezayo. Zaidi ya hayo, ni vyema ikiwa yaliyomo hayo yatafanikisha malengo ya elimu baada ya ufundishaji.

## 2.3 HATUA ZA KUANDAA MITALAA

Baada ya kufafanua dhana ya elimu na mitalaa, ni muhimu sasa kupitia hatua za uandalizi na ukuzaji wa mitalaa. Hatua hizi ni muhimu kwa sababu kufaulu au kutofaulu kwa mtalaa katika utekelezaji wake hutegemea kama zilizingatiwa. Ikumbukwe kwamba kila hatua ni muhimu. Hatua hizi saba kulingana na wataalamu wa taaluma ya ukuzaji mitalaa kama vile Hooper (1971), Oluoch (1982), Okech (1992), Shiundu na Omulando (1992) ni pamoja na:

(i) Kutathmini mahitaji

(ii) Uundaji wa mradi wa mtalaa

(iii) Upangaji wa mtaala

(iv) Majaribio

(v) Kufanya majaribio

(vi) Utekelezaji

(vii) Tathmini

Hatua hizi zilitumiwa katika ukusanyaji na uchanganuzi wa data ambapo maoni ya walimu yalikusanywa na kuchanganuliwa iwapo wanaelewa dhana na maandalizi ya mitalaa. Jambo hili ni muhimu kwa vile lilibainisha uhusiano uliopo baina ya uandalizi wa mitalaa na ufunzaji.

### 2.3.1 Kutathmini Mahitaji

Harakati muhimu zaidi katika ukuzaji mtalaa ni tathmini ya mahitaji. Tathmini ya mtalaa unaotumika hudhihirisha mahitaji na uwezekano wa mageuzi ya mtaala. Yaliyo muhimu zaidi katika hatua hii ni kujua:

(i) mahitaji ya nchi ni yepi?

(ii) nani atafanya tathmini ya mahitaji hayo?

(iii) nani atasimamia tathmini hiyo?

(iv) tathmini hii inatumiwa kutimiza lengo lipi?

Wafanyikazi wa mitalaa wanafaa wajue hali ya zana za kufundishia; ni zana zipi zinazotumika wakati huo na gharama ya zana hizo. Pia yawafaa wajue kuwa kwa sababu ya ongezeko la wanafunzi wanaosajiliwa, zana hizi haziwezi kamwe kuwatosha.

Chemichemi ya mahitaji hayo huwa ni sera za kiuchumi na kisiasa. Kwa mfano, matamshi ya raisi wa Jamhuri yanaweza yakaleta mabadiliko ya mtalaa. Ripoti ya bunge vile vile huweza kuzua uwezeko wa mtalaa mpya. Mwisho ni Kamati za kitaifa kama vile Kamati Tendaji ya Raisi (Presidential Working Party) ambayo ilipelekea kuanzishwa kwa Chuo cha pili nchini Kenya mwaka wa 1981 na ikapendekeza mfumo wa elimu kuwa wa 8-4-4. Katika mfumo huu wa elimu, somo la Kiswahili lilifanywa la lazima na la kutahiniwa katika mtihani wa kitaifa wa K.C.S.E (Taz. Mbaabu, 1996). Baada ya mapendekezo kama haya, wakuza mitalaa wa lugha ya Kiswahili wataanza kazi yao ili watayarishe mtalaa mpya utakaofuatwa na shule zote nchini.

Watakaotayarisha mahitaji mapya ni washikadau katika elimu kama vile walimu, wakuza mitalaa na taasisi kama vile Taasisi ya Elimu nchini Kenya (K.I.E). Katika somo la lugha ya Kiswahili, hatua hii ni muhimu kwa vile hudhihirisha hali ya lugha nchini. Wakuza mitalaa hawana budi kujua sera za lugha za nchi hiyo. Wanahitaji kuelewa vikwazo vya lugha na hivyo wajue jinsi watakavyoepukana navyo katika ukuzaji wa mtalaa huo wa lugha.

### 2.3.2 Uundaji wa mradi wa mtalaa

Hatua ya pili muhimu katika kukuza mtalaa ni uundaji wa mradi wa mtalaa. Katika hatua hii, mambo yafuatayo huzingatiwa:

(i) **Usuli** wa mradi ambapo wakuza mitalaa hubainisha swala la utafiti ili kuonyesha sababu za kuunda mtalaa mwingine na kuonyesha udhaifu wa mtalaa uliotangulia kulingana na matakwa ya nchi.

(ii) **Madhumuni** ya mtalaa mpya ambayo yatakuwa yanalenga muda mfupi na muda mrefu na vile yanavyohusiana na mahitaji ya mtalaa mpya.

(iii) **Mipango ya kazi** ambayo itaonyesha ratiba itakayofuatwa katika uundaji wa mtalaa mpya.

(iv) **Wataalamu** wa mtalaa na idadi itakayohitajika na kwa nini watahitajika.

(v) **Bajeti** itakayoonyesha pesa zitakazohitajika na kwa nini zitahitajika.

(vi) **Mahitaji** kama vile usafiri kwa wataalamu wa mradi huu, vyumba vya mikutano na mahitaji yoyote yatakayofaulisha mradi huu.

Hatua hii ni muhimu kwa wakuza mitalaa kwa vile wataona yaliyo mbele yao na kwa hivyo wajiandae kwa mahitaji yote ya mtalaa. Si vizuri kukuza mtalaa bila mpangilio maalum ili kujiepusha na athari mbaya kwa wanafunzi.

### 2.3.3 Upangaji wa Mtalaa

Hii ni hatua nyingine muhimu katika uundaji wa mtalaa. Mambo yafuatayo huzingatiwa katika hatua hii:

a) Kuelewa na kutaja malengo ya mtalaa.

b) Kuamua, kuandaa na kutaja malengo ya ujifunzaji.

c) Kuamua na kutaja mikakati ya kutathmini uelewa wa wanafunzi.

### 2.3.4 Maandalizi ya Zana za Kufundishia

Jukumu jingine muhimu baada ya kuunda mtalaa ni kuandaa zana za kufundishia. Hapa maswali yafuatayo hushughulikiwa:

- Ni zana zipi za kufundishia zinazotumika sasa zinazoweza kuendelea kutumiwa katika mtalaa mpya?
- Ni zana zipi zinahitajika kuongezwa?
- Zitatayarishwa na nani na vipi?
- Zana mpya zitagharimu pesa ngapi?

Ikiwa zana zingine zitahitajika katika mtalaa mpya, ni jukumu la wakuza mitalaa kujua gharama, idadi na hali ya zana hizo.

Mkuza mitalaa ya lugha huchagua matini za wanafunzi na walimu ambazo watahitaji.



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

Matini hizi ni vitabu, miongozo ya walimu na matini zozote zitakazoongeza maarifa kwa wanafunzi. Kuna zana zingine zinazohusiana na maendeleo ya kiteknolojia zinazoweza kutumiwa na wanafunzi kama kinasa sauti na video. Mkuza mitalaa huchagua vifaa hivi kwa sababu huwa na mada ambazo zitachangia ujifuzaji wa mbinu za lugha. Atachagua zana zile ambazo zitapatikana kwa urahisi na walimu na wanafunzi.

Jambo jingine la kuzingatia unapochagua zana za kufundishia ni kiwango cha wanafunzi. Unapochagua zana za kufundishia lugha, yaliyomo yatakayofundishwa wanafunzi lazima yawe ya kiwango chao. Kwa mfano, mada ambazo zitafunzwa wanafunzi wa shule za chekechea haziwezi kuwa sawa na za wanafunzi wa darasa la kwanza. Tajriba ya mwanafunzi ni muhimu kuzingatiwa unapochagua zana za kufundishia lugha. Kwa mfano, wanafunzi ambao wako na ujuzi wa lugha ya Kiswahili iwapo wanatoka Pwani watakuwa tofuati na wa mashambani ambao wamezoea lugha za mama. Wanafunzi kama hao wataelewa yaliyomo kwa njia tofauti hata ingawa watakuwa daraja moja kimasomo. Kwa hivyo, mkuza mitalaa yafaa achague zana ambazo hazitawabagua wengine lakini zile ambazo zitakuwa sawa kwa wote.

Tatu, mkuza mitalaa ya lugha anahitaji kufahamu jamii itakayotumia zana au mtalaa fulani wa lugha. Kila jamii huitumia lugha ili kuboresha uhusiano kati yao kwa kuwasiliana. Jamii tofauti huwa na mielekeo tofauti kuhusu uana, umri na matabaka. Kwa hivyo, katika kukuza na kupendekeza zana ama mada zitakazofunzwa, mkuza mitalaa lazima aone ama zitakubaliwa au zitakataliwa na jamii fulani.

### 2.3.5 Majaribio

Huku ni kufuatilia matumizi ya mtalaa mpya kwa kutumia taasisi chache ili kuona ufanyakazi wa mtalaa kabla ya kutekelezwa na taifa lote.

Si mapendekezo yote yanayofaulu kama yalivyopangwa. Ni muhimu maandalizi ya mtalaa na zana zitakazotumiwa na shule kujaribiwa kabla ya kutumiwa na shule zote ili kuona udhaifu wa mtalaa na kuurekebisha kabla ya utekelezaji. Jaribio hili hufanywa kwa kuwatumia walimu na wanafunzi katika shule.

Kuna hatua kadhaa ambazo hufuatwa katika jaribio kulingana na Oluoch (1982). Hatua hizi ni:

(i) Uchaguzi wa shule chache. Uchaguzi huu unastahili kufanywa kwa njia ambayo matokeo ya sampuli yatawakilisha uhalisi wa mtalaa mpya.

(ii) Kuwaelimisha wadau kuhusu majaribio na umuhimu wake.

(iii) Kuwaandaa walimu na wakuu wao kwa majaribio ili wajue ni yapi watakuwa wakijaribu. Ni muhimu wajue mtalaa huu mpya na zana za kufundishia.

(iv) Kupeleka zana za kufundishia kwa shule zinazofanya majaribio.

(v) Kutekeleza majaribio ambapo mtalaa mpya na zana za kufundishia huanza kutumiwa mara moja katika shule hizo.

(vi) Kukusanya na kuchanganua matokeo ya majaribio. Mapendekezo yatatumiwa kurekebisha na kuboresha mtalaa huo mpya.

(vii) Urekebishaji wa mtalaa mpya na zana za kufundishia yatafanywa na wataalamu wa mitalaa.

Baada ya marekebisho ya mtalaa na zana za kufundishia, mtalaa mpya utaanza kutekelezwa katika shule zote nchini. Hata hivyo siyo shule zote ambazo zitakuwa tayari kutekeleza mtalaa huo. Shule itakuwa tayari baada ya walimu kuandaliwa kwa kupewa mafunzo ya mtalaa mpya na pia baada ya ununuzi wa zana za kufunzia. Hatua hii ya majaribio ni muhimu sana katika ukuzaji wa mitalaa na ikiwa itaapuzwa kutakuwa na athari mbaya katika mtalaa huo mpya.

### 2.3.6 Utekelezaji

Ni wazi kuwa ukuzaji wa mtalaa hauwezi kuwa kamili bila utekelezaji. Katika hatua hii mtalaa mpya na zana za ufundishaji pamoja na vifaa vya ufundishaji huanza kutekelezwa shuleni na Vyuo vya walimu. Katika shughuli hii, kuna hatua zinazozingatiwa ambazo ni:

(i) Kuwahimiza watu wakubali mtalaa huo.

(ii) Kuelimisha wananchi juu ya mtalaa mpya.

(iii) Kuwaandaa walimu jinsi watakavyoutekeleza.

(iv) Kupelekea shule vifaa na zana zitakazotumika katika utekelezaji.

(v) Kupeleka mtalaa mpya kwa walimu kwa njia ya silabasi na miongozo ya walimu.

(vi) Kuendelea kuwaunga mkono walimu katika juhudi zao za kufunza mtalaa mpya na kushirikiana nao kutatua shida zinazotokea utekelezaji unapokuwa mgumu.

(vii) Katika mtalaa wa lugha ya Kiswahili jukumu la wakuza mitalaa kwa walimu litakuwa;

    (a) Kuwafunza katika maswala ya isimu.

    (b) Kuwaandaa kufunza lugha.

    (c) Kuwaongoza jinsi ya kutumia zana na vifaa vya kufunzia lugha.

Ni muhimu kujua kuwa wataalamu na walimu walioshiriki katika uundaji wa mtalaa mpya wanaweza kutumiwa kuwafunza walimu wenzao jinsi watakavyotekeleza mtalaa mpya. Walimu vile vile watafunzwa jinsi ya kuwatathmini wanafunzi. Itakuwa ni muhimu walimu waendelee kufunzwa kutumia mtalaa huo mpya mpaka tathmini ya mtalaa ifanywe ili ubora wake ubainike.

Matatizo yanayoweza kukumba utekelezaji wa mtalaa mpya ni kama:

(a) Ukosefu wa walimu wa kutosha.

(b) Ukosefu wa pesa

(c) Ukosefu wa vifaa na zana za kufundishia.

(d) Mielekeo hasi kutoka kwa wanafunzi na walimu kuhusu mtalaa mpya.

(e) Waandishi na wachapishaji kutoshirikiana na wakuza mitalaa.

### 2.3.7 Tathmini

Hii ni hatua ya mwisho katika ukuzaji wa mtalaa mpya. Tathmini ya mtalaa ni shughuli ya kukusanya na kuandaa ripoti inayoonyesha kama mtalaa ulioundwa na kutekelezwa una manufaa. Tathmini hii pia husaidia kukusanya ripoti inayoonyesha udhaifu wa mtalaa na kuurekebisha.

Tathmini ina dhima tatu kuu:



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

(i) Kujua hali ya mradi wa mtalaa.

(ii) Kurekebisha mtalaa ikiwa ni lazima ama kutoa uamuzi wa kuendelea kuutumia ikiwa hakuna matatizo makuu.

(iii) Kuchunguza jinsi ukuzaji ulivyofanywa ikiwa kazi yote ya ukuzaji imekwisha.

Itaonekana kuwa tathmini ya mtalaa mpya ni jambo la lazima ikiwa mtalaa mpya unatazamiwa kutimiza malengo yake. Ikiwa kuna hatua zilizohitaji marekebisho kutokana na kasoro ambazo hazikugunduliwa, hatua hii itaruhusu marekebisho kwa kasoro hizo. Hatua hii itasaidia uundaji na ukuzaji wa mtalaa mwingine ili kasoro kama hizo zisirudiwe.

Katika mtalaa wa lugha, hatua hii ni muhimu kwa njia zifuatazo:

a) Lugha iliyotumiwa kuandikia vitabu huchunguzwa iwapo ni sanifu na inalenga kiwango cha wanafunzi walengwa.

b) Shughuli za kufundisha iwapo zinasaidia ufunzaji wa yaliyomo kwenye mtalaa.

c) Mifano na maelezo katika vitabu vya kufundishia iwapo inatosha na kuafikiana na mada ya ufundishaji.

d) Vitabu na matini zingine iwapo zinawavutia walimu na wanafunzi.

e) Vifaa visivyohusiana na matini iwapo vina umuhimu wowote katika ufundishaji wa lugha.

f) Miongozo ya walimu ama inasaidia au ni kikwazo kwa ufundishaji.

g) Vitabu vya wanafunzi iwapo vinasaidia ufundishaji wa mada zinazopendekezwa na mtalaa.

h) Mazoezi yanayopatikana baada ya ufundishaji wa mada ama yanatathmini yanayopaswa kutathminiwa na lugha iliyotumika katika mazoezi hayo au ni ya kiwango cha hawa wanafunzi.

Jambo jingine muhimu katika tathmini ni uandalizi wa walimu. Ni vizuri kutathmini iwapo walimu waliandaliwa vya kutosha kutekeleza mtalaa mpya. Mkuza mtalaa wa lugha ni heri apate tajriba ya walimu ambao watasaidia utekelezaji wa mtalaa mpya. Nyanjani atapata walimu katika viwango vifuatavyo:

a) Walimu wenye ujuzi wa kutosha wa lugha ambao wanafunza lakini hawahitimu kufunza lugha.

b) Walimu wenye ujuzi wa kutosha wa lugha na wamehitimu kufunza lugha lakini hawajamakinika kufunza yaliyomo yaliyopendekezwa katika mtalaa mpya.

Viwango hivi viwili vya walimu vinadhihirisha kwamba walimu watakaotumiwa kutekeleza mtalaa mpya wa lugha lazima watathminiwe katika:

a) Ujuzi wao wa lugha.

b) Ujuzi wao wa lugha na elimu ya kufunza lugha.

c) Uelewa wao wa malengo, yaliyomo na mbinu za ufunzaji wa mtalaa mpya wa lugha.


d) Mielekeo yao dhidi ya mtalaa mpya wa lugha.

Aidha, walimu wanahitaji kuelekezwa jinsi ya kutathmini wanafunzi. Kutathmini huku kutahusu iwapo wanafunzi wana matatizo yoyote ya kuelewa vitabu vya lugha. Walimu vile vile wanahitaji usaidizi kuchanganua matokeo ya mitihani. Matokeo ya mitihani yanaweza kuwaonyesha kuwa pengine vipengele wanavyofunza vinahitaji kufunzwa tena, kufunza sehemu zingine za vipengele hivyo ama kuendelea na somo. Kuelekeza huku huwa na manufaa mawili kwao. Moja ni kuwa huboresha ufundishaji wao na pili hurahisisha kazi ya wakuza mitalaa kwa vile huwasaidia kufuatilia maendeleo ya mtalaa mpya wa lugha.

Sura hii imebainisha jumla ya hatua saba za uandalizi wa mitalaa kulingana na wataalamu mbalimbali. Hata hivyo, taasisi ya elimu Kenya (K.I.E.) yenye jukumu la

kuunda na kufanya mageuzi ya mitalaa na kuisambaza kwa walimu kwa njia ya silabasi na miongozo, imetolea hatua nane kwa muhtasari. Hatua hizi hutegemeana na hujengana kama inavyodhihirika katika ukurasa ufuatao.

**Mchoro 1: Uduara wa Utayarishaji na Urekebishaji wa mtalaa wa somo (K.I.E)**



## 2.4 MUHTASARI

Katika sura hii, dhana ya mitalaa na hatua za ukuzaji wake kulingana na wataalamu mbalimbali zimejadiliwa. Kwa njia hii, sehemu hii imebainisha aina tatu za maarifa ambayo yanafaa kutekelezwa na mada yoyote ya lugha ya Kiswahili kulingana na Bloom na wenzake. Imedhihirika kuwa ukuzaji na uendelezaji wa mtalaa mpya wa somo una hatua saba na kila hatua ni muhimu na wakuza mitalaa hawana budi kuzingatia vigezo hivi. Hata hivyo, Taasisi ya Elimu Kenya ina jumla ya hatua nane. Utayarishaji na uandishi wa silabasi umechukuliwa kama hatua inayojisimamia. Vigezo hivyo vyote vinaingiliana na kuchangiana katika utayarishaji au ubadilishaji wa mtalaa. Ikiwa hatua moja itapuuzwa, utekelezaji wa mtalaa utakuwa na matokeo mabaya kwa wanafunzi. Aidha, walimu wenyewe hawataweza kufunza somo hilo au pengine hukwepa sehemu iliyofanyiwa marekebisho. Mwishowe wanafunzi huanguka mtihani na kwa hivyo malengo ya elimu huenda yasifikiwe.

Baadhi ya masuala na dhana zilizogusiwa katika sura hii zitajitokeza katika sura zinazofuata. Ufundishaji mzuri wa vipengele mbalimbali vya Isimujamii lazima utegemee zana za kufundishia na uelewa wa wanafunzi na mambo haya mawili hutegemea utekelezaji wa hatua za uandalizi wa mitalaa. Uelewa wa walimu kuhusu dhana ya mtalaa na michakato ya kuiandaa na kuhusishwa kwao katika hatua zote

huamua mafanikio ya mtalaa mpya. Katika sura inayofuata, mawanda ya Isimujamii yaliyopendekezwa kufunzwa katika shule za sekondari katika mtalaa mpya yatajadiliwa pamoja na uchanganuzi wa maoni ya walimu na wakuza mitalaa kuhusu vipengele hivyo.

# SURA YA TATU

# MAONI YA WALIMU KUHUSU DHANA YA MTALAA NA MAANDALIZI YAKE

## 3.0 UTANGULIZI

Katika sura ya pili, vigezo vya kuandaa na kuendeleza mtalaa vimepitiwa. Katika hatua ya utekelezaji, zana za kufundishia pamoja na vifaa vya kufundishia huanza kutekelezwa shuleni. Zana na vifaa hivi vinahusu vitabu vitakavyotumiwa na walimu kufunzia pamoja na miongozo na silabasi zitakazowaongoza kufundishia mada mbalimbali. Kwa hivyo, mtalaa mpya hupelekwa shuleni na kuanza kutekelezwa mara moja na walimu. Walimu huchagua mada za kufunza kutoka vitabu wakati wa vipindi mbalimbali.

Kulingana na ufundishaji wa lugha ya mawasiliano, ujifunzaji wa lugha huendeleza ustadi katika kuwasiliana. Si kumaanisha kuwa walimu hawakuwa wanafunza somo hili. Ukweli ni kuwa walikuwa wanafunza lakini hawakuwa wanalipa msisitizo unaofaa. Kulingana na Gathumbi na Masembe (2005), ujifunzaji lugha utaimarika iwapo mwalimu atasisitiza uhusiano uliopo baina ya matamshi, sarufi na semantiki. Kipengee cha matamshi kinahusu fonetiki na fonolojia nacho kipengee cha sarufi kinahusu mofolojia na sintaksia. Kipengee cha Semantiki kinahusu misamiati au uchanganuzi usemi. Walimu hujishughulisha na kipengee cha matamshi na sarufi katika ufundishaji wao. Walimu hukwepa semantiki ambayo ikiwa itafundishwa

itaimarisha mawasiliano. Ni katika sehemu hii ya mwisho Isimujamii itajikita. Lakini swali ni je, ni makosa ya walimu au ni ya wakuza mitalaa?

Walimu hutumia miongozo na silabasi kwa njia isiyokuwa ya kitaaluma. Walimu wakiyasoma malengo ya somo ya kila kidato, wataweza kupata mawanda na kuyajumuisha bila shida katika mpango wa somo. Jambo hili likifanyika, Isimujamii itafunzwa na kuafikia lengo la kuinua ustadi wa mawasiliano wa wanafunzi.

Mapitio ya mtalaa wa 8-4-4 wa shule za sekondari kama unavyodhihirika katika silabasi, na ambao umetayarishwa na KIE umebainisha ufundishaji mwingi wa matamshi na sarufi. Ingekuwa vizuri ikiwa mtalaa ungekuwa na yaliyomo yanayosisitiza lugha ya mawasiliano. Kulingana na Howatt (1984) silabasi mawasiliano (communicative syllabus) inapendekeza mazoezi ya miundo ya lugha katika mawasiliano. Kwa mtazamo huu basi, maoni ya walimu kuhusu ukuzaji wa mitalaa yalichanganuliwa na hitilafu ilikotokea kupatikana. Hatua zilizopitiwa katika sura ya pili zimekuwa malighafi muhimu ya uchanganuzi wa data katika sura hii.

### 3.1 DHANA YA MTALAA NA HATUA ZA KUUANDAA

Asilimia 100 ya walimu waliohojiwa ilisema kuwa inaelewa maana na umuhimu wa mtalaa katika ufundishaji. Hata hivyo walitofautiana kuhusu asasi inayohusika na uundaji wa mitalaa na uandalizi wa silabasi kama inavyobainika katika jedwali 1 hapa chini.

**Jedwali 1: Asasi inayohusika na uundaji wa Silabasi**

| Asasi | Asilimia ya Walimu |
|---|---|
| Taasisi ya Elimu Kenya (K.I.E) | 50 |
| Baraza la Mitihani Kenya (KNEC) | 40 |
| Bila uhakika | 10 |

Asilimia 50 ilionelea kuwa Taasisi ya Elimu nchini (KIE) ndiyo iliyo na jukumu la kuunda na kutayarisha silabasi itakayowaongoza katika kutekeleza mtalaa huo. Asilimia 40 ilisema kuwa Baraza la Mitihani Kenya (KNEC) ndilo linaloamua ni mtalaa upi unaofuatwa nchini. Walipoulizwa na mtafiti kutetea hoja hiyo, walisema kuwa inapofika wakati wa utahini, maswali ambayo hayana uhusiano wowote na mtalaa ama yaliyomo yanaletewa wanafunzi. Wanapolalamika kwa maofisa wa kudhibiti ubora wa elimu, wanaambiwa wafuate yaliyo kwenye mtalaa lakini si kufuata nakala za mitihani. Isitoshe, hawa maofisa wa kudhibiti ubora wa elimu hawajamakinika na vipengele vipya vilivyoingizwa kwenye mtalaa. Kwa mfano, mwalimu mmoja alipotaka kujua ni yepi anayostahili kufunza katika Isimujamii, afisa mmoja alimwambia afanye utafiti maktabani. Mwalimu hakuridhishwa na jibu hilo na hivyo akashindwa iwapo hawa maafisa ni washikadau katika uandalizi wa mitalaa.

Hatua saba zinazohusika na uundaji wa mitalaa kulingana na wataalamu wa taaluma ya ukuzaji mitalaa ni kama vile kutathmini mahitaji, kuunda mradi wa mtalaa,

upangaji wa mtalaa, kuandaa zana za kufundishia, kufanya majaribio, utekelezaji na tathmini. Hatua hizi zimejadiliwa katika sura ya pili. Mielekeo na maoni ya walimu kuhusu hatua hizi yalichanganuliwa kwa njia ya maelezo (Tazama Jedwali 2 hapa chini).

**Jedwali 2: Maoni ya Walimu kuhusu hatua za uandalizi wa Mitalaa**

| Hatua | Idadi ya Walimu (%) | Maoni |
|---|---|---|
| 1 | 70 | Hawakushirikishwa |
| | 30 | Bila uhakika |
| 2 | 80 | Hawakushirikishwa |
| | 20 | Walishirikishwa |
| 3 | 100 | Walishirikishwa |
| 4 | 10 | Hakuna vitabu vya kufundishia |
| | 50 | Yaliyomo ya Chuo Kikuu |
| | 40 | Walishirikishwa |
| 5 | 100 | Majaribio hayakufanywa |
| | 90 | Hawakuelimishwa |
| | 10 | Walielimishwa |
| 7 | 50 | Tathmini ilifanywa |
| | 50 | Hawakutoa majibu |

Pamoja na hayo, mtafiti alichanganua maoni ya wakuza mitalaa kutoka Taasisi ya Elimu Kenya.

Asilimia 70 ya wahojiwa ilisema kwamba inaelewa hatua ya kwanza ni kutathmini mahitaji lakini asilimia 30 ikaungama kuwa haina uhakika na hatua hiyo. Wahojiwa hawa 70% walidai kuwa wakuza mitalaa walipoamua kuanzisha ufundishaji wa Isimujamii hawakuwa na ujumbe wa kutosha. Aidha, ikiwa walitarajia ujumbe wa kutosha kuhusu hali ilivyo ya Kiswahili, wangewaendea walimu na washirikiane nao ili kufanya Isimujamii iwe moja wapo ya somo katika Kiswahili. Katika hatua hii, washikadau wa uundaji wa mtalaa mpya huwa muhimu sana na ni wao wanaoamua ni yepi yakuongezewa au kuondolewa katika somo fulani.

Mhimili wa nadharia ya Isimujamii kuwa, Isimujamii ni kitengo cha isimu kinachoangalia matumizi ya lugha katika jamii, na jinsi miktadha ya jamii inavyoathiri lugha ni muhimu sana katika takwimu za maoni ya walimu kuhusu mahitaji ya mtalaa huu na hasa yaliyomo katika silabasi. Maoni ya walimu yamedhihirisha kuwa, wanaelewa hali ya lugha katika jamii na kwa wanafunzi wanaofundisha. Hii ni kwa sababu Fishman (1971), Gumperz (1982) na Saville-Troike (1982) miongoni mwa wanaisimu jamii wanashikilia kwamba, pana mtagusano wa moja kwa moja kati ya lugha na jamii. Mathooko (2007) pia anaunga mkono jambo hili anaposema kuwa kujipatia na kujifunza lugha ni shughuli ya kijamii kwani, kinadharia, mtoto anajifunza lugha kutegemea ujuzi wake wa kiakili na pia huathiniwa na matukio ya kijamii.

Asilimia hiyo 70 ilikuwa na maoni kuwa ikiwa ingeshirikishwa, ingependekeza vipengele mwafaka vya kufundishwa vya Isimujamii na pia zana kama vitabu vitakavyotumika katika ufundishaji huu. Asilimia hii ingekuwa katika mstari wa mbele kuonyesha umuhimu wa Isimujamii kwa wanafunzi na pia kuoanisha ufundishaji wa lugha ya Kiswahili na Isimujamii na kwa hivyo kurutubisha ufundishaji wa L2 na kukuza uwezo wa wanafunzi wa kuwasiliana.

Ikiwa washikadau wote hawatahusishwa kutoka hatua ya kwanza, matatizo yanaweza kutokea kama yalivyotokea katika mradi wa New Primary Approach (Muthwii, 2002). Muthwii akiwanukuu Hutasoit na Prator (1965) anasema kuwa mabadiliko haya ya ghafla katika ufundishaji wa lugha yalileta matatizo mengi. Kwa mfano, walimu na vitabu vya kufunzia havikutosha. Walimu wasiohitimu kufunza walianza kutekeleza mradi wa NPA baada ya kupewa kozi ya muda mfupi katika vyuo vya walimu. Kiwango cha ufunzaji kikashuka. Ufunzaji ukawa tofauti katika maeneo tofauti. Kwa mfano, shule za mijini zikawa zinafunzwa na walimu waliohitimu kufunza lugha vizuri na za mashambani zikawa na walimu wa lugha wasiohitimu. Katika mkabala huu basi, walimu walisema kuwa mradi wowote wa kielimu ukianzishwa, walimu wanafaa kuwa wa kwanza kushirikishwa. Walitoa sababu kuwa wao ndio walio nyanjani na wanajua uhalisi wa mambo. Wanajua kwa mfano, idadi ya wanafunzi itakayojiunga na shule mwaka ujao. Kwa hivyo, wanaweza kutabiri ongezeko la wanafunzi kutokana na mradi fulani kuanzishwa na serikali kama vile mradi wa masomo bila malipo na kupiku uwezo wa kuwashughulikia. Zaidi ya hayo,

idadi hiyo ya walimu ilisema ni wao wenyewe wanaojua ujuzi wa lugha ya wanafunzi na athari za lugha mama katika ufundishaji wa lugha ya mawasiliano.

Kwa hivyo, ili kufaulisha ufundishaji wa Isimujamii, ni vizuri kujua kuwa mawasiliano na lugha huwa kama shilingi kwa ya pili (Lopez, 2000). Kulingana na Lopez, kuna uhusiano kati ya mawasiliano na lugha. Wanafunzi wanapoanza kuhudhuria shule hujiunga na wengine kutoka jamii tofauti na mwishowe kila mmoja anazungumza lugha yake ya mama. Kunakuwa na vilugha au lahaja. Lopez anasema kuwa ujuzi wa kuwasiliana kwa lugha mama huwapa uwezo wa kujifunza lugha ya elimu (Kiswahili). Muthwii (2002) vile vile anakubaliana na Sifuna (1980), Parry (2000) na Milton (1992) ambao wanasisitiza kuwa matumizi ya lugha mama kama lugha ya ufunzaji imekubaliwa na wanaisimu kuwa hurahisisha ujifunzaji wa L2. Vile vile, lugha L1 huwasaidia kujieleza na hivyo ujifunzaji na ufunzaji huwa rahisi.

Maoni ya asilimia 70 ya walimu yaliwiana na mhimili wa nadharia ya Isimujamii. Hii ni kwa sababu mapitio ya nadharia ya Isimujamii yalidhihirisha kuwa tofauti za lugha kijamii hutokana na tofauti za miundo ya jamii zinazoletwa na elimu, tabaka, uana, umri na mielekeo (Taz. Labov, 1972). Labov, katika nadharia yake ya tofauti za usemi na mitindo ya lugha katika jamii, alithibitisha kwamba lugha zote hutofuatiana kwa namna moja au nyingine, kimuundo na kimatumizi. Kazi ya mwanaisimu jamii ni kueleza tofauti hizi. Walimu walidai kuwa, walipitia kozi za Isimu katika vyuo vikuu na vyuo vya walimu na kutokana na mtagusano na

wanafunzi wa jamii mbalimbali, wameweza kuelewa miundo yao ya lugha na matatizo yanayowatinga katika ujifunzaji wa L2 kutokana na athari za lugha ya kwanza.

Watafitiwa hawa, walimworodheshea mtafiti baadhi ya matatizo ya kifonolojia ya wanafunzi kutoka jamii mbalimbali na kuna imani kwamba makundi yafuatayo yanaweza kutambulishwa na kutofautishwa kwa sauti hizi: Walimu wakadai kuwa tofauti hizi huwa kikwazo kikubwa katika ujifunzaji wa wanafunzi wa L2.

| **Kikundi** | **Sauti** |
|---|---|
| Kikuyu | /v,l/ |
| Luo | /s, sh/ |
| Luhya | /b, p, ɣ/ |
| Meru | /nt, nk, mb, nd/ |
| Kamba | /h, mb, nd/ |
| Kalenjin | /t, d, k, ɣ/ |

Walimu ndio wanaomwelewa mwanafunzi: mazingira na jamii anayotoka na mambo haya huathiri ujifunzaji lugha. Hii ni kwa sababu kulingana na nadharia ya Isimujamii, ujifunzaji lugha unahusu jamii na mtu anayejifunza (Hymes, 1971). Dell Hymes alishikilia vikali kuwa mzungumzaji wa lugha anaathiriwa na mazingira yake



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

vilivyo. Vile vile, Fishman (1971), Gumperz (1982) na Saville-Troike (1982) wanashikilia kwamba pana mtagusano wa moja kwa moja kati ya lugha na jamii. Kujipatia lugha na kujifunza lugha ni shughuli ya kijamii kwani, kinadharia mtoto anajifunza lugha kutegemea ujuzi wake wa kiakili na pia huathiriwa na matukio ya kijamii. Hymes (1971) aliasisi dhana ya ujuzi wa kuwasiliana kuonyesha ujuzi tulio nao wa kutumia lugha katika mazingira maalum na mazingira mbalimbali. Alijishughulisha na kubainisha jinsi mzungumzaji wa lugha anavyozua sentensi (kama ilivyo katika nadharia ya Chomsky) lakini kwa jinsi ambavyo anavyoongozwa na sheria za kuzungumza, kama vile kunyamaza, kupisha wengine katika mazungumzo, na mada anazozungumzia, wapi na nani. Walimu hawa 70% walimfahamisha mtafiti mtazamo huu wa kiisimujamii na kumwambia kuwa wao wangehusishwa katika hatua hii ili kuonyesha hali ya lugha kwa wanafunzi katika maeneo mbalimbali nchini. Mtazamo huu ungesaidia kujua kama kuna haja ya kutilia mkazo ufundishaji wa Isimujamii katika lugha ya Kiswahili na jinsi wangerekebisha makosa ya kisarufi kutokana na athari za lugha mama kwa lengo la kuinua uwezo wa wanafunzi wa kuwasiliana. Mapendekezo yao katika hatua hii yangesaidia kubashiri matatizo yaliyowapata walimu katika utekelezaji kwa vile zana kama vitabu na miongozo haikutosha kama ilivyotokea katika mradi wa NPA. Sababu hii iliwafanya walimu hawa wakubali kwa kauli moja kuwa wao ndio uti wa mgongo katika hatua yoyote ya uundaji na urekebishaji wa mtalaa hususan, hatua ya kwanza.

Asilimia themanini (80%) ya walimu ilionelea kuwa hatua ya pili ya **uundaji wa mradi wa mtalaa** ni hatua nyingine ambayo haikushirikishwa kwao. Walisema kuwa vijihatua kuhusu hatua hii vinahitaji mchango wa walimu ambao wanajua ukweli wa mambo. Kijihatua cha kwanza kinahusu usuli wa mradi huu wa mtalaa wa Isimujamii ambapo wangeonyesha udhaifu wa mtalaa wa lugha ya Kiswahili. Mtafiti alitaka kujua utendakazi wa lugha na iwapo ufundishaji wa lugha ya Kiswahili mbeleni ulikuwa unatimiza lengo la ufunzaji wa lugha. Kwa kuongozwa na mhimili wa nadharia ya mawasiliano kuwa madhumuni makuu ya lugha ni kuwasiliana kwa vile lugha ni mfumo wa kueleza maana, ilibainika kuwa walimu walikuwa na habari kuwa mtalaa huo haukutimiza lengo hilo. Kwa hivyo, wangebainisha kuwa ufundishaji wa miundo pekee hautoshi na kupendekeza vipengele vitakavyofundishwa vyenye uamilifu zaidi wa lugha na jinsi ya kuvifundisha.

Asilimia 100 ya watafitiwa haikuwa na shida na hatua ya **upangaji wa mtalaa** lakini hatua ya **kuandaa zana za kufundishia** ilivutia hisia nyingi. Idadi hii ya walimu ilikuwa na maoni kuwa somo la Isimujamii lilianzishwa ghafla bila kuandaa zana za kufundishia. Vitabu vya wanafunzi na hata miongozo ya walimu haikuwa tayari wakati wa utekelezaji. Asilimia 10 ilikiri kuwa haijaweza kupata hata nakala moja ya kitabu cha Isimujamii kwa wanafunzi wa shule za sekondari na pia mwongozo wa kufundishia haujafika shuleni mwao. Asilimia hamsini (50%) ilikuwa na maoni kuwa vitabu vinavyopatikana katika maduka ya kuuza vitabu na ambavyo vinakusudiwa kutumiwa na wanafunzi wa shule za upili huwa na yaliyomo yanayolenga chuo kikuu.

Pengine tofauti hizi za walimu kuhusu zana za kufundishia zimechangiwa na uwezo wa kiuchumi wa shule.

Mazingira na tajriba ya wanafunzi vile vile huwa ni muhimu kuzingatiwa unapoandaa yaliyomo katika matini za wanafunzi. Asilimia 60 ya walimu ilisema kuwa matumizi na ujifunzaji wa Sheng' katika somo hili unakuwa mgumu kwa wanafunzi wao kwani wametoka maeneo ya mashambani na hawaelewi lugha hiyo ya mijini. Walinukuu sehemu moja ya kitabu cha Isimujamii na wakamwelezea mtafiti kuwa ilikuwa ni vigumu kwa wanafunzi wao kujibu maswali kuhusu kifungu hicho kwa tatizo la kimazingira.

**Mazungumzo:**

| | | |
|---|---|---|
| **Kavue** | : | Ingia forty four! Forthy four mbao stage yote 'mbao'. Ingia forty four! Stage yote mbao au 'sare'. |
| **Fatuma** | : | Tafadhali nina ashuu, niingie? |
| **Kavue** | : | Ingia beste! Kobole, mimi nitasimamia, kumbuka kesho mambo 'sare' hamna. |
| **Shikwekwe** | : | Kwa nini leo wewe konda ni mhostile hivi. Jana ulinilenga … |
| **Kavue** | : | Stori na maboiz sinanga. Dere poa, wacha moto! Dada njoo, usafirie mtumba … nafasi ya mtu mmoja … usiachwe, gari ni ishirini tu … Bei ya chini kuliko mkate. |
| **Dereva** | : | Auntie anasema nini? |

**Kavue** : Ananyonga ashuu.

**Dereva** : Basi mbebe sare.

**Kavue** : Dada, dere amekulipia. Basi dere gari liko seti, stage ya kwanza jijini.

**Maswali**:

(a) Andika muktadha wa mazungumzo haya.

(b) Taja sifa za muktadha wa mazungumzo haya.

(c) Umri mbalimbali umejumuishwa (umetajwa) katika mazungumzo haya. Taja umri huo ukitoa ushahidi.

Hata ingawa utafiti huu haukudhamiria kuchunguza utahini katika Isimujamii, wahojiwa hawa walielezea hofu yao kuhusu mada na mitihani inayotayarishiwa wanafunzi. Walimu hawa walilalamika kuwa huenda wanafunzi wao wasifanye vyema katika mtihani kama huo kutegemea wanafunzi wanakotoka. Ubaguzi huu kulingana na watafitiwa ungesuluhishwa na hatua hii ya nne. Ni heri walimu wawe wa kwanza kuamua yaliyomo au zana za kufundishia. Wakuza mitalaa pia wangetabua udhaifu huu na kuurekebisha kabla ya kutahini Isimujamii na ndiyo sababu wakadai kuwa majaribio ya mtalaa wa Isimujamii kabla ya utekelezaji hayakufanywa.

Asilimia mia moja (100%) iliyohojiwa ilitaja kuwa **hatua ya majaribio** ambayo ingefichua udhaifu wa mtalaa ilipuuzwa. Hawes (1979) anakubali kuwa hili ni tatizo

katika mataifa yote yanayoendelea. Tatizo hili husababishwa na ukosefu wa muda, rasilmali na wataalamu. Mapitio ya utafiti huu katika sura ya pili yamethibitisha hoja hii kwa vile iligunduliwa kuwa, kuna kuwaelimisha wadau na taifa ili wajue majaribio hayo yanahusu nini, kuandaa zana na kuzipeleka shuleni halafu zitumiwe kufanya majaribio. Hizi ni baadhi ya shughuli zinazohitaji pesa nyingi. Wakuza mitalaa kwa hivyo wanaepuka hatua hii kwa sababu ya gharama kubwa. Matokeo yake ni upungufu wa mtalaa ambao walimu walidai ungetambulishwa na kurekebishwa ikiwa majaribio yangefanywa.

Maoni ya walimu kuhusu hatua ya **utekelezaji wa mtalaa** yalikuwa na mchango mkubwa kwa utafiti huu. Ilibainika kuwa asilimia 90 katika maeneo mbalimbali hawakuelimishwa kuhusu mtalaa huu. Aidha, hawakuandaliwa namna ya kuutekeleza. Licha ya kuwatuma maofisa wa kudhibiti ubora wa elimu, maofisa hawa hawakumakinika na dhana hii ya Isimujamii. Wengi wao waliepuka maswali kuhusu Isimujamii na ujumuishaji wake katika lugha ya Kiswahili. Zaidi ya hayo, walimu walifikiri kwa sababu hawakushirikishwa katika ukuzaji na ubadilishaji wa mtalaa huu, Wizara ya Elimu ingeendelea kuwaunga mkono katika juhudi zao za kufunza na kushirikiana nao katika kutatua shida za utekelezaji huu jambo ambalo halikutokea. Matatizo mengi yakatokea ambayo yalifungamana na swala la utafiti huu. Baadhi ya matatizo hayo ni kama ukosefu wa vitabu na mada kutoratibishwa kwa njia ambayo ingewasaidia kufundisha vizuri. Tatizo lingine ni waandishi na wachapishaji kutoshirikiana na wakuza mitalaa na kwa hivyo vipengele

walivyoviandikia havilengi kiwango cha wanafunzi wa shule za sekondari na ujumuishaji wa vipengele hivyo unawawia vigumu walimu katika lugha ya Kiswahili. Walimu walisema kuwa utekelezaji huu pamoja na shida zilizotokea za kiutekelezaji zinawapa kiwewe kwa vile lengo la ufundishaji wa L2 la kukuza uwezo wa kuwasiliana wa wanafunzi huenda lisitimizwe.

Mtafiti alipowahoji kuhusu **hatua ya tathmini** ya mtalaa, asilimia 50 ya walimu haikuchangia hoja hii. Mtafiti aling'amua kuwa waliogopa kuchukuliwa kama wenye mtazamo hasi kwa Wizara ya Elimu na taaluma yao pengine hairuhusu jambo hili. Walisema wanangojea iwapo Wizara ya Elimu itachukua tahadhari yoyote kwa mtalaa huu. Matarajio yao ni kuwa KIE itachunguza jinsi ukuzaji na uandalizi wa mtalaa huu ulivyofanywa ikiwa watautathmini na kujua ukweli wa mambo. Walisema wamekuwa wakingojea ripoti yoyote kuhusu mtalaa huu lakini hawajapata. Lakini watafitiwa walipoulizwa kama wamewahi kutuma maoni yao kuhusu upungufu kwa Taasisi ya Elimu, asilimia 50 ilisema haijathubutu kwa kuchelea "kufuatwa" na wakuu wao.

Utafiti zaidi nyanjani ulidhihirisha uhalisi wa mambo kuhusu madai ya walimu kuhusu hatua za uandalizi wa mitalaa. Kulingana na afisa mmoja kutoka KIE anayehusika na utayarishaji wa mitalaa ya lugha, hatua hizi ni muhimu lakini siyo lazima zote zifuatwe na zihusishe walimu. Ilibainika kuwa, mabadiliko katika mtalaa wa Kiswahili yalitokea kwa vile walimu wengi katika ufunzaji wao hawakuhimiza

ufunzaji na ujifunzaji wa lugha kwa lengo la kuwasiliana. Jambo hili ni kulingana na mhimili wa nadharia ya lugha ya mawasiliano. Kwa hivyo, ikapendekezwa mageuzi yafanywe kwa lugha ya Kiswahili na Isimujamii ikaanza kufundishwa. Mageuzi haya hayakuhusu mtalaa mzima wa somo la Kiswahili na kwa hivyo haingekuwa ni lazima kufuata hatua zote. Zaidi ya hayo, walimu huchukuliwa kuwa ni wasomi na wanafaa kutumia silabasi na kutafitia yaliyomo ya Isimujamii wakiongozwa na malengo ya somo katika kila kidato. Kutokana na jambo hili, hawangekuwa na budi kufuata misingi ya nadharia ya Isimujamii kama vile kufunza lugha wakiihusisha na jamii kwa lengo la kuboresha uhusiano na wanajamii. (Taz. Hymes, 1971). Baadhi yao walikuwa sasa waongozwe na msingi wa nadharia ya mawasiliano kuwa vipashio muhimu vya lugha siyo vile vya kisarufi na kimuundo tu, lakini pia vile vya kimawasiliano. Kwa mtazamo huu basi, walimu wanafaa watumie tajriba zao na watende kazi kitaaluma na jambo hili litawaepusha na malalamiko kuhusu uandalizi na ukosefu wa zana za kufundishia.

## 3.2 MAANDALIZI YA WALIMU

Utafiti uliofanywa nyanjani ulifichua kuwa walimu wana maoni tofauti kuhusu maandalizi yao kama inavyoonekana katika jedwali 3 hapa chini.

**Jedwali 3: Namna uandalizi wa Walimu ulivyotolewa**

| Njia ya Uandalizi | Idadi ya Walimu |
|---|---|
| Kozi ya Isimujamii katika Chuo Kikuu | 50 |
| Bila mafunzo yoyote ya Isimujamii lakini wako na digrii ya elimu | 30 |
| Diploma ya ufundishaji lakini bila mafunzo ya Isimujamii | 20 |
| Wenye kozi ya ufunzaji wa Isimujamii kupitia semina | 40 |

Asilimia 50 ya walimu ilikiri kuwa ilisoma Isimujamii kama kozi katika vyuo vikuu. Asilimia thelathini (30%) ya walimu ilisema kuwa haijapata mafunzo yoyote ya Isimujamii kwa vile walipohitimu shahada ya digrii ya ufundishaji, vyuo vikuu havikuwa vimeanza kufundisha kozi hii. Asilimia ishirini (20%) ya walimu ilidai ilisomea diploma katika ufundishaji na haikupata maandalizi yoyote ya somo hili kama somo mahsusi la kufundisha.

Kulingana na misingi ya nadharia ya ufundishaji wa lugha ya mawasiliano, mbinu za ufundishaji kama vile matumizi ya lugha kwa wingi darasani hupendekezwa kwa vile mtu hujifunza lugha kwa wingi darasani vizuri kwa kuitumia. Ni vizuri kwa hivyo waandaliwe vizuri kufunza L2. Walimu waliosema walikuwa wamehudhuria semina, warsha au kozi fupi za kuwapiga msasa kuhusu mtalaa mpya wa Isimujamii walikuwa asilimia arobaine (40%) pekee. Wale waliosalia walikubali hawakupata mafunzo

kuhusu vipengele vya Isimujamii kwa njia yoyote ile. Waliodai walihudhuria semina na kongamano hata hivyo walikuwa na wasiwasi kwani licha ya kuhudhuria semina hizo, waandalizi walikuja kunadi vitabu walivyoandika vya Isimujamii badala ya kuwaelekeza jinsi ya kushughulikia somo hili. Hata hivyo, walimu walisema walielewa kuwa hata waandalizi hawakuwa wamemakinika na mtalaa huu. Mtafiti aligundua kuwa, upungufu wa kitaaluma wa walimu umezua utaratibu katika ufundishaji. Kwa mfano, katika shule ambazo zina walimu wawili au zaidi, mwalimu mmoja amefunza sarufi shule nzima, mwingine Isimujamii au fasihi na kadhalika. Hali hii ilijitokeza katika shule za kitaifa na za kimkoa. Ilibainika kuwa mwalimu ambaye amemakinika katika ufundishaji wa lugha ya mawasiliano, hubadilishana na mwenzake vipindi ili amfunzie Isimujamii.

Uchanganuzi zaidi wa data ulionyesha kuwa walimu waliosema walipata kuhudhuria semina na warsha walitoka shule za ngazi ya kitaifa na kimkoa. Sababu ya hali hii inajulikana. Shule za aina hii zina uwezo wa kifedha wa kuwadhamini walimu au hata kuwaalika wataalamu. Mtafiti ana ushahidi kuwa shule kama vile Shule ya Mangu, Shule ya Wasichana ya Maryhill, Shule ya Wavulana ya Chania, Shule ya Wasichana ya Chania, Shule ya Thika na Shule ya Wasichana ya Gatanga zimewahi kuandaa warsha kwa walimu wake wa Kiswahili. Asilimia 50 ya walimu shule za kiwilaya ilisema haijapata kuhudhuria warsha na hata asilimia 50 iliopata fursa ilidai kuwa muda wa warsha ulikuwa mfupi na haikufaidika. Uchanganuzi wa ratiba za masomo ulionyesha kuwa, ni 40% pekee ambazo zilikuwa na mbinu kama vile

uigizaji na majadiliano zinazohusu matumizi ya lugha kwa wingi darasani. Hii ni kulingana na mhimili wa lugha ya mawasiliano. Hii huenda ikawa ni asilimia ya walimu waliobahatika kuhudhuria semina na makongamano ya ufundishaji wa Isimujamii.

Utafiti huu vile vile ulidhihirisha kuwa 90% ya walimu wa lugha ya Kiswahili wilayani ina ujuzi na tajriba ya kutosha. Kati ya walimu waliohojiwa, asilimia 20 ina shahada ya uzamili katika lugha ya Kiswahili (M.A – Kiswahili). Asilimia 50 ina shahada ya kwanza na asilimia 30 ina stashahada yaani diploma. Walimu hawa wana tajriba ya miaka 10 wastani. Mwalimu ambaye amehudumu kwa miaka michache amekuwa nyanjani kwa miaka 4.

Uchambuzi wa taarifa za utafiti zilizokusanywa unaashiria kuwa walimu hawajaridhishwa na utaratibu wa masomo ya Kiswahili katika vyuo vikuu katika idara mbalimbali ukilinganishwa na utaratibu wa somo la Kiingereza. Walidai kuwa, wakurufunzi wa somo la Kiswahili hawapati fursa ya kuchukua kozi zote katika somo hili kwa sababu ya utaratibu unaowahitaji kuchukua somo la pili kama vile historia, dini, jiografia na kadhalika. Sababu hii inafanya walimu wengi kufuzu kabla ya kujifunza Isimujamii na vipengele vyake. Ukweli ni kuwa, ingawa walimu hawa walisomea taaluma hii ya Isimujamii, muda mrefu nyanjani umeyatia maarifa yao kutu licha ya kupitwa na mambo mapya. Kwa kweli wahojiwa 90% walionekana wenye upungufu wa kufundisha lugha ya Kiswahili kukuza uwezo wa mwanafunzi

wa mawasiliano lakini siyo kupita mitihani. Sababu hii pengine ndiyo inayofanya warudi vyuoni kusomea shahada ya pili katika somo la Kiswahili. Asilimia 50 ya wahojiwa ilisema kuwa wanasomea uzamili wakati wa likizo katika vyuo vikuu kama Moi, Maseno, Nairobi, Kenyatta na Masinde Muliro.

### 3.3 VIFAA NA VITABU VYA KUFUNDISHIA

Ijapokuwa utafiti huu haukudhamiria kuchunguza mbinu za ufundishaji, mtafiti alipata hisia za walimu kuhusu vifaa na vitabu kama upungufu unaolemaza utekelezaji wa mtalaa wa Isimujamii. Hii ni kwa sababu, mihimili ya nadharia ya ufundishaji wa lugha ya mawasiliano inaonyesha uwiano mkubwa na vifaa na vitabu. Kwa mfano, vitabu na vifaa vinafaa kuwawezesha walimu kutumia drili ambapo mwalimu humdhibiti mwanafunzi katika matumizi mwafaka ya lugha lengwa hadi atakapoitumia inavyotakikana. Vifaa hivi pia vinafaa kuibusha kuwasiliana kwingi darasani kati ya mwalimu na wanafunzi. Kwa hivyo, kazi ya mwalimu itakuwa kuzua miktadha mbalimbali darasani itakayoibusha mawasiliano kati yao. Majibu ya wasailiwa kuhusu vifaa na vitabu vya kufundishia yalielekea kuafikiana kwa kiasi kikubwa kama inavyoonekana katika jedwali lifuatalo.

**Jedwali 4: Matatizo ya Vifaa na Vitabu**

| Aina ya Tatizo | Idadi ya Walimu (%) |
|---|---|
| Vifaa vya kiteknolojia kama vile kanda | 80 |
| Wasiojua kutumia tarakilishi | 20 |
| Ukosefu wa vitabu | 45 |



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

Walimu 80% walitaja tatizo la vifaa. Walisema kuwa, baadhi ya vifaa hasa vya kiteknolojia kama vile kanda kutoka Taasisi ya Elimu nchini havipatikani. Walimu 20% walidai shule zao zina tarakilishi. Hata hivyo, walisema hawajatumia kompyuta wala mtandao kama nyenzo za kufundishia Isimujamii. Takwimu hizi zinaonyesha kuwa walimu hawapati mambo mapya hasa kuhusu masuala ibuka yanayopitishwa kwa wingi katika mtandao. Kutokana na ukosefu wa vifaa muhimu, walimu hawa hulazimika kutumia **drili** katika ufunzaji wao hata ingawa mbinu hii hupendekezwa na nadharia ya ufundishaji wa lugha ya mawasiliano.

Walimu wa shule za kimkoa na kitaifa walisema wana uwezo na rasilimali za kununua vitabu vya waandishi tofauti tofauti lakini tatizo ni kuwa, ni vichache mno vilivyochapishwa. Asilimia 45% ilisema ina ukosefu wa vitabu. Wahojiwa wote walitaja tatizo la vitabu rejea vya wanafunzi kuwa tatizo sugu kwao kwani walisema kuwa ikiwa kuna vitabu mahsusi vya wanafunzi, wangekuwa wakijisomea Isimujamii wakati wa ziada kwa sababu wakati uliotengewa Kiswahili hautoshi.

Aidha, walimu walisema kuwa kuna uhitilafiano kuhusu jinsi dhana ya Isimujamii na vipengele fulani vilivyoelezewa na waandishi tofauti na jambo hili huwakanganya walimu na wanafunzi. Kuna matumizi ya lugha ngumu katika baadhi ya vitabu. Mada nyingi zinalenga kiwango cha wanafunzi wa vyuo vikuu. Walimu walisema mambo haya huwatatiza wanafunzi zaidi.

## 3.4 NJIA ZA KUFUNDISHIA

Asilimia 100 ya walimu iliikashifu silabasi ya sasa chapisho (2002) kwa kutoorodhesha na kutotilia mkazo njia za kufundishia na zinazoupa uhusika wa walimu pekee kipaumbele. Nadharia ya ufundishaji wa lugha ya mawasiliano inapendekeza uhusishaji wa wanafunzi katika ufundishaji wa lugha. Johnson (1982) ana maoni kuwa, ili ufundishaji wa lugha ya mawasiliano uimarike, mazoezi mengi ya lugha inayofunzwa yanahitajika. Mwalimu atawashirikisha wanafunzi kwa kutumia mbinu kama vile **maigizo**, **utatuzi wa mambo**, **kazi mradi**, **uvumbuzi** au **utafiti nyanjani**. Walimu hawa walipoulizwa kama wanatumia njia hizi, wengi walikiri hawazitumii. Hata hivyo asilimia 30 ilidai inazitumia lakini zingine ni ghali na baadhi ya shule hizi hazijajimudu kifedha. Mtafiti alipotaka kujua kwa nini hawatumii njia zisizohitaji fedha na za kujibunia hawakuweza kujibu. Bishop (1985) anafafanua kuwa walimu wengi huogopa kujaribisha njia mpya maana huziona kama tisho kwa uzoefu wao.

## 3.5 MUDA NA MAJUKUMU YA WALIMU

Kuhusu jambo hili, walimu walikuwa na maoni yafuatayo (Tazama Jedwali 5 hapa chini).

**Jedwali 5: Muda na Majukumu ya Walimu**

| Maoni | Idadi ya Walimu (%) |
|---|---|
| Vipindi vichache vya Kiswahili | 90 |
| Muda usiotosha wa kufanya mazoezi ya Kiswahili | 70 |
| Majukumu ya walimu kando na kufunza | 40 |

Kati ya walimu waliohojiwa, asilimia 90 kati yao ilikiri kuwa vipindi vilivyotengewa Kiswahili havitoshi. Kulingana na maoni yao, mwalimu wa somo la Kiswahili analazimika afundishe somo la pili alilohitimu chuo cha ualimu. Isitoshe, somo la Kiswahili ni pana mno: Fasihi ya Kiswahili, lugha yenyewe pamoja na Isimujamii. Upana huu unawafanya wasiweze kufanya utafiti na maandalizi ya kina ya Isimujamii.

Kwa hivi sasa, ratiba ya shule za sekondari inatenga vipindi rasmi vitano vya Kiswahili kwa kidato 1 na 2 na vipindi sita kwa kidato 3 na 4. Asilimia 70 ya wahojiwa ilisema kuwa muda huu hauwatoshi wanafunzi kufanya mazoezi ya lugha. Mtafiti aligundua kuwa, nyingi ya shule alizotembelea hufundisha wakati wa ziada. Wakati wa ziada ni wakati wa likizo na jioni. Shule za bweni hufanya maandalizi ya walimu kufunza jioni baada ya chajio na asubuhi saa kumi na mbili. Jambo hili huzipa shule za bweni uwezo wa kukamilisha silabasi ya shule za upili mbele ya shule

za kutwa. Walimu walidai sababu hii hufanya shule hizi kufanya vyema katika mtihani wa kitaifa.

Majukumu mengine ya walimu ni jambo jingine lilowafanya walimu wadai hawapati muda wa kuzingatia ufundishaji vilivyo. 40% ya walimu ilisema kufanywa wakuu wa idara kama vile michezo, kilimo na mabweni huwakosesha muda wa kutosha wa ufundishaji wa Isimujamii. Walisema walimu wenzao hawataki kutwikwa vipindi vingi na hivyo hudai haki kufanywa katika ugawanyaji wa vipindi hivyo. Jambo hili linawafanya walimu hawa kushughulikia lugha ya Kiswahili bila kutilia mkazo Isimujamii ambayo inalenga kuinua uwezo wa wanafunzi wa kuwasiliana.

### 3.6 MUHTASARI

Katika sura hii, uhusiano baina ya mtalaa na ufunzaji umebainika. Zaidi ya hayo, vigezo vinavyopima utendakazi wa mtalaa vimepitiwa na kuhusishwa na mtalaa mpya wa Isimujamii katika shule za sekondari. Muumano kati ya vigezo hivi au hatua hizi umedhihirika na utekelezaji au ufundishaji halisi wa somo la Isimujamii. Maoni ya walimu kuhusu dhana ya mtalaa na maandalizi yake yalibainisha hoja hii. Imebainika kuwa, walimu ndio wanaotekeleza au wanaofundisha mtalaa wowote ule unaokuzwa, kubadislishwa au kuundwa na wakuza mitalaa kama vile KIE. Jambo hili limepewa nguvu na msingi wa nadharia ya Isimujamii kuwa uchaguzi na matumizi ya lugha hutawaliwa na maumbo na miundo ya jamii zinazoletwa na elimu, tabaka, uana, umri na mielekeo. Kutokana na mhimili huu, ilibainika walimu ndio wanaelewa hali ya

lugha ya wanafunzi hasa matatizo ya kifonolojia na kwa hivyo wangeweza kupendekeza mahitaji na umuhimu wa somo hili. Kwa hivyo, wangekuwa chemichemi ya yaliyomo ya mtalaa huu. Sababu hii iliwafanya wawe na maoni kuwa ikiwa kuna mabadiliko yoyote yangenuiwa kufanywa, wangeendewa kwanza kwa vile ni wao wana ujuzi na wanajua ni yepi yanayofaa kuondolewa au kuongezewa. Sababu za kutowahusisha ama kutoshughulikia hatua ya kutathmini mahitaji au majaribio ndiyo kwa mfano, iliyozua matatizo katika mtalaa wa Isimujamii kiutekelezaji.

Kabla ya mtalaa wowote mpya kuanza kutekelezwa shuleni, maandalizi ya walimu ni muhimu sana. Asilimia 40 pekee ya walimu ilisema imewahi kuhudhuria warsha au semina kuhusu ufundishaji wa Isimujamii. Licha ya kuhudhuria semina hizo, waandalizi hawakufahamikiwa ni yepi wayafunze walimu na kwa hivyo walimu wakadai kuwa waandalizi hawa walikuja kunadi vitabu vyao vya lugha ya Kiswahili. Ilidhihirika kuwa ni asilimia 40 iliyobahatika kuhudhuria semina na ilitoka shule za ngazi za kimkoa au kitaifa kutokana na uwezo wao wa kifedha. Uchanganuzi wa ratiba za masomo umethibitisha kuwa, mbinu kama vile maigizo, mijadala na michezo ya lugha zilipatikana katika asilimia arobaine (40%) ya walimu pekee. Mbinu hizi kulingana na msingi wa nadharia ya ufundishaji wa lugha ya mawasiliano huwezesha kuwe na matumizi mengi ya lugha ambayo hufaulisha ufundishaji wa L2. Hii ni asilimia ya walimu iliyoweza kuandaliwa kupitia semina na makongamano.

Imedhihirika pia kuwa ukosefu wa vifaa na vitabu vya kufundishia unalemaza utekelezaji wa mtalaa mpya wa Isimujamii katika shule za upili nchini Kenya. Hata kama zingine zina tarakilishi, 20% ya walimu ilisema haijatumia tarakilishi kama nyenzo za kufundishia Isimujamii. Imedhihirika kuwa, ukosefu huu wa vifaa muhimu huwafanya walimu kutumia **drili**, mbinu ambayo hupendekezwa na nadharia ya lugha ya mawasiliano. Kwa hivyo, Wizara ya Elimu inafaa kuwahimiza wakuu wa shule hizi kuwapeleka walimu kupata kozi za mawasiliano ya kiteknolojia ili wamakinike katika matumizi ya vifaa kama hizi. Sura ifuatayo imechanganua maoni ya walimu na wakuza mitalaa kuhusu yaliyomo kwenye silabasi. Zaidi ya hayo, maoni ya walimu kuhusu uboreshaji wa mtalaa wa Isimujamii yamechanganuliwa katika sura iyo hiyo.

# SURA YA NNE

## MAONI YA WALIMU NA WAKUZA MITALAA KUHUSU MAWANDA YA ISIMUJAMII KATIKA SHULE ZA UPILI

### 4.0 UTANGULIZI

Katika sura ya pili, vigezo vya kuandaa na kuendeleza mtalaa vimepitiwa. Katika hatua ya utekelezaji, zana za kufundishia pamoja na vifaa vya ufundishaji huanza kutekelezwa shuleni. Zana na vifaa hivi vinahusu vitabu vitakavyotumiwa na walimu kufunzia pamoja na miongozo na silabasi zitakazowaongoza kufundishia mada mbalimbali. Kwa hivyo, mtalaa mpya hupelekwa shuleni na kuanza kutekelezwa mara moja na walimu. Walimu huchagua mada za kufunza kutoka vitabu wakati wa vipindi mbalimbali.

Katika sura hii, baadhi ya mawanda ya Isimujamii yaliyopendekezwa kufunzwa katika mtalaa wa Isimujamii mpya katika kila kidato yamepitiwa na kuchanganuliwa kwa kuongozwa na mihimili ya nadharia ya Lugha ya Mawasiliano na nadharia ya Isimujamii. Maoni ya walimu kuhusu yaliyomo wanayofunza yamechanganuliwa. Utafiti ulidhamiria kupata sifa bainifu zinazotawala matumizi ya lugha katika miktadha mbalimbali kulingana na mtalaa wa Isimujamii na kuchanganua maoni ya walimu kwa kusudi la kutoa mapendekezo kuhusu mawanda hayo. Uchanganuzi wa aina hii ulihusisha utafiti wa nyanjani, mahojiano yaliyoongozwa na maswali kutoka

kiambatisho I na II na hatimaye uchanganuzi wa data na matokeo ambayo yanaweza kuimarisha ufundishaji wa Isimujamii katika shule za sekondari.

Katika kuamua ni mawanda yepi yanayoshughulikiwa katika shule za sekondari, mtafiti aliongozwa na mwongozo wa walimu uliotayarishwa na wakuza mitalaa wa K.I.E (Taz. K.I.E. 2006). Kulingana na mwongozo huo, lengo kubwa la kuwafunza vijana Isimujamii ni kule kutumia Sheng' bila kuzingatia muktadha. Mwongozo huo unasema,

> **Vijana wengi mijini na hata mashambani wameingilia matumizi ya sajili ya Sheng' bila kubainisha wanatumia kwa nini, lini, na inahusu mada gani n.k. (Uk. 28)**

Kulingana na mwongozo huo, hii ndiyo sababu mtaala mpya umeshirikisha mafunzo ya Isimujamii katika mafunzo ya Kiswahili. Wakuza mitaala wanapendekeza walimu watumie silabasi na miongozo katika uchaguzi wa mada. Walimu wakuu wanastahili kuwanunulia walimu silabasi na miongozo lakini wengi wao huwanunulia silabasi pekee. Walimu wanastahili kujumuisha Isimujamii katika ratiba yao ya kazi ili waifunze wakati wa somo la Kiswahili. Hata hivyo, walimu wengi hushindwa kujumuisha Isimujamii katika maandalizi na ufunzaji wa somo hili.

Sura hii imechanganua majibu ya walimu kuhusu mawanda ya Isimujamii kama yanavyoorodheshwa na mwongozo wa mwalimu. Mafunzo ya Isimujamii katika shule za sekondari hupatikana chini ya stadi za kusikiliza na kuzungumza na sehemu

ndogo ya sarufi (K.I.E. 2006). Kulingana na mwongozo huu wa mwalimu, kinachohitajika ni kubainisha sifa zinazotawala matumizi ya lugha katika miktadha iliyoorodheshwa katika kila kidato, kwa mfano:

| | |
|---|---|
| Kidato cha Kwanza: | Sifa za matumizi ya lugha katika miktadha ya nyumbani, dukani, mitaani, sokoni, shuleni, mahojiano ya watu mbalimbali, mijadala, hotuba n.k. |
| Kidato cha Pili: | Sifa za matumizi ya lugha katika miktadha ya hotelini, hospitalini, posta, kituo cha polisi, shuleni, mahojiano ya watu mbalimbali, hotuba n.k. |
| Kidato cha Tatu: | Sifa za matumizi ya lugha katika miktadha ya maabadini, ofisini mwa mtawala, mahakamani, baina ya wataalamu wawili au zaidi, mijadala, hotuba. |
| Kidato cha Nne: | Sifa za matumizi ya lugha katika miktadha ya viwandani, bungeni, baina ya mwajiri na mwajiriwa, wataalamu wawili, mijadala, hotuba n.k. |

Matumizi haya ya lugha yamepitiwa katika sura hii na kuyaoanisha na uandalizi wa mtalaa na kuchanganua maoni ya walimu kuyahusu kwa kuongozwa na misingi ya nadharia na kuweza kutathmini mafanikio ya mtalaa mpya wa Isimujamii katika shule za sekondari. Zaidi ya hayo, maoni ya maafisa wa mitalaa kutoka Taasisi ya Elimu Kenya kuhusu yanayofunzwa yamechanganuliwa na matokeo kuwasilishwa kwa njia ya mjadala katika sura hii.

## 4.1 YALIYOMO KWENYE SILABASI

Kuna tofauti kati ya dhana ya mtalaa na silabasi. Katika sura ya pili, mtalaa ulifafanuliwa kama maarifa na ujuzi unaopitishwa na mfumo wa elimu kwa wanafunzi. Kwa upande mwingine, silabasi ni mpangilio wa kijumla wa mada zinazotakiwa kufunzwa katika darasa fulani kwa mwaka mzima katika somo mahsusi (Taz. Musau na Chacha, 2001). Hivyo, silabasi humwongoza mwalimu kufahamu kinachofunzwa. Kile kinachofunzwa ndicho tunachokiita mtalaa au yaliyomo. Aidha, silabasi hufafanua malengo ya somo na kutoa vidokezo vya mambo yanayotakikana kufundishwa ili kutimiza malengo hayo. Umuhimu mwingine ni kuwa ratiba ya kazi hutayarishwa kutokana na silabasi. Hili humwezesha mwalimu kutafuta vifaa vya kufundishia na humwongoza katika utungaji wa mitihani na majaribio mengine. Nchini Kenya, silabasi hutayarishwa na Taasisi ya Elimu ya Kenya (KIE) ikishirikiana na Baraza la Kutunga Mitihani la Kenya (KNEC).

Mahojiano ya ana kwa ana na wakuza mitalaa kutoka Taasisi ya Elimu Kenya yamebainisha tofauti zaidi kati ya mtalaa na silabasi. Kulingana na wao, silabasi ni orodha ya yanayotakiwa kufunzwa wanafunzi. Yale (yaliyomo) yanayofunzwa wanafunzi ndiyo huitwa mtalaa. Mtalaa hufikiriwa na kuchunguzwa ili baada ya kufikiria wanayotaka kufunza huorodheshwa kwa namna ya silabasi. Walimu nao hutekeleza mtalaa (yaliyomo) kwa kutumia silabasi ambazo husambazwa kwao wakati wa utekelezaji katika taifa nzima.



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

### 4.1.1 Sifa za matumizi ya lugha katika miktadha mbalimbali

Kulingana na mtalaa wa Isimujamii wa shule za upili, walimu wanafaa kutumia silabasi kuwaongoza kufunza uteuzi na matumizi ya lugha. Aidha, kulingana na nadharia ya Isimujamii, matumizi ya lugha huathiriwa na **mazingira**, **muktadha**, **kichwa cha mazungumzo**, **jinsia**, **lugha azijuazo mtu**, **elimu**, **usuli au mbari**, **tabaka**, **wadhifa**, **kazi**, **mielekeo**, **tajriba**, **malezi**, **umri** na **hadhira**. Kwa hivyo, mwalimu anapofundisha mawanda au vipengele mbalimbali vya Isimujamii, anafaa azingatie mambo haya. Sehemu hii imeonyesha miktadha mbalimbali au sajili mbalimbali. Sajili kulingana na Masinde (2007) ni mitindo maalum ya kutumia lugha kwa mujibu wa muktadha.

Aidha, lengo kuu katika ufundishaji wa L2 ni kumrithisha mwanafunzi uamilifu wa mawasiliano na kwa hivyo maana ya miundo husisitizwa kwa vile lugha ni mfumo wa kueleza maana. Ikiwa mwanafunzi atapata uamilifu wa mawasiliano, ataweza kutagusana na watu, kujitambulisha (Giles, 1990 na Scotton 1993) na pia kujinasibisha na kujitofuatisha ili apate kutuzwa (Giles, 1990 na Ting Tomey, 1989). Swali ni je, mwalimu wa somo la Isimujamii anatimiza malengo haya? Mtalaa wa Isimujamii umeorodheshwa kwa njia nzuri katika silabasi? Haya yatajulikana baadaye kutokana na maoni ya walimu nyanjani. Kwa sasa sajili au matumizi ya lugha katika miktadha mbalimbali yamejadiliwa na maoni ya walimu kuyahusu kujadiliwa baadaye.

### 4.1.2 Sajili za Lugha

Sajili za lugha ni matumizi ya lugha kutegemea muktadha (Buliba, Njogu na Mwihaki, 2006). Miktadha tofaoti tofauti huzua mitindo mbalimbali ya lugha. Kila taaluma au aina ya mawasiliano ina sajili yake. Sajili hujibainisha wazi zaidi kupitia uteuzi wa msamiati kwa upande mmoja na maumbo ya sentensi kwa upande mwingine. Kwa hivyo, mwalimu anapofundisha sifa za matumizi ya lugha katika miktadha mbalimbali huwa anashughulikia sajili za lugha. Mifano ya sajili za lugha kulingana na Masinde (2007), Buliba, Njogu na Mwihaki (2006), Mathooko (2007) na Muiruri na Ndegwa (2005) ni:

- **Sajili ya Mahakamani**
- **Sajili ya Hotelini**
- **Sajili ya Hospitalini**
- **Sajili ya Biashara**
- **Sajili ya Shuleni**
- **Mwajiri na Mwajiriwa**
- **Lugha ya Kimapenzi**
- **Sajili ya Dini**
- **Sajili ya Vijana**
- **Sajili ya Sayansi**
- **Sajili ya Siasa**
- **Sajili ya Matatu**
- **Sajili ya Magazeti**
- **Lugha ya Matangazo**

- **Sajili ya Kandanda**
- **Sajili ya Simu**
- **Sajili ya Maongezi ya Kawaida**

Baada ya mtalaa kutayarishwa kwa kupitia hatua saba ambazo zilijadiliwa katika sura ya pili, mtalaa huo huhifadhiwa kwa njia ya silabasi na mwongozo wa mwalimu. Makala haya huwaongoza walimu katika utekelezaji wa mtalaa. Kulingana na mtalaa wa Isimujamii, mwalimu anafaa ajumuishe ufundishaji wa Isimujamii katika masomo ya lugha jambo ambalo nyanjani liliwafanya walimu kulalamika. Kwa hivyo mwalimu anafaa afundishe sajili ambazo zimeorodheshwa hapo juu. Ni vizuri katika ufundishaji wake awaelezee wanafunzi kuwa matumizi ya lugha huathiriwa na mambo yafuatayo:

**Muktadha**

Kulingana na Aswani, Njogu na Mwihaki (2007), muktadha ni hali inayomzunguka mtu anapoitumia lugha na hivyo kuathiri maana na matumizi ya lugha. Miktadha, kwa hivyo, ni hali mbalimbali zinazofungamana na utamaduni ulioko. Zaidi ya kitu chochote kingine, muktadha ni kitu muhimu kinachoathiri maana na matumizi ya lugha.

Muktadha hutawaliwa na kuelekezwa na:

a) Washiriki

b) Lengo

c) Mada

d) Mazingira na Mandhari

e) Hadhi/Cheo

f) Jinsia

g) Elimu

**Washiriki** humuongoza msemaji anapozungumza. Kwa mfano, lugha anayoitumia mtu mahali pake pa kazi siyo anayoitumia nyumbani na jamii yake. Pia wakili akiwa kortini atatumia lugha tofauti na ile anayoitumia akiwa nyumbani. Lugha yake ya kazini italingana na kazi anayoifanya. Lugha iwe tamkwa au andishi, hubadilika kutegemea washiriki.

**Lengo** huelekeza muktadha pia. Lugha haitumiki bila lengo. Lengo huathiri maana. Kwa mfano, mtu anapozungumza na mwanake, uteuzi wake wa maneno utaelekezwa na lengo au ujumbe anaotaka kupitishia mwenzake.

**Mada** huathiri lugha inavyotumika kwa kiasi kikubwa. Mada za kitaaluma na kiufundi zinahitaji istilahi za kitaaluma.

**Mazingira na Mandhari** nayo huathiri lugha. Kwa mfano, katika mihadhara ya Chuo Kikuu au hafla za kidini, kuna urasmi wa lugha zaidi ya wakati watu wa familia moja wanapostaftahi au kustarehe mkahawani.

**Hadhi** au **Cheo** vilevile huathiri matumizi ya lugha. Watu wasio wa daraja moja, kihadhi, hawana uhuru mwingi katika mazungumzo yao. Mazungumzo yao yana urasmi mwingi. Watu wa daraja moja wana uhuru mwingi katika mazungumzo yao. Katika mazungumzo ya watu wawili wasio wa daraja moja, kuna hali ya mhusika wa daraja ya juu kuwa na satua na uwezo juu ya mwenzake wa daraja ya chini.

**Jinsia** - Utafiti wa kiisimujamii umedhihirisha kwamba matumizi ya lugha hutegemea jinsia. Mazungumzo baina ya wanawake na wanaume aghalabu hutofautiana kimaumbo, kimada, kimaudhui na kimatumizi. Kwa mfano:

a) Wanaume wanapenda kuonyesha taasubi ya kiume katika matumizi yao ya lugha.

b) Aghalabu wanaume hawatumii lugha sanifu. Wanatumia lugha ya mtaani kama vile Sheng'.

c) Mara nyingi wanaume huzungumzia mada kama vile michezo, pesa, kazi na siasa.

d) Wanaume mara nyingi wanapenda kutumia lugha nzito. Aidha wanapenda kutumia lugha ya matusi kwa urahisi zaidi kuliko wanawake.

e) Wanawake wanapenda kutumia maneno laini kama Jamani!, Mungu wangu!, Mama eeh!

f) Wanawake wanapenda kuzungumzia mambo ya mapambo na nguo zaidi ya wanaume.

**Elimu** huathiri matumizi na uteuzi wa lugha pia. Kuna hali ya watu walioelimika kutumia lugha kwa usanifu zaidi. Kwa mfano, lugha ya Kiswahili inayotumiwa katika shughuli za kitaaluma kama vile kutolea mihadhara ni tofauti na ile inayotumika sokoni.

**Umri** huelekeza muktadha. Watu wa umri mmoja hutumia lugha inayofanana. Kwa mfano, wazee hutumia methali, mafumbo na taswira ilhali vijana hutumia lugha nyepesi na inayoeleweka kwa urahisi. Katika mawasiliano kati ya wazee na vijana, vijana hutumia lugha ya adabu na heshima. Mawasiliano kati ya vijana huwa na matumizi mengi ya Sheng'. Lugha hii ni maarufu kati ya vijana wanaoishi shehemu za mijini kama chombo cha **kujitambulisha** kimtaa. Sheng' in **kitambulisho cha ujana**. Pia ni dhihirisho kwamba msemaji ni **mmoja wa wasemaji** wa msimbo wa vijana. Ni njia ya vijana ya **kujihami** na **kujitenga** na watu wazima. Hali hii ya umri hudhihirisha kuwa lugha huweza kutumiwa **kujitofautisha na kujitambulisha** (Gile, 1990 na Ting Tomey, 1989). Kwa mfano, vijana hutumia Sheng' ili kujitofautisha na wazee na ili wajinasibishe na ili waweze kutuzwa na kukubaliwa na vijana wenzao.

## 4.2 MAONI YA WALIMU KUHUSU YALIYOMO YA MTALAA KWENYE SILABASI

Watafitiwa 100% walisema kuwa wameipitia silabasi inayowaongoza kutekeleza mtalaa mpya wa Isimujamii. Walimtolea na kumwonyesha silabasi mtafiti iliyotolewa mwaka 2002 na KIE. Kama ilivyo katika ufafanuzi wa dhana ya mtalaa

na silabasi, utafiti huu ulidadisi kutoka kwa walimu kama wanaelewa maana ya silabasi na dhima yake katika ufunzaji. Asilimia mia moja (100%) ilisema inaelewa kuwa silabasi ni orodha ya yaliyomo. Mtafiti alitaka kujua kutoka kwa walimu iwapo wamemakinika na lengo la ufunzaji wa Isimujamii kwa kuzingatia yaliyomo ya mtalaa yaliyoorodheshwa katika silabasi. Kuhusu jambo hili, mtafiti aliongozwa na mihimili ya nadharia za lugha ya mawasiliano na Isimujamii.

Kwa kurejelea mhimili wa nadharia ya mawasiliano unaosema kuwa, katika ufunzaji wa lugha ya mawasiliano, maana ya miundo husisitizwa kwani lengo kubwa la ufunzaji wa L2 ni mawasiliano, mtafiti alipitia baadhi ya sajili za lugha ambazo zimepitiwa hapo awali na kutaka kujua maoni ya walimu kuhusu jambo hili. Asimilia arobaini (40%) hufunza sajili hizo ikidhani inafunza sarufi ya lugha bila kuweka mkazo katika maana ya maneno au miundo ili kukuza uwezo wa kuwasiliana kwa wanafunzi. Kwa kufanya hivi, mtafiti aligundua kuwa, asilimia hii ya walimu haizingatii msingi wa nadharia ya mawasiliano kuwa **vipashio muhimu vya lugha siyo vile vya kisarufi na kimuundo tu, lakini pia vile vya kimawasiliano**.

Iligunduliwa kuwa, asilimia thelathini (30%) ya walimu hufunza sajili hizo kwa lengo la kukuza uamilifu wa mawasiliano ya wanafunzi. Hawa huenda ikawa ni walimu ambao wamewahi kuhudhuria semina na warsha kuhusu utekelezaji wa mtalaa wa Isimujamii. Vile vile, asilimia hii ya walimu ilimthibitishia mtafiti kuwa, inaposhughulikia sajili hizi, kuna **matumizi ya lugha kwa wingi darasani kwani**

**mtu hujifunza lugha vizuri kwa kuitumia**. Jmbo hili ni kutokana na mhimili wa nadharia ya mawasiliano.

Hata hivyo, 30% ya wahojiwa haikuwa na uhakika iwapo inashughulikia sajili hizo kwa mtazamo wa lugha ya mawasiliano – ili kuinuia kiwango na uwezo wa wanafunzi wa kuwasiliana. Kupitia uchunguzi na kuwadadisi zaidi walimu, mtafiti alihisi kuwa hawa ni baadhi ya walimu wanaofunza somo wakiwa na dhamira ya kuwapitisha mtihani. Zaidi ya hayo, huenda walimu hawa huwekewa sharti katika shule zao kuwa wanafunzi wasipopita mtihani, watatimuliwa kazini au kuhamishwa hadi shule zingine.

Kupitia mahojiano ya ana kwa ana na mtafiti, walimu walibainisha hofu yao. Walipoulizwa iwapo wanafikiria silabasi imewaongoza vilivyo kufundisha vipengele vya Isimujamii chini ya stadi za kusikiliza na kuzungumza, walikuwa na maoni tofauti. Mwalimu mmoja alikuwa na haya ya kusema:

> **La. Mimi sijaongozwa kamwe. Hebu nionyeshe katika nakala hii ni wapi pametajwa mada yoyote ya Isimujamii! Ikiwa wanataka (KIE) tushirikishe vipengele vya Isimujamii katika ufunzaji wetu wa Kiswahili, wangeonyesha ni vipengele vipi vishirikishwe. Kwa hivyo vipengele havijapangwa jinsi vitakavyofunzwa. Katika shule nyingi nchini, huenda baadhi ya walimu wasifunze somo hili kamwe kwa sababu hakuna chochote kinachohusu Isimujamii katika silabasi. Zaidi ya hayo, hakuna mwanzo na mpaka wa ufunzaji wa somo hili na kwa hivyo mwalimu hataridhika kuwa amefunza yanayostahili kwa kukosa mpaka.**

Walimu wengine walikuwa na maoni yafuatayo kuhusu jambo hili kama inavyoonekana katika Jedwali 6 hapa chini

**Jedwali 6: Maoni ya Walimu kuhusu yaliyomo kwenye Silabasi**

| **Maoni** | **Idadi ya Walimu (%)** |
|---|---|
| Mtindo jumuishi | 20 |
| Vipengele kutokuwa na uhusiano na Isimujamii | 5 |
| Vigumu kwa mwalimu mgeni kuendelea na kazi ya mwalimu aliyehama | 60 |
| Ugumu wa kutayarisha ratiba ya kazi | 15 |

(i) Asilimia 20 ilisema kuwa, wakuza mitalaa walitumia mtindo jumuishi walipotayarisha silabasi katika kujumuisha vipengele vya Isimujamii. Kwa hivyo ikiwa mwalimu si mbunifu hataweza kuitumia kutekeleza mtaala huu.

(ii) Asilimia 5 ikawa na maoni kuwa, wanafunzi hawaoni uhusiano kati ya vipengele wanavyofundishwa vya Isimujamii na somo lenyewe la Isimujamii. Baadhi yao wanaposoma kwa mfano, mazungumzo, wanauliza kama ni ufunzaji wa kawaida wa ufahamu ama ni Isimujamii. Lakini utafiti umeweka bayana misingi ya ufunzaji wa lugha ya mawasiliano na Isimujamii na kwa hivyo walimu wakizingatia mihimili hii, wanafunzi wataweza kuelewa umuhimu wake.

(iii) Asilimia 60 ikaonelea kuwa, mwalimu anapohama shule moja hadi nyingine, inakuwa ni vigumu kwa mwalimu atakayechukua jukumu la kufundisha darasa

lililokuwa la mwalimu aliyehama kujua aanze wapi kwa vile vipengele havijaratibishwa vizuri na kirasmi katika silabasi.

(iv) Asilimia 15 ikakiri kuwa, ni vigumu kutayarisha ratiba ya kazi na kujumuisha vipengele vya Isimujamii.

Aidha kulingana na wizara ya elimu, mwalimu anafaa atayarishe ratiba ya muhula mzima ya kazi ya ufundishaji wa Kiswahili kwa darasa moja. Ratiba ya kazi hutayarishwa kutokana na silabasi iliyo na mtalaa fulani kama wa Isimujamii. Hili humwezesha mwalimu kutafuta vifaa vya kufundishia kama vile vitabu, redio na humwongoza katika utungaji wa mitihani na majaribio mengine. Vile vile, ratiba hii itakuwa na malengo ya kazi ambapo patatajwa msingi wa ufunzaji wa Isimujamii au L2. Ratiba hii itamsaidia mwalimu kutekeleza mtalaa wa Isimujamii.

Asilimia 70% ya walimu ilikiri kuwa kujumuisha vipengele vya Isimujamii kunakuwa si kazi rahisi kwa vile wakuza mtalaa wa Isimujamii walipotayarisha silabasi hawakuonyesha ni yepi yashughulikiwe katika darasa gani na lini. Mtafiti aling'amua kuwa, hii ni asilimia ya walimu ambayo haina mwongozo (K.I.E. 2006) ambao umeorodhesha yanayofaa kushughulikiwa na wao (Taz. Uk. 50 wa utafiti huu). Mtafiti aliweza kupewa ratiba na walimu wa shule alizotembelea na kuzipitia ili athibitishe iwapo walimu wanaratibu Isimujamii katika ratiba zao. Utazamaji huu pia ulimsaidia kuona iwapo ufunzaji huu umezingatia mihimili ya nadharia za lugha ya mawasiliano na Isimujamii kwa kuchambua shabaha ya ratiba hizo. Aliweza kutohoa sehemu moja ya ratiba ya kazi ya mwalimu wa shule moja iliyokuwa imeratibiwa

kufundishwa Isimujamii katika vipindi vya wiki na nyingine ya shule ambayo haikuratibiwa kufundishwa Isimujamii. Tazama jedwali 1 na 2 katika kurasa zinazofuatia.

**Jedwali 7:** **RATIBA YA MASOMO**

**SHULE:** Shule ya Upili ya A

**DARASA:** Kidato cha Tatu Mashariki

**SOMO:** Kiswahili

**MWAKA:** 2008

**MUHULA:** Wa pili

| WIKI | KIPINDI | FUNZO | YALIYOMO | SHABAHA | MAREJELEO | VIFAA | MBINU ZA KUFUNDISHIA | MAZOEZI/KAZI | MAONI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 4 | 3 na 4 | KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA: ISIMUJAMII | Maamkizi ya Heshima na Mazungumzo katika mazingira ya:<br>(i) Sehemu za kuabudu.<br>(ii) Maha-kamani | Wanafunzi waweze:<br>(i) Kutaja na kueleza sifa za matumizi ya lugha ya maabadini, ofisini kwa mtawala na mahakamani.<br>(ii) Umu-himu wa mazungumzo katika taaluma ya Isimujamii.<br>(iii) Kuigiza mazungumzo haya. | (i) KIE Kiswahili kwa kidato cha 3 kitabu cha wanafunzi Uk. 50-54.<br>(ii) Mwo-ngozo wa mwalimu Uk. 39-40.<br>(iii) Masinde (2007) Uk. 15-22.<br>(iv) Buliba na wengine (2006) Uk. 47-64. | . Darasa lifanywe na kutumiwa kama maabadini na ofisi.<br>. Wanafunzi na mwalimu. | (i) Drili<br>(ii) Uigizaji | (i) Kuigiza<br>(ii) Kujadiliana<br>(iii) Kujibu maswali | |

Kupitia mahojiano kati ya mwalimu na mtafiti, ilithibitika kuwa siyo walimu wote wanaoshindwa kujumuisha ufundishaji wa Isimujamii. Mwalimu alieleza kuwa alihudhuria kongamano moja la kitaifa kuhusu utekelezaji wa mtalaa mpya wa Isimujamii na kujua jinsi ya kutayarisha ratiba ya kazi. Hata hivyo mwalimu alieleza kuwa kipengele kimoja kama mazungumzo huwa kipana kiasi cha kumfanya mwalimu akishughulikie kwa vipindi viwili. Vilevile, kipengele kama hicho huwa kipana kwa vile kuna mazungumzo ya aina nyingi na wanafunzi hukanganyikiwa. Kwa hivyo, kulingana na mwalimu huyu, wakuza mitalaa wanafaa watenge vipengele mahsusi vya Isimujamii vitakavyofunzwa kutoka kidato cha tatu na cha nne pekee au Isimujamii isifunzwe kabisa.

Utafiti huu ulithibitisha kuwa walimu wanapofundisha mada zingine za lugha hushughulikia Isimujamii bila kujua. Katika hali hii inakuwa ni vigumu kulipa somo hili uzito unaostahili. Mfano mzuri ni wa ratiba iliyokabidhiwa mtafiti na mwalimu wa shule nyingine. Mtafiti alitohoa sehemu ya kipindi kimoja ifuatavyo:

**Jedwali 8:** **RATIBA YA MASOMO**

**SHULE:** Shule ya Upili ya F

**DARASA:** Kidato cha Tatu Magharibi

**SOMO:** Kiswahili

**MWAKA:** 2008

**MUHULA:** Wa pili

| WIKI | KIPINDI | FUNZO | YALIYOMO | SHABAHA | MAREJELEO | VIFAA | MBINU ZA KUFUNDISHIA | MAZOEZI/KAZI | MAONI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 4 | 2 | KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA | Maamkizi ya Heshima na Mazungumzo ofisini kwa mtawala. | Wanafunzi waweze: (i) Kusoma ufahamu wa mazungumzo ya ofisini na kujibu maswali. (ii) Kueleza maana ya semi mbalimbali za Kiswahili zilizotumika. (iii) Kutunga sentensi wakitumia semi zilizotumika. | (i) KIE Kiswahili kwa kidato cha 3 kitabu cha wanafunzi Uk. 60-61. | . Ubao ili kuorodheshea maneno magumu. | (i) Kueleza (ii) Kusoma | (i) Kujibu maswali. (ii) Kutunga sentensi. | |

Majadiliano kati ya mwalimu na mtafiti yaliyonyesha kuwa wakuza mitalaa walipuuza kuwaandaa walimu jinsi ya kushughulikia somo hili. Mwalimu alipoulizwa kama anapofundisha kwa mfano **mazungumzo katika ofisi** ya mtawala anaihusisha na Isimujamii, alikuwa na haya ya kusema:

> **Dhana yenyewe haieleweki kwa wanafunzi. Mimi ninafundisha kipengele hicho kama ufahamu nikiwa na matumaini kuwa ujuzi wa mawasiliano kwa wanafunzi utaimarika na vile vile wanafunzi wataweza kujibu maswali ya Isimujamii pindi mtihani utakapowadia. Shida kubwa ni kuwa waliokuza mtalaa huu hawakutushirikisha ama kutuandalia kozi ya muda mfupi ili kutuelekeza jinsi ya kujumuisha Isimujamii tunapofundisha vipengele vingine vya Kiswahili. Kwa hivyo, huenda baadhi ya sisi walimu tusilipe somo hili uzito na umuhimu linalostahili.**

Shabaha ya ufundishaji wa Isimujamii ilichanganuliwa na mtafiti kupitia utazamaji wa ratiba za kazi za walimu hawa kwa kuhusishwa na mihimili ya nadharia za lugha ya mawasiliano na Isimujamii. Imebainika kwa mfano, mwalimu katika jedwali la 1 badala ya kuwa na shabaha mahsusi inayosema kuwa, "Mwanafunzi aweze kueleza kuwa matumizi ya lugha huathiriwa na mazingira, wadhifa, elimu n.k.", mwalimu huyu alitaja shabaha kijumla bila kuihusisha na muktadha maalum. Ratiba ya mwalimu katika jedwali la 2 nayo haikulenga lengo la ufundishaji wa Isimujamii wala lugha ya mawasiliano. Mtafiti alipotaka kujua athari ya jambo hili, watafitiwa hawakujibu. Waliogopa wasichukuliwe kuwa hawatendi kazi vizuri.

Katika utafiti wake, mtafiti alipata asilimia 30 ya walimu pekee ambayo iliratibu Isimujamii katika ratiba zao za kazi. Asilimia 20 haikuwa imeratibu lakini ikamweleza mtafiti kuwa inapofundisha vipengele fulani vya ratiba hiyo, hujaribu

kuihusisha Isimujamii. Hata hivyo, walipoulizwa na mtafiti watolee mfano wa vipengele hivyo, walichelea na kusema kuwa si jambo jepesi lakini wakamwambia mtafiti abane majina yao wasije kujulikana na kuchukuliwa hatua ya kinidhamu na wakuu wa shule. Asilimia 40 mwishowe ikakiri kuwa hawaishughulikii Isimujamii kwa njia yoyote ile. Asilimia 10 ilisema haikuwa na la kusema kuhusu jambo hili.

## 4.3 MAONI YA WAKUZA MITALAA KUHUSU YALIYOMO KWENYE SILABASI

Utafiti zaidi kwa wakuza mitalaa nyanjani ulidhihirisha maoni tofauti kuhusu yaliyomo kwenye silabasi na madai ya walimu. Mwakilishi mmoja wa wakuza mitalaa katika Taasisi ya Elimu Kenya (K.I.E.) alipohojiwa na mtafiti alisema kuwa zilikuweko sababu kadhaa za kufunza Isimujamii katika shule za sekondari. Sababu ya kwanza na inayoingiliana na misingi ya nadharia ya L2 na Isimujamii ni kuwa ni lazima wanafunzi waweze kutumia lugha kimuktadha. Mtafiti alipotaka kujua zaidi kuhusu jambo hili na uhusiano wa muktadha na sajili zinazopendekezwa kufundishwa katika silabasi, mtafitiwa alisema kuwa walimu wanaodai hawajui yaliyomo ya kufunzwa na jinsi ya kuyafunza, ni lazima wahakikishe kuwa muktadha hupewa nafasi muhimu katika ufundishaji. Kwa hivyo, wanapofundisha miundo fulani ya kisarufi waiweke katika muktadha wa mawasiliano kama vile katika sentensi na makala. Katika hali hii basi, chochote wanachofundisha katika lugha kilenge kuinua ujuzi wa kuwasiliana wa wanafunzi.

Pili, Isimujamii ilitazamiwa kuwa, katika ufunzaji wake, maswala ibuka kama vile Ukimwi, jinsia, maadili, utandawazi na teknolojia ya habari na mawasiliano yataeleweka kwa uwazi. Hii ni kwa sababu sarufi ya lugha hata ingawa ni muhimu haitasisitizwa na wanafunzi watavutiwa na kuelewa maswala haya kwa uwazi na bila kikwazo cha lugha.

Kuhusu matumizi ya silabasi yenye mtalaa wa Isimujamii, afisa huyu alisema kuwa, walimu ndio huchangia shida za utekelezaji. Walimu wasitegemee yaliyomo yaodheshwe kwa njia ambayo wakifungua ukurasa wa silabasi wataanza kufundisha moja kwa moja. La. Udhaifu unaojitokeza kwao ni kuwa, hawawezi kusoma malengo ya kijumla yaliyotajwa kabla ya yaliyomo kutajwa ya kila kidato katika stadi za kusikiliza na kuzungumza. Afisa huyu alinukuu lengo la kwanza la kidato cha tatu linalosema hivi.

> **Kustawisha mawasiliano kwa lugha fasaha kutegemea muktadha, mahusiano na mahitaji (Uk. 41).**

Mwalimu anastahili kusoma na kuelewa lengo hili. Licha ya silabasi hii kutoorodhesha yaliyomo ya kufunza ya Isimujamii, ajue ni sajili zipi atafunza ili atimize lengo hili kwa wanafunzi. Ili kuafikia lengo hili, hatakuwa na budi kuongozwa na misingi ya nadharia za lugha ya mawasiliano na Isimujamii iliyotajwa katika utafiti huu. Kwa mfano, ikiwa atachagua sajili ya mahakamani, mwalimu anaweza kuchagua mbinu zinazopendekezwa na mhimili wa nadharia ya mawasiliano kama vile uigizaji na michezo ya lugha. Wanafunzi katika darasa hili wanaweza

kuigiza yanayotendeka mahakamani na kazi ya mwalimu itakuwa kuwaelezea maana ya maneno au miundo ya mahakamani na mwishowe wataelewa na kutumia misamiati inayotumika mahakamani bila kikwazo. Haya pia ni kwa mujibu wa mhimili wa nadharia ya lugha ya mawasiliano kuwa maana ya miundo husisitizwa kwani lengo kubwa la nadharia hii ni mawasiliano.

Ilidhihirika kuwa, baadhi ya walimu huzembea kazini zao. Ithibati kulingana na afisa huyu ni kuwa, wao hununua ratiba za kazi ambazo zimeandaliwa na watu wengine wanaozitayarisha na ambao si walimu. Kutokana na jambo hili, walimu husumbuka kupata mawanda ya kushughulikia au pengine hushughulikia mawanda tofauti kabisa na yanayopendekezwa na K.I.E. Shutuma zilielekezwa kwa Tume ya Kuwaajiri Walimu (T.S.C.) ambayo miaka michache iliyopita ilitoa marupurupu kwa walimu wa lugha na sayansi. Waalimu ambao hawakuwa wapenzi na wasiokuwa na motisha kwa lugha wakajiunga na idara za lugha katika vyuo vya walimu kwa kutarajia kuwa baada ya kuajiriwa mshahara wao utakuwa juu. Walimu hawa baada ya kuajiriwa ndio wanaotoa shutuma kwa wakuza mitalaa kuwa hawawaongozi vyema katika utekelezaji wa mitalaa. Kwa hivyo, afisa huyu alipendekeza Wizara ya Elimu Kenya (M.O.E.) ishirikishe pia walimu katika utendaji wa kandarasi (performance Contract) ili wahakikishie serikali kuwa watafanya kazi na utendaji wa wanafunzi uimarike.

## 4.4 UBORA NA UDHAIFU WA MTALAA WA ISIMUJAMII

Watafitiwa wote walisema kuwa wameupitia mtaala wa Isimujamii ulionenakiliwa katika silabasi. Kuhusu ubora wake, 70% ilionelea kuwa mtalaa huu ni mzuri. Wahojiwa hawa waliulizwa kutaja vipengele mahsusi vinavyobainisha uzuri wa mtalaa huu na wakataja ufundishaji wa sifa za matumizi ya lugha katika miktadha mbalimbali na mada mpya kama Sheng' na lahaja. Walimu hawa walisema kuwa wanaomba Isimujamii ifunzwe kivyake kama vile fasihi inavyofunzwa ili waweze kufundisha vipengele vyake vizuri. Ujumuishaji wa vipengele hivyo unatatiza utekelezaji na asilimia 10 ya walimu huvikwepa kabisa.

Aidha, wahojiwa walipoulizwa kuelezea uzuri wa mtalaa huu kwa ujumla kwa wanafunzi, maelezo yao yaliingiliana na msingi wa ufundishaji wa lugha ya mawasiliano. Asilimia tisini (90%) ilisema kuwa licha ya mwanafunzi kufunzwa muundo wa maumbo ya lugha na kuwa na umilisi wa mawasiliano, ni lazima aweze kuitumia lugha hiyo vilivyo na kuwa na uamilifu wa mawasiliano. Kwa hivyo, Isimujamii itamfanya mwanafunzi aweze kueleza maana ya miundo na msisitizo kuwekwa kwa miundo hiyo kwani lengo la ufunzaji huu ni mawasiliano. Mwishowe wanafunzi hawa wataweza kuingiliana na jamii (Taz. Hymes, 1972; Trudgil, 1974; Edwards, 1979; Fasold, 1984). Kulingana na Momanyi (2001) katika Masinde (2007), wataalamu hawa walibainisha kuwa mbali na kule kuelewa utaratibu wa sauti na mpangilio wa maneno, nadharia ya isimu haina budi kuzingatia uhusiano kati ya sauti hizo za lugha na maana zipatikanazo. Hii ni kulingana na miktadha mbalimbali

ya kijamii. Kutokana na haya basi, Isimujamii kama taaluma inayohusika na mahusiano kati ya lugha na jamii, inaweza kutumiwa kurekebisha adabu na sheria za mawasiliano miongoni mwa waneni wa lugha ya Kiswahili. Walimu hawa walikubaliana na kauli hii na kuongezea kuwa sarufi wanayoifunza wanafunzi inapewa nguvu zaidi na taaluma hii ya Isimujamii: Wanafunzi wanafanywa waitumie lugha ya Kiswahili katika miktadha halisi ya mawasiliano.

Ili kufikia malengo yao darasani, asilimia 70 ilikiri kuwa inahakikisha kuwa kuna matumizi mengi darasani ya lugha kwani ufunzaji wa lugha ya mawasiliano unasisitiza kuwa mtu hujifunza lugha vizuri kwa kuitumia. Katika sura ya kwanza, mtafiti alisema kuwa, ili mwanafunzi awe na ujuzi wa kuwasiliana, ni heri kuwe na kuwasiliana kwingi kati ya mwalimu na wanafunzi na pia wanafunzi wenyewe. Ili jambo hili lifanikiwe, mwalimu anaweza akatumia mbinu za ufundishaji wa lugha ya pili kama vile **michezo ya lugha**, **michezo ya kuigiza** na **majadiliano** mengi katika darasa. Watafitiwa walipohojiwa kuhusu jambo hili, 80% ilisema inazitumia lakini muda hautoshi kwa sababu ya upana wa somo la Kiswahili. Mwalimu mmoja alikiri kuwa yeye hutumia mbinu hizo na akatolea mfano wa kipengele cha **sajili ya Mahakamani** na kusema yafuatayo:

> **… sajili ya mahakamani ndiyo iliyowasisimua wanafunzi wangu mno mpaka ikanibidi niwaandalie ziara mahakamani ili wajionee shughuli hiyo. Tulipofika, wanafunzi walijionea wenyewe jinsi kesi inavyokatwa. Baada ya kesi tatu kufanywa wanafunzi waliruhusiwa na hakimu kuigiza mumo humo mahakamani. Walipokuwa wanaigiza, hakimu na wasaidizi wengine waliwakosoa na mwishowe wanafunzi wakamakinika na sajili ya mahakamani. Mpaka sasa wanakumbuka yote yanayotendeka tangu hakimu aingie mpaka mwisho wa kesi.**

Mhojiwa alipoulizwa na mtafiti kama kuwatembeza wanafunzi mahakamani pekee kunatosha kutimiza malengo yake, alisisitiza kuwa ziara hiyo ilitosha. Alipoulizwa kwa nini, alisema kuwa katika ufundishaji wa lugha ya mawasiliano, muktadha hupewa nafasi muhimu. Kwa hivyo wanafunzi waliweza kujua maneno na miundo fulani ya kisarufi ambayo inatumika mahakamani. Waling'amua kuwa maneno kama hayo hayawezi kutumiwa na mtu wa kawaida. Kutokana na jambo kama hilo, wanafunzi wataweza kuelezea sifa za lugha ya maabadini, hotelini, n.k. na kujua kuwa matumizi ya lugha hufungamana na hali mbalimbali katika jamii. Kwa njia hii, mwanafunzi anahimizwa kutumia lugha kulingana na hali hizi na kuzingatia kaida za kijamii zinazotawala matumizi ya lugha. Mathalan, mwanafunzi atang'amua kuwa lugha anayoitumia kwa hirimu wake ni tofauti na ile atakayotumia kwa wakubwa wake.

Jambo jingine lililojitokeza kupitia mahojiano zaidi ni kuwa baadhi ya walimu hutumia **drili** katika ufundishaji wao wa vipengele vya lugha. Hata ingawa wengine walikiri kuwa wanaandaa mijadala darasani ili kufundisha misamiati ya bungeni, hawana uhakika iwapo hujumuisha Isimujamii. Walimwambia mtafiti kuwa, katika kufundisha sajili kama hiyo ya bungeni na sajili zingine kama za kidini, hotelini na mwajiriwa na mwajiri wao hutumia drili. Ilibainika kuwa katika matumizi ya drili, mwalimu humdhibiti mwanafunzi katika matumizi ya sajili fulani hadi atakavyoitumia inavyotakikana. Baadaye mwanafunzi ataweza kuitumia lugha kutegemea muktadha na atakuwa na nidhamu katika mawasiliano. Mengi ya matatizo

yanayowakumba wanafunzi wa shule, vyuo vya ualimu na hata vyuo vikuu hayatokani na kile Chomsky (1962) alichokiita uwezo na utendaji bali Hymes (1967) alichokiita ustadi au umahiri katika mawasiliano. Uamilifu huu humwezesha mtu kujua ni wakati gani anyamaze, atumie lugha gani, lini, wapi, na kwa nini. Mara nyingi tunaona wanafunzi wetu wakishindwa kutumia miktadha mwafaka hususan pale wanapoongea na wakubwa zao. Upungufu huo huweza kujitokeza katika salamu za kawaida ambapo utaweza kumsikia mwanafunzi akikusabahi, "Mwalimu sasa?" au "Mwalimu mambo" au "Habari mwalimu, vipi mambo?" na kadhalika. Katika muktadha wa adabu za lugha, salamu hizi zinaashiria utovu wa nidhamu. Ni salamu zisizotambua kigezo cha umri au hadhi ya mtu. Kwa hivyo, kupitia drili na mazoezi mengi ya lugha kutegemea muktadha, mwanafunzi atakuwa na nidhamu katika mawasiliano.

Licha ya mtalaa huu mpya wa Isimujamii kuwa na uzuri na umuhimu kwa wanafunzi, walimu wote walieleza kuwa una udhaifu unaotatiza utekelezaji. Udhaifu waliotaja wahojiwa ulichanganuliwa na kuorodheshwa kutegemea uzito kama inavyoonekana katika jedwali 3 hapa chini.

**Jedwali 9: Udhaifu wa mtalaa kutegemea uzito**

| | Udhaifu | Walimu | % |
|---|---|---|---|
| (a) | Ukosefu wa vitabu na miongozo ya kufunzia. Pia mada kutoratibishwa vizuri kwa njia zitakavyofunzwa na mwalimu. | 9 | 90 |
| (b) | Mada ngumu na ambazo walimu hawazijui kama vile lahaja, ulumbi, msimbo, n.k. | 8 | 80 |
| (c) | Mrundiko wa vipengele na upana wa somo. Vipengele ni vingi na licha ya hayo somo lenyewe ni pana. Wanahitajika kusoma lugha, fasihi insha. Muda hautoshi. | 7 | 70 |
| (d) | Ugumu wa kutekeleza mwelekeo mseto. Kujumuisha Isimujamii katika ufunzaji wa lugha si jambo jepesi. | 5 | 50 |
| (e) | Tofauti kati ya KIE na KNEC. KIE wanasema vipengele fulani visifunzwe lakini KNEC inaishia kuvitahini. | 2 | 20 |

Kupitia mahojiano ya ana kwa ana na wahojiwa, wengi wao walisema hawajui lengo la Wizara ya Elimu kuanzisha Isimujamii – ni kama kwamba walichukulia Isimujamii ni mada inayoweza kufunzwa kwa wiki moja. Walimu 80% walidai kuwa baadhi ya mafunzo yalilenga kiwango cha Chuo Kikuu. Walimu hawa walieleza kuwa mada ngumu huwatisha wanafunzi na kuwafanya wachukie somo la Kiswahili. Walidai kuwa jambo hili linafanya utendaji wao ushuke. Ingawa utafiti huu haukudhamiria kutafitia utendaji wa wanafunzi, walimu wote walimtolea mtafiti ithibati ya kutosha. Walimu walimwonyesha mtafiti matokeo ya mtihani wa kidato cha tatu wa lugha ya

Kiswahili wa 2008 walioufanya wakitahini Isimujamii na wa 2007 wakiwa kidato cha pili bila kutahini Isimujamii Wilayani Thika. Mlinganisho wa alama walizopata wanafunzi mwisho wa mwaka 2007 katika kidato cha pili na muhula wa kwanza 2008 katika kidato cha tatu ulielekea kuunga mkono maoni ya walimu kuhusu kushuka kwa utendaji wa wanafunzi kama inavyoonekana katika jedwali 4 hapa chini.

**Jedwali 10: Mlinganisho wa Utendaji wa Wanafunzi**

| **Shule** | **Muhula III Kidato II Mwaka 2007 (%)** | **Muhula I Kidato III Mwaka 2008 (%)** | **Tofauti** |
|---|---|---|---|
| A | 74 | 30 | -44 |
| B | 77 | 66 | -7 |
| C | 56 | 48 | -8 |
| D | 39 | 42 | +3 |
| E | 81 | 73 | -8 |
| F | 80 | 79 | -1 |
| G | 46 | 51 | +5 |
| H | 73 | 37 | -36 |
| I | 72 | 76 | +4 |
| J | 66 | 79 | +13 |
| Wastani | 66.4 | 58.1 | -8.3 |

**Maelezo**: Shule **A** na **B** - Taifa
Shele **C** na **D** - Mkoa
Shule **E** na **F** - Wilaya
Shule **G** na **H** - Kutwa
Shule **I** na **J** - Binafsi

Japo matokeo haya yanaonyesha kushuka kwa wanafunzi katika somo, huenda yalisababishwa na mrundiko wa kazi nyingi kwa wanafunzi ikichukuliwa kuwa ni wakati huo walianza kushughulikia masomo mengine kama vile fasihi.

Hata hivyo, washikadau wanafaa wakague matokeo kama haya na wachukue tahadhari mapema ili athari mbaya zisitokee kwa wanafunzi.

## 4.5 MAPENDEKEZO YA WALIMU KUHUSU UBORESHAJI WA MTALAA WA ISIMUJAMII WA SHULE ZA UPILI NCHINI KENYA

Uchambuzi wa taarifa za utafiti zilizokusanywa umefichua kuwa walimu wana mapendekezo yaliyo sawa kuhusu uboreshaji wa utekelezaji wa mtalaa wa Isimujamii. Kupitia mahojiano ya ana kwa ana na mtafiti, asilimia 100 ya walimu ilikuwa na mapendekezo yafuatayo kwa Wizara ya Elimu na washikadau wengine wanaochangia elimu kwa wanafunzi.

### 4.5.1 Baraza la Mitihani nchini (KNEC)

Walimu walikuwa na maoni kuwa, ikiwa mwanafunzi anatarajiwa kiwango chake cha mawasiliano kiinuke baada ya miaka minne, basi mtindo wa utahini kwa wanafunzi lazima ubadilishwe. Hii ni changamoto katika utahini wa Kiswahili nchini. Kwanza kulingana na watafitiwa hawa, utahini wa kitaifa hapa nchini ni wa kijumla mno (summative). Si rahisi mtihani wa masaa mawili kwa mfano kupima ikiwa mtahiniwa ameyamudu mambo yote katika kujifunza lugha fulani. Uchunguzi uliofanywa na

mtafiti ulidhihirisha kuwa, swali la Isimujamii ni moja tu na huwa ni la nne linalobeba alama kumi. Malengo ya ufundishaji wa lugha ya mawasiliano ni kumwezesha mwanafunzi asiwe na vikwazo anapowasiliana kwa L2 aliyojifunza. Katika mtihani huo hakuna utahini wa mawasiliano au matamshi kwa mfano. Kwa hivyo, mwanafunzi wakati huu anapokuwa akijifunza Kiswahili atakuwa akikizungumza atakavyo, bora aweze kuyajibu maswali ya mtihani kwa maandishi. Ikiwa **maarifa tekelezi** na **maarifa hisi** yangetahiniwa, basi malengo yote ya kitaifa ya somo la Kiswahili yangetimizika bila matatizo yoyote.

Baraza la Mitihani nchini (KNEC) kwa sasa halitathmini mambo yaliyo nje ya **maarifa tambuzi** katika Kiswahili ambacho kina watahiniwa wengi kabisa (KCSE na KCPE) na hii ni changamoto kwao. Jambo lililomshangaza mtafiti ni kuwa walimu 90% walikiri ni wao wanaochangia kuteleza huku kwa KNEC. Walipoulizwa kwa nini hawaishinikizi KNEC kutahini ustadi wa wanafunzi kimaongezi (oral skills) walitolea mfano wa mtihani wa Kiingereza ambao walimu walipinga mtihani wa stadi simulizi. Walimu walisema kuwa KNEC haina uwezo wa kufika kote nchini kutahini kila mwanafunzi lakini ilibainika kuwa wenyewe hawakujiona kama chombo ambacho KNEC ingetumia kuwatahini wanafunzi katika stadi hizi (Taz. Njogu, 2007). Ikiwa utahini huu ungekuzwa, KNEC wakishirikiana na walimu wangetahini Isimujamii katika mtihani wa Kiswahili kwa kutumia stadi simulizi ili waone uwezo wa wanafunzi wa kujieleza na kuwasiliana kwa L2 badala ya kutumia mtindo wa utahini kwa njia ya majibu kimaandishi.

Watafitiwa walitoa changamoto nyingine kwa KNEC. Walisema kuwa, mitihani nchini Kenya imekuwa ni chombo cha kujiendeleza kimasomo, kikazi na kadhalika. Hivyo basi kuna ushindani mkubwa wa kila mtahiniwa kutaka kujipatia alama nyingi ili awe mbele katika ushindani huu. Mwanafunzi wa L2 ataishia kujifunza na kuimundu miundo ya lugha bila kuzingatia uamilifu wa lugha ili aweze kupita mtihani na kuendelea na masomo. Si ajabu kupata wanafunzi katika vyuo vikuu walio na shida za kimawasiliano kwa kutumia L2 lakini wawa hawa walipata alama ya wastani **A** katika mitihani yao. Ni katika hali hii ambapo malengo na makusudi ya ufundishaji wa Isimujamii katika lugha ya Kiswahili yanapotea. Katika mkabala huu basi, walimu walikuwa na maoni kuwa, mtazamo wa KNEC kuhusu utahini unafaa ubadilishwe kabisa. Maofisa wa KNEC na KIE wanafaa kupewa mafunzo maalum kuhusu utahini na ufundishaji wa Isimujamii na haya mawili yafungamanishwe na maendeleo ya teknolojia. Walipendekeza kwamba pawe na utahini wa kimaongezi katika somo hili katika kidato cha nne. Ukosefu wa muda usiwe ni kisingizio cha kutoanzisha utahini huu. Mtazamo wa lugha ya mawasiliano kuwa, muktadha hupewa nafasi muhimu katika ufundishaji umekosa maana basi. Utahini wa kimaongezi utadhihirisha uelewa wa wanafunzi wa kutumia lugha kulingana na muktadha.

### 4.5.2 Ualimu na Vyuo vya Walimu Nchini

Asilimia 100 ya walimu ilikuwa na maoni kuwa ingekuwa manufaa kwa wanafunzi ikiwa walimu hawa wangepewa kozi za muda za kuwapiga msasa kuhusu ufundishaji

wa Isimujamii. Walitoa maoni haya kwa KIE iwe inaandaa kozi hizi wakati wa likizo ambapo watakuwa wakihudhuria katika vyuo vikuu na Vyuo vya walimu. Kozi hizo zitawafaa kwa kuwawezesha kufunza vizuri, kutumia vifaa na zana za kufunzia na jinsi ya kutahini Isimujamii kwa lengo la kuinua kiwango cha mawasiliano cha wanafunzi.

Mapendekezo mengine yalihusu utayarishaji wa walimu vyuoni. Kiswahili kinafundishwa katika vyuo vikuu na pia katika vyuo vya walimu wa diploma. Katika ufundishaji na utahini wa lugha ya Kiswahili, walimu walikuwa na maoni kuwa wahadhiri wanafaa kukabiliana na changamoto kadhaa. Kwanza, wanafunzi kuwa walimu wa lugha ni lazima waweze kufundisha lugha ya mawasiliano. Wengine wanatoka vyuoni bila ustadi unaofaa wa lugha hii. Upungufu mkuu uliopo katika ufundishaji na utahini unahusu taaluma ya Fonetiki. Ufundishaji na utahini wa taaluma hii hauhusishi hali ambapo wanafunzi wanaweza kutahiniwa kimaongezi kwa kupewa fursa ya kutofautisha vitamkwa mbalimbali kwa kuvitamka. Hili likitekelezwa, laweza kuongeza uelewa na ujuzi wa wanafunzi katika taaluma ya Fonetiki na watakapoenda kufundisha, wataweza kukabiliana na shida za wanafunzi za kimawasiliano zinazoletwa na athari za L1. Watawasaidia wanafunzi kuwa na ustadi wa mawasiliano na hivyo kuendeleza na kulipa nguvu somo la Isimujamii katika shule za sekondari. Walipoulizwa kama matumizi ya drili yangesaidia jambo hili, 80% waliunga mkono mbinu hii lakini 20% wakasema mbinu hii huwachosha na

wanafunzi huchukia ufunzaji huu. Asilimia hii 20% ilidai kuwa drili huwa mwafaka kwa watoto wa shule za chekechea ambao wako tayari kufunzwa lugha yoyote ile.

Asilimia 100 ya walimu ilitoa mapendekezo kwa Wizara ya Elimu wakishirikiana na vyuo vya ualimu kuhusu utahini wa ufundishaji wa Kiswhaili nyanjani (Teaching Practice). Wao wenyewe walipokuwa nyanjani walipotahiniwa, walishuhudia hali hii ambayo haikuwapendeza na ambayo haiwezi kuinua kiwango cha ufundishaji wa Isimujamii. Mazoezi ya Ufundishaji (Teaching Practice) yanahusu wanafunzi wanaopata mafunzo ili baadaye wafundishe Isimujamii. Tatizo hili linalotokana na hali kwamba wakati wa mafunzo ya nyanjani, asilimia kubwa ya watahini ambao hutumwa na vyuo kutathmini ufundishaji nyanjani hawana ujuzi wowote katika somo hili na namna linavyopaswa kufundishwa. Wanapofundisha vipengele kama mazungumzo vinavyofaa kuwashirikisha wanafunzi, hawawaelekezi watahiniwa hawa vilivyo. Kwa hivyo, mwalimu kama huyo baada ya kufuzu na kuajiriwa kufundisha, huwa hajamakinika vizuri katika ufundishaji. Kosa si la mwalimu huyu lakini ni la watahini ambao wanawahitimisha walimu ambao hawana ujuzi wa kutosha katika ufundishaji wa Isimujamii.

Walimu walielezea shida nyingine kuhusu ufundishaji wa kozi ya Kiswahili katika vyuo vikuu inayotinga utekelezaji mzuri wa mtaala wa Isimujamii. Vyuo vikuu vinawalazimisha kuchukua somo la Kiswahili pamoja na somo lingine katika shahada ya kwanza. Maoni ya walimu 80% yalikuwa kuwa, wanaishia kuwa na kazi nyingi za



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

kusoma katika masomo yote mawili na kwa hivyo vipengele muhimu vya Kiswahili kama Isimujamii havishughulikiwi vinavyostahiliwa. Wanafunzi wanaochukua somo la Kiingereza husoma Kiingereza na fasihi na kwa hivyo wanabahatika kuchambua taaluma zote mbili jambo linalowasaidia ufundishaji wao katika shule za upili. Isitoshe, wanapoanza kufundisha, walimu hawa wa Kiswahili wanalazimishwa na wakuu kufundisha somo la pili na wanapolalamika wanaambiwa walilisomea vyuoni. Lakini katika wakati huu, mtafiti aling'amua kwamba wanafunzi wote wanaosomea lugha ya Kiingereza au Kiswahili wanastahili kuchukua somo la pili kulingana na barua kutoka Tume ya Kuwaajiri Walimu (T.S.C.). Utafiti zaidi kuhusu jambo hili unafaa kufanywa ili msimamo utakaofaidi ufundishaji wa lugha kudhibitiwa ili malengo ya elimu yafanikiwe. Maoni zaidi ya asilimia 50 ya walimu yalidhihirisha kuwa wangetaka somo la Kiswahili litenganishwe na Fasihi. Jambo hili litawezekana ikiwa vyuo vikuu vitaanza kufunza Fasihi ya Kiswahili kama taaluma kivyake na isimu ya Kiswahli kivyake. Walimu walidai kuwa somo la Kiswahili ni pana na upana huu unafanya vipengele kama Isimujamii visishughulikiwe vilivyo.

Mwisho, asilimia 70 ya walimu ilisisitiza kuwa mwalimu anapohitimu kufunza, kabla hajaanza kutekeleza kazi yake apewe mawaidha kwa kuandaliwa warsha na KIE. Umuhimu wa warsha hii utakuwa ni kumhimiza kufundisha lugha akilenga mawasiliano lakini siyo kufunza ili mwanafunzi apite mitihani. Ni vyema ikiwa atapewa funzo la jinsi atakuwa akitathmini utendaji wa wanafunzi wa mawasiliano katika hatua mbalimbali za ufunzaji wake. Bila shaka mwalimu kama huyo atakuwa

mmoja wa wale watatimiza malengo ya ufundishaji wa Isimujamii katika shule za upili nchini Kenya.

### 4.5.3 Wazazi

Utafiti huu pia ulifichua kupitia walimu kuwa, wazazi wana jukumu kubwa katika kufaulisha mtalaa huu wa Isimujamii kutokana na maoni ya walimu.

Asilimia 90 ya walimu ilisema kuwa wazazi wanaweza kuinua ujuzi wa wanafunzi wa kuwasiliana kwa kuchangia ifuatavyo:

- Kuwahimiza wasikilize vipindi vya televisheni na radio na kuchangia katika majadiliano hayo wakati wa mapumziko. Jambo hili linaungwa mkono na mhimili wa nadharia ya ufundishaji wa lugha ya mawasiliano: muktadha hupewa nafasi muhimu katika ufunzaji na ujifunzaji ambapo miundo fulani ya kisarufi huwekwa katika muktadha wa mawasiliano.
- Kuwanunulia gazeti na makala mengine yatakayosaidia kuinua ujuzi wao wa lugha.
- Kuwahimiza wahadithiane jioni au wakati wowote mwafaka.
- Matumizi ya Kiswahili nyumbani.
- Matumizi ya Kiswahili nyumbani kama lugha ya kwanza.
- Kuwapa motisha wa kujadiliana yale waliyojifunza shuleni kuhusu lugha ya Kiswahili.

#### 4.5.4 Kamati ya Chama cha Wazazi

Asilimia 90 ya walimu vile vile ilipendekeza kuwa kamati ya chama hiki ihakikishe kuwa imekusanya pesa za kununua vitabu na zana za kufundishia Isimujamii katika shule za sekondari. Tarakilishi na ujuzi wa mtandao huwa ni mradi unaogharimu pesa nyingi lakini kwa ushirikiano wao na wakuu wa shule, watapata njia na uwezo wa kuzinunua. Vifaa hivi huweza kuchangia ufundishaji wa Kiswahili kama lugha ya mawasiliano.

#### 4.5.5 Udhibiti wa Ubora wa Elimu

Asilimia 100 ya walimu ilikuwa na hisia kwamba Idara ya Kudhibiti Ubora wa Elimu (Quality Assurance) ni muhimu katika utekelezaji wa mtalaa wa Isimujamii. Maofisa kutoka idara hii wanapokuja kuwakagua jinsi wanavyotekeza mtalaa huu, wengi wao hawajamakinika na taaluma ya Isimujamii na ufundishaji wake. Kwa hivyo, wakaguzi hawa wanastahili kuandaliwa semina za kuwapiga msasa kuhusu jinsi ya kutekeleza mtalaa huu mpya. Wanastahili kumakinika na kuzingatia mapendekezo ya nadharia na taratibu za kitaaluma katika utendakazi wao. Jambo hili likitekelezwa maofisa hawa watatumia ujuzi huo kuwalainisha walimu kufundisha somo hili.

### 4.6 MUHTASARI

Maoni ya walimu na afisa wa elimu kutoka K.I.E. kuhusu yaliyomo yanayoshughulikiwa na mtalaa wa Isimujamii wa shule za upili nchini Kenya yamechanganuliwa katika sura hii. Uchanganuzi huu umehusishwa na mihimili ya

nadharia ya lugha ya mawasiliano na Isimujamii. Imebainika kuwa licha ya wanafunzi kuwa na uelewa wa miundo ya lugha, wanapaswa kuwa na uamilifu wa mawasiliano. Jambo hili humaanisha kuwa ni lazima mwanafunzi ajue kuitumia vilivyo lugha aliyojifunza. Mwanafunzi ataweza kuitumia lugha katika miktadha mbalimbali. Kutokana na haya basi, Isimujamii kama taaluma inayohusika na mahusiano kati ya lugha na jamii, inaweza kutumiwa kurekebisha adabu na sheria za mawasiliano miongoni mwa wanafunzi wa lugha ya Kiswahili. Ili kutimiza lengo lake, na kwa kulingana na misingi ya nadharia ya lugha ya mawasiliano, mwalimu anayeshughulikia ufundishaji wa L2 darasani lazima awashirikishe wanafunzi katika ufundishaji. Kwa hivyo, ukaririshaji wa mawasiliano hautaepukika katika darasa kama hilo. Itamlazimu mwalimu kuzua mijadala na michezo ya kuigiza darasani. Ikiwa mwanafunzi atamakinika katika matumizi haya ya lugha kulingana na miktadha mbalimbali, bila shaka atakuwa na nidhamu katika mawasiliano milele.

Utafiti huu umeonyesha kuwa, utekelezaji wa mtalaa mpya wa Isimujamii unatingwa na matatizo kadhaa. Silabasi iliyotolewa na wakuza mitalaa ili kuwaongoza na kuwaelekeza walimu haitimizi lengo hili. Vipengele vinavyofaa kushughulikiwa na walimu havijaratibiwa kwa njia itakayowafanya wafundishe kimantiki. Licha ya hayo, inawawia vigumu kuandika ratiba ya kazi wakitumia mwongozo wa silabasi hiyo.

Tofauti na imani kuwa walimu hawashughulikii somo hili la Isimujamii na wana mielekeo hasi katika kulifundisha, utafiti huu umebainisha kuwa kauli hii si kweli. Hii ni kwa sababu, kupitia mahojiano na walimu, mtafiti aligundua kuwa walimu wengi wanaliratibu katika ratiba ya kazi ya somo. Zaidi ya hayo, kwa sababu walimu 90% wanalifundisha, wameweza kuonyesha baadhi ya matatizo yanayolikumba na ambayo yakiondolewa ufundishaji wake utakuwa kama wa somo lolote. Kwa hivyo, utafiti ulitarajia kuwa somo hili halifunzwi na walimu wengi lakini ukweli ni kuwa baadhi ya walimu wanatenda kazi yao hasa ya ufundishaji wa Isimujamii vizuri.

Utafiti zaidi nyanjani na afisa wa mitalaa kutoka K.I.E. umeonyesha kuwa, madai ya walimu yanadhihirisha udhaifu wao katika kutekeleza mtalaa huu wa Isimujamii. Malengo katika silabasi ni kiwakilishi tosha cha yaliyomo yanayostahili kufunzwa. Malengo haya kwa kupewa nguvu na mihimili ya nadharia za lugha ya mawasiliano na Isimujamii ambayo imesisitizwa na utafiti huu, yanafaa yawe malighafi ya yaliyomo ambayo yatapatikana kutoka kwa orodha ya sajili mbalimbali zilizotajwa.

Aidha, walimu walikubali kuwa, mtalaa huu una uzuri na udhaifu wake. Kuhusu ubora wa mtalaa huu, wengi walikiri kuwa somo la Isimujamii linampa mwanafunzi ujuzi wa lugha. Mwanafunzi anaweza kung'amua uamilifu wa lugha licha ya kufundishwa sarufi. Anaweza kuiweka lugha katika matumizi. Hata hivyo walimu walielezea woga wao kuhusu mtalaa huu. Baadhi ya mambo waliyotaja yanayotinga somo hili ni kama vile mrundiko wa vipengele katika kila kidato na kutoratibishwa

kwa vipengele mahsusi vitakavyofunzwa katika darasa mahsusi miongoni mwa mengine. Wahojiwa walisema ikiwa tahadhari haitachukuliwa, utendaji wa wanafunzi katika somo la Kiswahili huenda ushuke na lawama itakuwa kwa walimu lakini si kwa wakuza mitalaa.

Bila kupata mapendekezo ya walimu kuhusu uboreshaji wa mtalaa wa Isimujamii katika kiwango hicho, utafiti huu haungekamilika. Kupitia kwao, imebainika kuwa KNEC inajukumu kubwa katika kuona kuwa lengo la ufundishaji wa Isimujamii linatimizwa. Imebainika kuwa, mtindo wa utahini wa KNEC lazima ubadilishwe kwa vile unaelekea kuwahimiza wanafunzi kupita mitihani badala ya kukuza uwezo wa mwanafunzi wa kuwasiliana kwa kutumia lugha aliyojifunza shuleni. Katika uchanganuzi wa data, imedhihirika kupitia msingi wa nadharia ya lugha ya mawasiliano kuwa, vipashio muhimu si vya kisarufi lakini ni vile vinavyosisitiza mawasiliano. Baadhi yao huwa na matokeo mema katika somo la Kiswahili, lakini hawawezi kabisa, au hawawezi kujieleza vyema kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Jambo hili hukwamiza udumishaji wa uhusiano mwema katika jamii. Hii ni kwa sababu imethibitika kupitia nadharia ya Isimujamii kuwa, ujifunzaji lugha unahusu jamii na mtu anayejifunza (Hymes, 1971). Kutokana na hali hii, walimu wengi walikuwa na maoni kwamba pawe na utahini wa kimaongezi katika somo hili katika kiwango hiki. Lakini taasisi kama vile KIE, KNEC na walimu hawatoshi kuboresha mtalaa huu wa Isimujamii. Maoni ya walimu yameonyesha kuwa wazazi huwa na mchango pia katika kukuza uwezo wa mawasiliano kwa mwanafunzi.

Wanapendekezewa wawatie motisha wanafunzi kutumia lugha kwa kuzua mijadala mingi nyumbani kwa lugha hii na wawanunulie vitabu na magazeti nyumbani. Vyama vya wazazi shuleni vitachangia kwa kuanzisha miradi kama vile ujengaji wa maktaba na ununuzi wa vitabu shuleni. Mambo haya yataweza kuinua kiwango cha somo la Isimujamii na utekelezaji wake utakuwa rahisi kwa walimu na washikadau wengine. Muhtasari na matokeo ya utafiti yametolewa katika sura inayofuatia.

# SURA YA TANO

## MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 5.0 UTANGULIZI

Sura hii imetoa muhtasari wa yaliyoshughulikiwa katika utafiti huu. Matokeo na hitimisho la utafiti huu pia ni mambo mengine ambayo yameangaziwa katika sura hii kulingana na malengo ya utafiti yaliyotolewa. Mapendekezo pia yametolewa yanayonuia kuboresha ufundishaji wa Isimujamii katika shule za upili.

### 5.1 MUHTASARI

Dhamira ya utafiti huu ilikuwa ni kufanyia tathmini mtalaa wa Isimujamii wa shule za upili nchini Kenya iliyoanza kufundishwa kwa mara ya kwanza mnamo mwaka 2003 na kutahiniwa kwa mara ya kwanza mwaka 2006 katika mtihani wa Kitaifa wa K.C.S.E. katika mfumo wa 8-4-4. Nia hasa ya kufanya tathmini hii ilikuwa ni kubainisha maoni ya walimu wa Kiswahili katika shule za sekondari kuhusu maudhui ya mtalaa mpya wa Isimujamii na uelewa wao kuhusu maandalizi ya mtalaa. Aidha, ili kufikia lengo hili, vipengele mbalimbali vinavyobainisha matumizi ya lugha katika miktadha mbalimbali kulingana na mtalaa wa Isimujamii na maoni ya walimu kuvihusu vilichanganuliwa. Kwa kifupi, utafiti huu ulikusudia kuchunguza changamoto zinazowakumba walimu wa Kiswahili katika harakati zao za kufunza Isimujamii.

Uchanganuzi huu ulifanywa kwa kufuata misingi ya Nadharia za Lugha ya Mawasiliano na Isimujamii ambapo imeonyeshwa kuwa katika ufundishaji huu, vipashio muhimu siyo vile vya kisarufi na kimuundo tu, lakini pia vile vya kimawasiliano. Pia, dhana ya muktadha ilikuwa ichunguzwe na kutathminiwa iwapo yaliyomo yanayopendekezwa kufunzwa yanaisisitiza kwa vile muktadha hupewa nafasi muhimu katika ufundishaji wa lugha ya mawasiliano. Zaidi ya hayo, uandalizi wa mitalaa pamoja na yaliyomo umechanganuliwa kwa kutumia msingi wa nadharia ya Isimujamii kwa kuiangalia Isimujamii kama kitengo cha isimu kinachoangalia matumizi ya lugha katika jamii, na jinsi miktadha ya kijamii inavyoathiri lugha. Ni kutokana na misingi ya nadharia hizi ambapo malengo ya kazi hii yameweza kuafikiwa.

Sura ya kwanza imetoa maelezo ya kijumla kuhusu kazi hii ambapo utangulizi wa utafiti, swala la utafiti, maswali yaliyoongoza utafiti huu, madhumuni na malengo ya utafiti yamejadiliwa. Malengo haya yalihusisha uchunguzi wa maoni ya walimu wa lugha na wataalamu wa mitalaa kwa misingi ya ufundishaji wa lugha ya mawasiliano na Isimujamii. Hali kadhalika, mna maelezo kuhusu yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti, misingi ya nadharia na mbinu za utafiti.

Sura ya pili imetoa ufafanuzi wa dhana ya mitalaa na uandalizi wake kwa kuzingatia somo la lugha. Fafanuzi mbalimbali kutoka kwa wataalamu wa mitalaa zimeangaziwa. Vigezo vinavyopima utendakazi wa mitalaa vimepitiwa na



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

kufafanuliwa. Vigezo hivi ni hatua za kuandaa mitalaa. Jumla ya hatua saba zimejadiliwa kulingana na wataalamu wa ukuzaji mitalaa na elimu. Hatua hizi zinaathiri kufaulu na utekelezaji wa mtaala mpya wa somo.

Sura ya tatu ni kimelea cha sura ya pili. Katika sura hii kama ilivyo katika sura ya tatu, kuna maelezo na mjadala wa maoni ya walimu kuhusu dhana ya mtalaa na maandalizi yake. Ili kuelewa sababu za udhaifu na matatizo katika utekelezaji wa mtalaa mpya wa Isimujamii katika shule za upili nchini Kenya, walimu walidadisiwa kuhusu uelewa wao katika kila hatua ya uandalizi wa mtalaa na maoni hayo kuchanganuliwa kwa njia ya mjadala. Maelezo ya wataalamu wa mtalaa pia yaliongezea data sura hii na kusukuma mbele utafiti.

Sura ya nne imehusu uwasilishaji wa data na mjadala ambapo maoni ya walimu na wataalamu wengine katika taaluma ya elimu kuhusu mawanda ya Isimujamii katika mtalaa mpya yamechanganuliwa. Yaliyomo kwenye silabasi (K.I.E. 2002) na mwongozo kwa walimu (K.I.E. 2006) kuhusu Isimujamii yamepitiwa na maoni ya walimu na wataalamu wengine katika elimu kuchunguzwa na kuchanganuliwa. Zaidi ya hayo, ubora na udhaifu wa mtalaa wa Isimujamii umechunguzwa na kuhakikiwa katika sura hii kwa kuhimiliwa na nadharia za ufundishaji wa lugha ya mawasiliano na Isimujamii. Mapendekezo juu ya uboreshaji wa mtalaa wa Isimujamii yamechanganuliwa katika sura hii. Aidha, sura ya tano inahusu muhtasari wa tasnifu, matokeo, hitimisho na mapendekezo yake.

## 5.2 MATOKEO NA HITIMISHO LA UTAFITI

Kwa kuongozwa na mihimili ya nadharia za ufundishaji wa lugha ya mawasiliano na Isimujamii, utafiti huu umebainisha mambo kadhaa kuhusu mtazamo wa walimu juu ya utekelezaji wa mtalaa wa Isimujamii wa shule za sekondari iliyojumuishwa katika somo la Kiswahili.

Imedhihirika kuwa, walimu wameipitia silabasi ambayo imeorodhesha yaliyomo ya mtalaa wa Kiswahili na ambayo wanastahili kudondoa vipengele vya Isimujamii na kuvijumuisha katika ufundishaji wao. Licha ya kutarajia kuwa walimu wangeongozwa na mhimili wa nadharia ya lugha ya mawasiliano unaosisitiza maana ya miundo kwa lengo la kustawisha mawasiliano kwa wanafunzi, 40% ya walimu ilikiri kuwa inafunza sajili mbalimbali ikiweka mkazo katika sarufi na kukosa kulenga kufunza Isimujamii ili kuinua ustadi wa wanafunzi wa kuwasiliana. Katika hali hii basi, tahadhania ya utafiti huu imepata mashiko kuwa mtaala wa Isimujamii katika shule za sekondari una udhaifu katika kumwongoza mwalimu.

Walimu wamekiri kuwa wanatumia silabasi kutayarisha ratiba ya somo la Kiswahili iliyojumuisha Isimujamii. Utafiti huu umeonyesha hofu yao kuhusu jambo hili na kuongezea udhaifu wa mtalaa huu. Wamesema silabasi ya mtalaa huu hailengi vipengele mahsusi vya Isimujamii. Kwa hivyo, katika kushughulikia lengo la Isimujamii kutokana na mihimili iliyotajwa ya Isimujamii, mwalimu anashindwa

kufundisha Isimujamii kama kitengo cha Isimu kinachoangalia matumizi ya lugha katika jamii na jinsi miktadha ya jamii inavyoathiri lugha (Fasold, 1984). Mwalimu asiyekuwa mbunifu hatashughulikia jambo hili na utafiti huu umegundua kuwa walimu wana matatizo ya kutayarisha somo la Isimujamii katika ratiba zao na kuifunza kwa mtazamo huu wa Isimujamii. Walimu wanaoratibu Isimujamii na kuijumuisha katika ufundishaji wao walikiri kuwa walihudhuria warsha za kitafifa muda mfupi tu baada ya mtalaa huu kuanzishwa. Kutokana na jambo hili, ithibati zaidi ya tahadhania ya utafiti huu kuwa somo hili lilianzishwa bila kuwaandaa walimu vilivyo inajitokeza.

Licha ya madai ya walimu kutoongozwa na silabasi ya mtalaa wa Isimujamii vilivyo, wataalamu wa elimu kutoka Taasisi ya Elimu Kenya (K.I.E.) wametofautiana nao. Kulingana na wataalamu hawa, walimu wanafaa kuongozwa na malengo ya ufundishaji wa stadi za kusikiliza na kuzungumza ya kila kidato yaliyotajwa katika silabasi (Taz. KIE, 2002: uk. 36-46). Kuna walimu wanaotazamia kuwa wanapofungua ukurasa fulani wa kitabu waanze kufundisha moja kwa moja bila kujiandaa kokote. Walimu wasitarajie orodha ya vipengele vya mtalaa wa Isimujamii wavifundishe na wanafunzi wawe wanavikariri kikasuku. Kulingana na mhimili wa nadharia ya Isimujamii unaosema kuwa **tofauti za lugha kijamii hutokana na tofauti za miundo ya kijamii zinazoletwa na elimu, tabaka, uana, umri na mielekeo (Labov, 1972)** ni wazi kuwa walimu kwa mfano wanaweza kudondoa shabaha ya (c) Uk. 31, inayosema kuwa, **"kustawisha mawasiliano yafaayo**

**kulingana na kaida za jamii**" na kufunza yaliyomo yatakayotekeleza lengo hili. Mhimili wa nadharia ya mawasiliano kuwa vipashio vya lugha sivyo vile vya kisarufi na kimuundo tu, lakini pia vile vya kimawasiliano linalipa wazo hili nguvu zaidi. Misingi hii basi inaweza kumwongoza mwalimu katika kufunza sajili kama "mazungumzo kati ya kijana na babu au mwalimu". Hata hivyo, kulingana na tahadhania ya utafiti huu kuwa somo hili liliandaliwa bila kuwaandaa walimu vilivyo, walimu hawawezi kuzingatia jambo hili. Wanafaa kuandaliwa kabla ya utekelezaji na kwa hivyo tahadhania hii inaendelea kupata mashiko.

Kufuatia madai ya walimu, wataalamu wa mitalaa kutoka K.I.E. wameilaumu Tume ya Kuwaajiri Walimu (T.S.C.) kwa kuwapa nyongeza ya mshahara walimu wa sayansi na lugha. Imebainika kuwa jambo hili liliwavutia walimu wengi kujisajilisha kwa masomo haya katika vyuo vikuu. Walimu walivutiwa na pesa lakini si kwa kuwa wapenzi wa lugha ya Kiswahili. Walipoajiriwa, wakawa wazembe kazini kwa vile talanta yao haikuwa kufundisha somo la Kiswahili. Imedaiwa kupitia utafiti huu kuwa, hawa ni baadhi ya walimu wanaosema hawawezi kujumuisha Isimujamii na kutafuta vipengele mwafaka vya kufundisha. Kasoro ilitokea katika maandalizi yao lakini si la wakuza mitalaa.

Aidha, walimu wametambua ubora wa mtalaa wa Isimujamii hasa kuambatana na mihimili ya nadharia za lugha ya mawasiliano na Isimujamii. Kozi hii itamwezesha mwanafunzi kuwa na ujuzi wa lugha kufuatia msisitizo wa vipengele vya

mawasiliano. Mwanafunzi atajua kuwa uchaguzi na matumizi ya lugha hutawaliwa na maumbo na miundo mipana ya kijamii na wala sio tu motisha na sababu za mzungumzi. Kwa mfano, matumizi ya lugha huathiriwa na **mazingira**, **kichwa cha mazungumzo**, **lugha azijuazo mtu**, **elimu**, **usuli au mbari**, **hali ya mtu**, **tabaka**, **wadhifa**, **kazi**, **mielekeo**, **tajriba**, **malezi**, **uana**, **umri** na **hadhira**. Ujuzi huu utampa mwanafunzi uwezo wa kuitumia lugha kulingana na muktadha au atakuwa na ujuzi wa kipragmatiki. Kufuatia haya, utafiti huu umeweza kuonyesha sifa zinazotawala matumizi ya lugha katika miktadha mbalimbali kulingana na mtalaa wa Isimujamii.

Hata hivyo, walimu wamedhihirisha kuwa mtalaa huu una udhaifu unaotinga utekelezaji wake. Kutokana na utafiti huu na mjadala uliomo, kuna ukosefu wa vitabu vya Isimujamii na vichache vinavyopatikana vina mada ngumu zinazolenga chuo kikuu. Zaidi ya hayo, hakuna kitabu mahsusi kilichoteuliwa na K.I.E. kutumiwa kufunzia Isimujamii katika shule za sekondari mpaka sasa. Utafiti huu ulipokuwa unaendelea, ilibainika kutoka kwa wataalamu wa mitalaa kutoka K.I.E. kuwa wameorodhesha vitabu vitano vya Isimujamii ili ukaguzi ufanywe ni kipi kitakachoteuliwa kutumiwa na shule zote. Mjadala huu unaendelea kupa mashiko tahadhania ya utafiti huu kuwa somo hili lina udhaifu unaotatiza utekelezaji.

Udhaifu mwingine unaotatiza utekelezaji wa Isimujamii ni kama vile mrundiko wa vipengele na upana wa somo, ugumu wa kujumuisha Isimujamii katika ufunzaji na



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

kutokuwa na uhakika kwa walimu ni vipengele vipi vinavyothaminiwa na kutahiniwa na Baraza la Mitihani Nchini (K.N.E.C.). Matatizo haya yote yanaathiri utendaji wa wanafunzi katika lugha ya Kiswahili.

Jambo lingine ambalo limebainika ni kuwa walimu na wataalamu wa elimu wanajua dhana na umuhimu wa mtalaa katika ufundishaji. Imebainika kuwa, walimu wanaotofautiana kuhusu ni nani mwenye jukumu la kuunda na kuandaa mitalaa, kati ya K.I.E. na K.N.E.C. Jambo hili linafaa kuwekwa wazi kwao ili wajue watapata usaidizi kutoka kwa nani wanapokabiliana na matatizo ya utekelezaji. Lakini kupitia utafiti nyanjani katika Taasisi ya Elimu Nchini Kenya (K.I.E.) ilithibitika kuwa ndiyo iliyo na jukumu la kutayarisha, kusambaza na kufanyia utafiti mtalaa wa taifa nzima na vifaa vyote vya kufundishia mtalaa wowote ule.

Utafiti umeweza kuonyesha maoni ya walimu na wataalamu wa mitalaa kuhusu hatua zinazofuatwa katika uundaji na utayarishaji wa mtalaa na athari zake katika utekelezaji wa mtalaa huo. Hatua hizi ambazo kulingana na Taasisi ya Elimu Nchini Kenya (K.I.E.) ni nane na ni za kiduara, hujengana na hukamilishana. Hatua ya kwanza ya **kutathmini mahitaji** ilikuwa na kasoro kwa vile walimu hawakuhusishwa. Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha uwiano mkubwa wa hatua hii na mihimili ya nadharia za Isimujamii na ya lugha ya mawasiliano. Misingi ya nadharia hizi imeonyesha matakwa ya wanafunzi wa lugha. Kulingana na walimu, wao ndio wanaojua mahitaji ya wanafunzi wa L2 na kwa hivyo wangekuwa malighafi

muhimu katika hatua hii. Wangewaonyesha wakuza mitalaa yaliyomo ambayo yangeongezwa katika lugha ya Kiswahili yanayohusu Isimujamii na vitabu mwafaka vya marejeleo. Vitabu vya Kiswahili vingekuwa na mada chini ya stadi za kusikiliza na kuzungumza ambazo zimejumuisha sajili mbalimbali za lugha. Sajili hizi ndizo wangezifundisha kama Isimujamii. Msisitizo ungewekwa katika ufafanuzi wa maana wa miundo ya sajili hizo ili kuzingatia lengo la lugha ya mawasiliano badala ya kusisitiza usarufi wa sajili hizo. Hii ni ithibati nyingine ya tahadhania ya utafiti huu *kuwa mtalaa wa Isimujamii una udhaifu mwingi na haumwongozi mwalimu.*

Vile vile, imebainika kuwa, **uundaji wa mradi wa mtalaa** ni hatua ambayo ikiwa walimu wangeshirikishwa kwayo, wangeweza kubainisha na kufafanua malengo ya elimu na malengo ya yaliyomo katika lugha ya Kiswahili. Kulingana na msingi wa nadharia ya lugha ya mawasiliano, madhumuni makuu ya lugha ni kuwasiliana kwa vile lugha ni mfumo wa kueleza maana, ilibainika kutoka kwa walimu mtalaa wa lugha ya Kiswahili haukutimiza lengo hilo. Lengo hili lingebainika zaidi katika hatua hii na wangependekeza yaliyomo ambayo yangelitimiza na sababu hii huenda ikafanya walimu kuendelea kufundisha miundo au sarufi.

Vitabu, uandishi wa silabasi, semina za uandishi, miongozo ya walimu na makala ya walimu kwa ujumla hushughulikiwa na hatua ya **upangaji wa mitaala** ambapo walimu wamedai hawajaweza kupata vifaa hivi vilivyotajwa. Zaidi ya hayo yaliyopendekezwa kufundishwa katika hatua hii ni kikwazo cha ujifunzaji wa L2.



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

Vile vile, yaliyomo kama vile Sheng' ni kikwazo kikubwa kwa wanafunzi wa mashambani ambao hawajazoea msimbo huu. Hii vile vile ni ithibati tosha ya tahadhia ya utafiti huu kuwa walimu hawakuandaliwa vyema kufundisha somo hili. Hii ni kwa sababu wangeshirikishwa katika uandishi wa silabasi, semina za uandishi na pia katika utayarishaji wa miongozo ya walimu mambo ambayo hayakufanyika.

Hatua ya **majaribio** ingefichua udhaifu wa mtalaa huu na utafiti huu ulithibitisha kuwa mtalaa huu haukuipitia. Hali kadhalika, hatua ya **tathmini** imevutia hisia tofuati na walimu wamesema wanangojea kama Taasisi ya Elimu Kenya (K.I.E.) itatoa taarifa yoyote kuhusu kufaulu au kutofaulu kwa mtalaa wa Isimujamii.

Utafiti huu hata hivyo umebainisha kutoka kwa wakuza mitalaa wa K.I.E. kuwa, ingawa hatua zote saba ni muhimu katika kutayarisha mtalaa wowote ule, siyo lazima mtalaa upitie zote au walimu kushirikishwa. Kulingana nao, ikiwa somo nzima litafanyiwa marekebisho, ni lazima lipitie hatua zote. Ikiwa mtalaa unahusu marekebisho ya sehemu moja, hatua zote siyo lazima zihusike na marekebisho kama hayo. Mfano mzuri ni katika utafiti huu ambapo Isimujamii ni kitengo cha Isimu au lugha ya Kiswahili. Mtalaa huu ulipitia hatua kadhaa lakini hatua kama vile majaribio haikuwa muhimu kwa sababu tayari lugha ya Kiswahili ilikuwa inafundishwa. Vile vile, si kumaanisha Isimujamii haikuwa inafundishwa bali ni kwa vile ilionekana kuna umuhimu wa kuhimiza ujifunzaji na umilisi wa mawasiliano. Kupitia misingi ya nadharia ya lugha ya mawasiliano na Isimujamii, umilisi

mawasiliano ni ujuzi wa vikwazo vya kijamii utakaomfanikisha mwanafunzi katika kutumia lugha kwa njia ya kuridhisha na kufurahisha. Kwa kusisitiza, mwanafunzi atahitajika kumiliki sheria za kisarufi (umilisi lugha) sambamba na sheria za matumizi ya lugha kulingana na vikwazo vya kijamii (umilisi mawasiliano).

Imethibitika pia kuwa, maandalizi ya walimu ni muhimu sana katika utekelezaji wa mtaala mpya. Semina na makongamano huwapiga msasa walimu na kuweza kushughulikia somo hilo vizuri. Walimu hawa wameweza kujumuisha Isimujamii katika kazi zao za kufundisha somo la Kiswahili. Hata hivyo kutokuwa na uwezo wa kiuchumi katika zile shule ndogo kunawanyima walimu fursa za kuhudhuria semina za kuwaandaa kufunza mtalaa mpya.

Vipindi vichache na majukumu ya walimu na ukosefu wa vifaa imegunduliwa kutoka kwa walimu kuwa ni mambo yanayotinga utekelezaji wa Isimujamii. Vipindi vilivyotengewa somo la Kiswahili havitoshi kwa vile somo hili ni pana. Kuna fasihi, lugha yenyewe, insha na Isimujamii na upana huu unatinga utekelezaji wa mtalaa huu.

Utafiti huu utaweza kuwafaida watu kadhaa. Kati ya watakaofaidika ni wadau katika sekta ya elimu. Kupitia malengo ya utafiti huu, sifa mbalimbali zinazotawala matumizi ya lugha zimedhihirika kwa kuangalia sajili mbalimbali. Sajili hizi ni zile ambazo zimependekezwa kufunzwa kama yaliyomo na mtalaa huu. Kwa hivyo,

walimu watapata mawanda ya kushughulika kwa uwazi zaidi. Wanafunzi nao watafaidika kwa vile baada ya kufundishwa watakuwa na ujuzi wa vikwazo vya kijamii utakaowafanikisha katika kutumia lugha yenye kuridhisha (umilisi mawasiliano). Katika kujadili jambo hili kwa hivyo, lengo la utafiti huu la kubainisha mchango wa Isimujamii katika mtalaa wa elimu kwa wanafunzi wa sekondari limeafikiwa.

Utafiti huu pia umebainisha maoni ya walimu na wakuza mitalaa wa somo la Kiswahili kuhusu maudhui ya mtalaa wa Isimujamii na vigezo vilivyotumiwa katika uandalizi wake. Matokeo haya yatasaidia Taasisi ya Elimu Kenya (K.I.E.), Baraza la Mitihani Kenya (K.N.E.C.) na Idara ya Kudhibiti Ubora wa Elimu kuelewa nafasi yao katika utekelezaji wa mtalaa mpya wa Isimujamii. Taasisi hizi zitakuwa tayari kufuata taratibu zinazofaa wakati wa kuanzisha mtalaa mwingine mpya.

Utafiti huu pia utafaidi **sera** na **upangaji wa lugha**. Upangaji wa lugha unamaanisha harakati zenye utaratibu zinazonuiwa kutafuta utatuzi wa matatizo ya lugha katika kiwango cha Kitaifa (Taz. Buliba, Njogu na Mwihaki (2006), Masinde (2007) na Mathooko (2007). Kama ilivyotajwa awali, moja kati ya majukumu ya Isimujamii ni kutafuta mikakati ya kutatua shida za mawasiliano katika jamii, hususan jamii zenye lugha nyingi au kama ilivyobainika matumizi ya Sheng' miongoni mwa vijana ambao wanasoma. Katika nchi zenye lugha nyingi, mpango wa lugha huhitajika ili kupata lugha itakayotumika kikamilifu kwa manufaa ya wanaohusika. Katika hali ya lugha

nyingi, huhitajika sera maalum inayoelekeza matumizi ya lugha katika mawanda ya kiuchumi, elimu, shughuli rasmi na uelewano unaokuza umoja kitaifa. Upangaji huu wa lugha na sera ya lugha unaweza kufanywa kufuatia matokeo na mapendekezo ya utafiti huu. Serikali inaweza kuwa na lugha moja itakayotumiwa nchini kupitia kuifunza shuleni na kwa hivyo inaweza kutumia vigezo vya uandalizi wa mitalaa vilivyojadiliwa pamoja na maoni ya walimu kufikia lengo hili.

## 5.3 MAPENDEKEZO

Kutokana na matokeo ya utafiti huu, ni wazi kuwa kuna mambo mengi yanayoweza kufanywa ili kufanikisha utekelezaji wa mtalaa mpya wa Isimujamii katika shule za upili nchini Kenya. Mambo yafuatayo yanapendekezwa katika utafiti huu.

Mosi, kuhusu vifaa na vitabu vya kufundishia, walimu wanafaa kumakinika katika matumizi ya kompyuta na mtandao wa mawasiliano kama nyenzo ya kufundishia Isimujamii. Vitabu na miongozo itayarishwe na iteuliwe inayolenga kiwango cha wanafunzi wa sekondari itayarishwe na kuteuliwa. Zaidi ya hayo, njia mwafaka za kufundishia Isimujamii au L2 zigunduliwe kwa vile ukariri wa miundo ya lugha hautoshi bali umepitwa na wakati. Ikiwa ufundishaji wa lugha ya mawasiliano utaimarika, mbinu kama vile maigizo, kazi mradi, uvumbuzi na utatuzi wa mambo hazina budi kutumiwa.

Pili, warsha, semina na mafunzo maalum yapangwe kwa ajili ya kuwapiga msasa walimu wote wa Kiswahili wa shule za upili kuambatana na mahitaji ya mtalaa mpya wa Isimujamii. Katika mkabala huu basi, inapendekezwa kuwa warsha hizi zisiwe za siku moja bali ziwe zinaandaliwa angalau kwa mwezi mmoja wakati wa likizo. Itakuwa ni sharti walimu wahudhurie na baada ya kozi hiyo, wapewe vyeti vya kuthibitisha kuwa walihudhuria na wanaweza kutekeleza mtalaa huu vizuri. Walimu watakaoajiriwa baadaye pia wahakikishwe kuwa wamepitia mafunzo hayo. Katika warsha hizo pia, asasi kama vile Baraza la Mitihani la Kenya (K.N.E.C.) na Taasisi ya Elimu Kenya (K.I.E.) zitume wawakilishi wao ambao watawaelezea walimu matarajio yao katika Isimujamii.

Tatu, vyuo vya walimu, vyuo vikuu na asasi za kukuza na kutekeleza mitalaa kama vile Taasisi ya Elimu ya Kenya, Idara ya Kudhibiti Ubora wa Elimu na Baraza la Mitihani washirikiane kuandaa mafunzo mwafaka ya Isimujamii ili mwalimu akihitimu vyuo hivyo awe amejiandaa vilivyo kufunza Isimujamii. Ingekuwa bora asasi hizo zikinadi na kuwatayarisha walimu wa Kiswahili ambao lengo lao ni kufunza lugha kwa lengo la kukuza uwezo wa wanafunzi wa kuwasiliana na siyo tu kupita mtihani.

Pia, inapendekezwa kuwa Taasisi ya Elimu Kenya iliyopewa wajibu wa kuteua vitabu mwafaka vya kufundishia mtalaa fulani iteue vitabu mahsusi vitakavyotumiwa na walimu kufunzia Isimujamii. Uteuzi wa vitabu hivyo unafaa kufanywa kwa

kuzingatia misingi ya lugha ya mawasiliano na Isimujamii. Fauka ya hayo, maoni ya walimu na matarajio ya wakuza mitalaa yapewe kipaumbele katika uteuzi huo. Vitabu hivyo vinafaa vilenge kiwango cha wanafunzi wa shule za upili.

Aidha, inapendekezwa kuwa somo la Kiswahili liongezewe vipindi viwili rasmi kwa sababu vipindi vitano havitoshi kushughulikia upana wa somo hili. Mwalimu wa Kiswahili anatarajiwa kushughulikia lugha ya Kiswahili na fasihi ambapo katika lugha yenyewe mna ufahamu, matumizi ya lugha, muhtasari na Isimujamii. Katika fasihi kuna fasihi simulizi na fasihi andishi ambapo ameteuliwa vitabu ambavyo atavihakiki pamoja na wanafunzi wake na pia mashairi. Upana huu haumruhusu mwalimu kushughulikia somo la Isimujamii vizuri.

Isitoshe, utafiti huu unapendekezea Tume ya Kuwaajiri Walimu (T.S.C.) iruhusu walimu wa Kiswahili kuchukua kozi ya somo moja pekee la kufundisha baada ya kuhitimu. Hata ingawa ilivyo sasa Tume hii imesema ni lazima walimu wote wasomee masomo mawili na hata walimu wa Kiingereza, itabidi waghairi msimamo wao na wawakubalie walimu wa lugha kushughulikia somo hilo pekee. Hii ni kuambatana na matokeo ya utafiti huu kuthibitisha kuwa ikiwa Isimujamii itafundishwa kwa lengo la kuinua uamilifu wa mawasiliano na kwa kuona upana wa somo la Kiswahili, basi itabidi walimu wasomee na wafundishe somo la Kiswahili pekee.

Pendekezo lingine linaloweza kutatua utekelezaji wa mtalaa wa Isimujamii na mtalaa mwingine mpya unaonuiwa kuanzishwa ni kwamba, mtalaa unapofanyiwa mageuzi wadau wote washirikishwe kikamilifu na majaribio yafanywe kabla haujatumiwa katika shule.

Ili kuondoa na kuzuia utekelezaji wa mtalaa wa Isimujamii wenye udhaifu na athari zake, inapendekezwa kuwa utafiti ufanywe nchini ili kufichua matatizo ya mtalaa huu na kuyatafutia ufumbuzi. Kati ya mambo muhimu ya kuchunguzwa ni pamoja na mrundiko na uchangamano wa mada, ujumuishaji katika ufunzaji na upana wa somo.

Utafiti huu ulihusu uchunguzi wa mtalaa wa Isimujamii katika shule za upili kama kipengele kipya katika lugha ya Kiswahili. Utafiti zaidi unaweza kufanywa kuhusu utendaji wa wanafunzi katika Kiswahili. Utafiti kama huu unaweza kuchunguza iwapo utendaji wa wanafunzi uliimarika baada ya kutekelezwa kwa mtalaa wa Isimujamii katika lugha ya Kiswahili tofauti na yale tuliyoyashughulikia. Matokeo ya utafiti wa aina hii yatawasaidia walimu na washikadau wengine katika elimu kufanya marekebisho kiutekelezaji.

Utafiti huu pia ulilenga jinsi yaliyomo katika Isimujamii yanavyotekelezwa. Utafiti mpana waweza kufanywa kuhusu namna walimu na wakuza mitalaa wanavyoweza kutahini stadi za maongezi (oral skills) za wanafunzi kutokana na kufunzwa kwao Isimujamii. Utafiti kama huu utakuwa na mchango katika taaluma ya lugha kwa vile

utasaidia kuimarisha ufunzaji na ujifunzaji wa lugha ya mawasiliano. Jambo hili likitekelezwa, laweza kuongeza uelewa na ujuzi wa wanafunzi katika taaluma ya fonetiki, semantiki na sintaksia.

Kwa vile utafiti huu umezingatia shule za upili, hasa katika wilaya ya Thika, inapendekezwa utafiti zaidi ufanywe katika sehemu zingine ili kuona iwapo matatizo ya kiutekelezaji ya mtalaa mpya wa Isimujamii katika shule za upili yanafanana. Aidha, ni muhimu pia kuzingatia nadharia zingine tofauti na zile zilizotumiwa katika utafiti huu.

**MAREJELEO**


Angiella, O. (2002). "Literacy, Attitudes and Language Revitalization: The Case of Suba in Kenya." Katika Owino, F. (Mh.)

Aswani, B., Njogu, K. na Mwihaki, A. (2006). *Isimujamii kwa Wanafunzi wa Kiswahili.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Benaars, G.A., Otiende, J.E. na Boisvert, R. (eds.) (1994). *Theory and Practice of Education*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Besha, R. (1994). *Utangulizi wa Lugha na Isimu*. Dar-es-Salaam: Dar es Salaam University Press.

Bishop, G. (1985). *Curriculum Development: A Textbook for Students*. London: Macmillan Education Ltd.

Chesire, J. and Trudgill, P. (1968). *Gender and Discourse. The Sociologuistic Reader.* London: Arnold.

Chomsky, N. (1965). *Aspects of the Theory of Syntax*. Cambridge: Massachusettes Institute of Technology.

Eaton, J. (1975). *An ABC of the Curriculum*. Edinburgh: Oliver and Boyd.

Fasold, R. (1984). *The Socio-linguistics of Society*. Oxford: Basil Blackwell.

_________(1990). *The Socio-linguistics of Language*. Oxford: Basil Blackwell.

Fishman, J. (1968). *Readings in the Sociology of Language*. The Hague: Mouton.

Gathumbi, A. na Masembe, S. (2005). *Principles and Techniques in Language Teaching: A Text for Teacher Educators, Teachers, and Pre-service Teachers*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Giles, H. (1975). *Logic and Conversation*: *Syntax and Semantics*. New York: Academic Press.

Government of Kenya. *The Mackay Report*. (1981) Nairobi: Government Printer.

Groenewegen, T. (ed.) (2008). *Benchmarks for English Language Education*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Gumperz, J. Hymes, D. (1972). *Directions in Sociolinguistics: The Ethnography of Communication*. USA: Basil Blackwell.

Halliday, M. (1964). *The Linguistic Science and Language Teaching*. London: Longman.

Halliday, M. (1985). *An Introduction to Functional Grammar*. London: Edward Arnold.

Halliday, M. (1994). *An Introduction to Functional Grammar*. 2nd Edition. London: Oxford University Press.

Hawes, H. (1979). *Curriculum and Reality in the African Primary School*. London: Longman.

Holsay, R. (2001). *Teach Yourself: 101 Key Ideas, Linguistics*. UK. Hodder Headline.

Howatt, A. (1984). *A History of English Language Teaching*. Oxford: Oxford University Press.

Hudson, R. (1980). *Sociolinguistics*. New York: Cambridge University Press.

Hymes, D. (1971). *On Communicative Competence*. Philadelphia: University of Pennysyvania Press.

Johnson, K. (1982). *Communicative Syllabus Design and Methodology*. Oxford: Pergamon Institute of English.

Kerr, F. (1968). "All the Learning Planned and Guided by the School." In Kerr, J.F. (Ed.) *Changing the Curriculum*. London: University of London Press.

Kihara, D. (2006). "Uchambuzi wa Matini: Matumizi ya Lugha katika sajili ya Matatu". Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Lawton, D. (1973). *Social Change, Educational Theory and Curriculum Planning*. London: University of London Press Ltd.

Lopez, L. (2000). *Cognition, Culture, Language and Learning: An Introduction for Educational Planners in Multilingual and Multicultural Contexts. In Distance Learning Course on the Language of Instruction in Basic Education*. (November 27, 28, 29, December 1, 2000).

Masinde, E. (2007). *Mawanda ya Isimujamii*. Nairobi: Taaluma Publishers.

Mathooko, P. (2004). "Towards An Integrative Perspective of Linguistic Accommodation: A Case of Kikamba and Kitharaka". Tasnifu ya Uzamifu ambayo haijachapishwa, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Mathooko, P. (2007). *Isimujamii: Misingi na Nadharia*. Nairobi: Njigua Books.

Mbaabu, I. (1985). *Kiswahili Lugha ya Taifa*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

_________ (1996). *Language Policy in East Africa: A Dependency Theory Perspective*. Nairobi: Educational Research and Publications.

McDonough, J. and Shaw, C. (1993). *Materials and Methods in ELT: A Teachers Guide*. Oxford: Blackwell Publishers Ltd.

Menya, J. (1977). "Importance of Curriculum Development in Education Advancement". Lecture Delivered at the Inservice Course for teachers organised by K.N.U.T. at Machakos T.T.C. on Saturday, 13th August, 1977 at 9.30a.m.

Milroy, L. (1987). *Observing and Analyzing Natural Language. A Critical Account of Sociolinguistic Method*. Oxford: Basil Blackwell.

Ministry of Education, Science and Technology (2002). *Secondary Education Syllabus, Volume One*. Nairobi: Kenya Institute of Education.

Ministry of Education, Science and Technology (2006). *Teachers Handbook*. Nairobi: Kenya Institute of Education.

Momanyi, C. (2001). "Matumizi ya Kiswahili katika Njia Panda: Mtazamo wa Kiisimu-Jamii." Makala katika Kiswahili – A TOOL FOR DEVELOPMENT. THE MULTIDISCIPLINARY APPROACH. Chakita, Moi University.

Mugenda, O. na Mugenda, A. (1999). *Research Methods. Quantitative and Qualitative Approaches*. Nairobi: Kenya Act Press.

Muiruri, P. na Ndegwa, D. (2005). *Isimujamii: Toleo la Tatu: K.C.S.E. Silabasi Mpya*. Nairobi: Akapuko Kikuyu.

Musau, P. (1993). *Aspects of Interphonology:The Study of Kenyan Learners Swahili*. Bayrenth: Bayrenth African Study.

Musau, P. na Chacha L. (2001). *Mbinu za Kisasa za Kufundishia Kiswahili. Kwa Walimu wa Shule Msingi, Upili na Vyuo*. Nairobi: Kenya Literature Bureaus.

Muthui, N. (2002). "KNUT cautions teachers against going on strike". Katika East African Standard, tarehe 06-10-2002.

Muthwii, M. (2002). *Language Policy and Practices in Education in Kenya and Uganda*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Odeo, I. (2007). "Utekelezaji wa Silabasi Mpya ya Somo la Kiswahili katika Shule za Upili: Mtazamo wa Walimu". Katika Njogu, K. (Mh.) *Kiswahili na Elimu Nchini Kenya*. Limuni:Kolbe Press.

Okech, J. (1992). *Curriculum Development for Schools*. Nairobi: Educational Research and Publications Ltd.

__________ (1990). "Research Report on Analysis of Curriculum Problems in Kenya and Their Influence on the Teachers' Decision-Making about Subject-Matter to be Taught". Unpublished, Kenyatta University.

Oluoch, P. (2002). *Essentials of Curriculum Development*. Bondo: Bondo Bookshop Limited.

Onyango, J. (1990). "Mielekeo ya Wasomi kuhusu matumizi ya Kiswahili Nchini Kenya". Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Rivers, W. (1983). *Communicting Naturally in a Second Language; Theory and Practice in Language Teaching*. Cambridge: Cambridge University Press.

Scotton, C. (1967). *A look at Swahili of Two Groups of Upcountry Speakers of Swahili*, Journal of Institute of Swahili Research JZ la 39/1.

Scotton, M. (1993). *Social Motivations for Code Switching: Evidence from Africa*. Oxford: Claredon Press.

Seliger, W. na Shohamy, E. (1989). *Curriculum Theory and Practice in Kenya*. Nairobi: Oxford University Press.

Shiundu, J. na Omulando, J. (1992) *Curriculum Theory and Practice in Kenya*. Nairobi: Oxford University Press.

Sifuna, D. (1980). *Short Essays on Education in Kenya*. Kenya Literature Bureau: Nairobi.

Spolsky, B. (1989). *Conditions for Second Language Learning*. Oxford: Oxford University Press.

Taba, H. (1975). *Curriculum Development Theory and Practice.* New York: Harcourt Brace and World.

Tanner, D. (1971). *Secondary Curriculum: Theory and Development.* New York: The Macmillan Co.

Tyler, R. (1949). *Basic Principles of Curriculum and Instruction.* Chicago Press.

Wanyoike, E. (1978). *Vikwazo katika mafunzo ya Kiswahili Nchini Kenya.: Lugha Journal for Language Teachers Kenya.* Nairobi JZ la 5, 35-42.

Wenyaa, N. (2007). "Athari ya Duksi katika ufunzaji na Ujifunzaji wa Kiswahili. Mtazamo wa Uchanganuzi Linganishi". Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Whiteley, W. (1974). *The Classification and Distribution of Kenya's African Languages.* Nairobi: Oxford University Press.

Willis and Willis (1996). *Challenge and Change in Language Teaching.* Oxford: Heineman.

Yule, G. (1996). *Pragmatics.* London: Oxford University Press.

## KIAMBATISHO I

## MASWALI YA MAHOJIANO KWA WALIMU

Jina -------------------------------------------------------------------------------------

Kidato unachofundisha: --------------------------------------------------------------

Aina ya shule (Taja ya kitaifa au ya mkoa) --------------------------------------

**Jinsia: ----------------------------------------------------------**

A. (i) Eleza kama unajua dhana ya mtalaa na hatua za kubadilisha mitalaa ----------------------------------------------------------------------

----------------------------------------------------------------------------------

----------------------------------------------------------------------------------

(ii) Unafikiria silabasi hii mpya ya Isimujamii ina udhaifu wowote? Toa sababu za kusema hivyo.

----------------------------------------------------------------------------------

----------------------------------------------------------------------------------

(iii) Baada ya somo hili kupendekezwa, umekumbana na matatizo katika ufundishaji?

----------------------------------------------------------------------------------

----------------------------------------------------------------------------------

----------------------------------------------------------------------------------

----------------------------------------------------------------------------------

----------------------------------------------------------------------------------

(iv) Je, unafikiria silabasi imekuongoza vilivyo kufundisha vipengele vya Isimujamii chini ya stadi za kusikiliza na kuzungumza?

--------------------------------------------------------------------------------

--------------------------------------------------------------------------------

(i) Kuna maandalizi uliyopata kutoka kwa Wizara ya Elimu kuhusu mtalaa huu wa Isimujamii kabla ya utekelezaji? Fafanua.

------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------

(ii) Toa mapendekezo ya jinsi ya kuboresha mtalaa wa Isimujamii kwa Wizara ya Elimu.

(a) ---------------------------------------- (d) -----------------------

(b) ---------------------------------------- (e) -----------------------

(c) ----------------------------------------

B. (i) Una maoni gani kuhusu vifaa na vitabu vya kufundishia mtalaa huu?

--------------------------------------------------------------------------------

--------------------------------------------------------------------------------

--------------------------------------------------------------------------------

--------------------------------------------------------------------------------

--------------------------------------------------------------------------------

--------------------------------------------------------------------------------

(ii) Ni njia zipi za kufundishia Isimujamii unazotumia?

--------------------------------------------------------------------------------

--------------------------------------------------------------------------------

--------------------------------------------------------------------------------

--------------------------------------------------------------------------------

--------------------------------------------------------------------------------

--------------------------------------------------------------------------------

(iii) Unafikiria muda uliotengewa kufundisha Isimujamii watosha?

--------------------------------------------------------------------------------

--------------------------------------------------------------------------------

--------------------------------------------------------------------------------

--------------------------------------------------------------------------------

--------------------------------------------------------------------------------

--------------------------------------------------------------------------------

## KIAMBATISHO II

**KIONGOZI CHA MASWALI NA AFISA ANAYEHUSIKA NA UANDALIZI WA MITALAA NA UTEUZI WA YALIYOMO YA SOMO LA KISWAHILI KATIKA TAASISI YA ELIMU KENYA**

A. Kuna tofauti gani kati ya silabasi na mtalaa?

i. ____________________

ii. ____________________

iii. ____________________

B. Una maoni gani kuhusu silabasi ya sasa yenye mtalaa wa Isimujamii ambayo haimwongozi mwalimu katika ufundishaji wa Isimujamii?

i. ____________________

ii. ____________________

iii. ____________________

iv. ____________________

C. Kwa nini hamjateua vitabu mahsusi vya kufundishia Isimujamii katika shule za upili?

i. ____________________

ii. ____________________

iii. ____________________

D. Unafikiria ni kwa nini walimu hawakushirikishwa katika mageuzi ya mtalaa mpya wa Kiswahili ya shule za upili?

i. ____________________

ii. ____________________

iii. ____________________

iv. ____________________

E. Je, Isimujamii haikuwa inafundishwa katika mtalaa huo wa awali wa lugha ya Kiswahili?

____________________

____________________

____________________



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY